

MTINDO KATIKA KAZI ZA KUBUNI ZA LEONARD SANJA

NA

NYUTU WANJIKU JACQUELINE

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA  
YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2016

## **UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kingine.

Sahihi \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

Nyutu Wanjiku Jacqueline  
(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi – Idara ya Kiswahili.

Sahihi \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

Dkt. Evans Mbuthia  
(Msimamizi)

Sahihi \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

Dkt. Amiri Swaleh  
(Msimamizi)

## **TABARUKU**

Ninaitabarukia tasnifu hii wazazi wangu: John Nyutu Njihia na Purity Njeri Nyutu. Pia mume wangu mpendwa James Lemereige, binti yangu Velcon Lemereige na Mark Lemereige

## **YALIYOMO**

Ungamo.....	ii
Tabaruku .....	iii
Yaliyomo.....	iv
Shukrani .....	vii
Ikisiri.....	viii

## **SURA YA KWANZA**

1.1 USULI WA MADA .....	1
1.2 SWALA LA UTAFITI.....	2
1.3 MALENGO YA UTAFITI .....	2
1.4 NADHARIA TETE.....	3
1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA .....	3
1.6 UPEO NA MIPAKA.....	3
1.7 MSINGI WA KINADHARIA .....	4
1.7.1 Utangulizi .....	4
1.7.1 Sura Tofauti za Nadharia ya Umitindo.....	6
1.7.1.1 Kiwango cha Maandishi au Grafolojia.....	6
1.7.1.2 Kiwango cha Umbo.....	7
1.7.1.3 Kiwango cha Kisemantiki .....	7
1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA .....	8
1.9 MBINU ZA UTAFITI.....	11

## **SURA YA PILI**

### **MTINDO NA TANZU ZA FASIHI ANDISHI**

2.1 Utangulizi .....	12
2.1.1 Mtazamo wa Kiisimu .....	12
2.1.2 Mtazamo wa Kifasihi .....	13
2.1.3 Mtazamo wa Kifasihi na wa Kiisimu .....	13

2.1.4 Mtazamo wa Mtindo kama Mtu Binafsi.....	15
2.2.1 Mtindo katika Tanzu mbalimbali za Fasihi Andishi .....	17
2.2.2 Riwaya.....	18
2.2.3 Tamthilia .....	20
2.2.4 Hadithi Fupi.....	21
2.3 Hitimisho.....	24

### **SURA YA TATU**

#### **UCHANGANUZI WA TAMATHALI ZA USEMI KATIKA “MIMBA INGALI MIMBA”, “MWAVYAJI WA ROHO”, ZINGUO LA MZUKA NA YASINYA**

3.1 Utangulizi .....	26
3.1.1 Majazi.....	26
3.1.1.1 Majazi katika “Mwavyaji wa Roho” (2011) .....	27
3.1.1.2 Majazi katika <i>Zinguo la Mzuka</i> (2011) .....	31
3.1.1.3 Majazi katika Yasinya (2014) .....	35
3.2.1 Jazanda na Istiari .....	47
3.2.1.1 Jazanda na Istiari katika “Mimba Ingali Mimba” .....	47
3.2.1.2 Jazanda katika “Mwavyaji wa Roho” (2011).....	49
3.2.1.3 Jazanda katika <i>Zinguo la Mzuka</i> .....	51
3.2.1.4 Jazanda katika <i>Yasinya</i> .....	52
3.3.1 Ndoto.....	56
3.3.1.1 Ndoto katika Yasinya .....	56
3.3.1.2 Ndoto katika <i>Zinguo la Mzuka</i> .....	61
3.4.1 Kinaya .....	62
3.4.1.1 Kinaya katika “Mimba Ingali Mimba” .....	62
3.4.1.2 Kinaya katika “Mwavyaji wa Roho” .....	63
3.4.1.3 Kinaya katika <i>Zinguo la Mzuka</i> .....	64

3.4.1.4 Kinaya katika Yasinya.....	67
3.5.1 Maswali ya Balagha.....	68
3.5.1.1 Maswali ya Balagha katika “Mimba Ingali Mimba” .....	68
3.5.1.2 Maswali ya Balagha katika “Mwavyaji wa Roho” .....	70
3.5.1.3 Maswali ya Balagha katika <i>Zinguo la Mzuka</i> .....	71
3.5.1.4 Maswali ya Balagha katika <i>Yasinya</i> .....	73
3.6 Hitimisho.....	77

### **SURA YA NNE**

#### **MTINDO WA SANJA KATIKA YASINYA, ZINGUO LA MZUKA, “MIMBA INGALI MIMBA” NA “MWAVYAJI WA ROHO”**

4.1 Utangulizi .....	79
4.1.1 Hisia za Mwandishi .....	80
4.1.2 Usimulizi .....	81
4.1.3 Uteuzi wa Msamiati.....	82
4.1.4 Muundo wa Kazi .....	82
4.1.5 Uchanganyaji wa Tanzu Mbalimbali .....	83
4.6 Hitimisho.....	84

### **SURA YA TANO**

#### **HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.1 Utangulizi .....	86
5.2 Muhtasari wa Matokeo.....	86
5.3 Hitimisho.....	88
5.4 Mapendelekezo .....	88

## **SHUKRANI**

Ninampa mwenyezi Mungu utukufu na adhama kwa neema zake katika safari hii ambayo haijakuwa rahisi. Amenineemesha na kuniwezesha kuifanya kazi hii na kuifanya ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili kutimia.

Ninawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Evans Mbuthia na Dkt. Amiri Swaleh ambao wamenifaa kwa uelekezi, ushauri na uvumilivu wao. Wamenitia moyo hasa kwa kuwepo nilipowahitaji na kunihimiza nilipolemewa.

Wahadhiri wa Idara ya Kiswahili wamechangia pakubwa katika kufanikiwa kwangu. Ninawashukuru Prof. Habwe, Prof. Iribé, Prof. Mutiso, Dkt. Mukhwana, Prof. Mbatia, Dkt. Zaja, Dkt. Mweri, Dkt. Jerono na mwalimu Ndung'u. Kwa njia ya kipekee ninawashukuru Prof. Iribé, na Dkt. Mukhwana kwa changamoto walijonipa katika mwaka wangu wa kwanza.

Ninawashukuru wanafunzi wenzangu kwa ushirikiano wao katika masuala ya kiusomi na ya kijamii. Kwa hakika wamekuwa marafiki wa dhati kwa mchango waliota katika maisha yangu. Hawa ni: Muchiri, Njeri, Bosibori, Simon, Mutali, Asha, Zahra, Agnes, David, Kimetto, Zaar, Winny, Faith, Adeline, Caroh, Emily, Florence, Asiko, Lilian, Jared, Jayson na wengine.

Familia yangu imechangia pakubwa katika ufanisi wangu kwa hali na mali. Ninamshukuru mume wangu mpendwa, James Lemerige kwa kuwa mhimili mkuu katika maisha yangu na pia katika masomo yangu. Ninawashukuru wanangu Velcon na Mark ambao wamenishajiisha kusoma ili niwe mfano mwema kwao. Waliniombea kila siku na ninawashukuru. Ninawashukuru Wazazi wangu kwa kuwa waliniwekea msingi wa masomo na hata maswala ya kidini. Siwezi kuwalipa lakini ninamwomba Mungu awajalie maisha marefu yaliyojaa baraka. Ninamshukuru dadangu Patricia Njoki kwa kunipa makao siku zote nilizokuja Nairobi kwa masomo, Mungu akubariki sana. Siwezi kuwasahau ndugu zangu Stephen, Caro, Ken, Willy, Rose, Joan na Mark. Ninawashukuru kwa maombi yenu. Mungu awajalie mema na neema zake ziwatoshe. Ninamshukuru mhubiri wangu Charles Mutua na mkewe Naomi Ndolo kwa maombi na mawaiidha walijonipa kuhusiana na masomo yangu. Ninamshukuru rafiki yangu Ambuki kwa ushauri wake na kuwa tayari kunisaidia kila wakati nilipomhitaji. Mungu awaneemeshe kwa kujitolea kwenu.

Utukufu na adhama kwa Mwenyezi Mungu.

## **IKISIRI**

Katika tasnifu hii tulichunguza mtindo katika kazi za kubuni za mwandishi Leonard Sanja. Kazi hizi ni “Mimba Ingali Mimba” katika *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (mh McOnyango) (2006), “Mwavyaji wa Roho” katika *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (mh Sanja) (2011) (hadithi fupi), *Zinguo la Mzuka* (2011) (tamthilia), *Yasinya* (2014) (riwaya). Tulitumia nadharia ya Umitindo kuchanganua kazi hizi nne kitaaluma. Tasnifu yetu ina sura tano. Katika sura ya kwanza tulieleza swala la utafiti ambalo lilikuwa kuchunguza mtindo na hasa kipengele cha tamathali za usemi katika kazi nne teule za Sanja. Sababu iliyotupelekea kuchagua mada hii ni kuwa kazi hizi zilichapishwa miaka michache iliyopita na hivyo tuligundua kuwa hakuna ufafiti uliokuwa umefanyiwa kazi hizi nne kimtindo na hasa kipengele cha tamathali za usemi. Tulichunguza tofauti za kimtindo baina ya tanzu tofauti tofauti za fasihi andishi ambapo tuligundua kuwa kila utanzu wa fasihi andishi huwa na wasifu unaoutofautisha na utanzu mwingine katika fasihi andishi. Tulitambua vipengele vya kimtindo na hasa tamathali za usemi katika kazi nne teule za L. Sanja na tuligundua kuwa vipengele tulivyochunguza vya majazi, jazanda, kinaya, kejeli na ndoto zilidhihirisha upekee katika kazi za Sanja. Tulidhibitisha upekee wa kimtindo wa mwandishi Sanja katika kazi zake nne ambao ulidhihirika katika: Hisia zake, usimulizi aliotumia, uteuzi wa msamiati, muundo wa kazi na uchanganyaji wa tamathali mbali mbali. Katika kuchunguza upekee wa mwandishi Sanja tuligundua kuwa alitumia mbinu ya jazanda kwa mapana ili kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake. Kazi zake pia zilidhihirisha hisia za kusinyika, kukirihika na kutofurahishwa na tabia za viongozi wa Kiafrika za ufisadi, ubinagsi, kutoshirikiana na pia uongozi mbaya uliowaudhi raia wao.

## SURA YA KWANZA

### 1.1 USULI WA MADA

Utafiti wetu ulihusu uhakiki wa mtindo katika kazi nne teule za Leonard Sanja: Hadithi fupi mbili; “Mimba Ingali Mimba” katika *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (mh. McOnyango) (2006) na “Mwavyaji wa Roho” katika *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (mh. L. Sanja) (2011), tamthilia *Zinguo la Mzuka* (2011) na riwaya *Yasinya* (2014) tulijikita hasa katika kipengele cha tamathali za usemi. Tulitumia nadharia ya Umitindo ili kuzichanganua kazi hizi kitaaluma.

Kulingana na wataalamu Leech na Short (2007), Nadharia ya Umitindo inaweza kutumiwa kubainisha uhusiano uliopo baina ya umbo na athari zake katika kiwango fulani cha lugha. Yaani, Umitindo hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi wa matini za kifasihi kwa kuchunguza mtindo kwa njia ya kisayansi – yenye nidhamu na taratibu za kitaaluma; na huweza kuelezwa kama nadharia iliyokatikati ya Isimu na Fasihi. Kimsingi, wanaeleza kuwa nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiria kuchunguza mtindo wa kinachozungumziwa.

Nadharia ya Umitindo ilifafanuliwa zaidi na Wamitila (2008) aliposema kuwa, Mtindo ni jinsi msanii anavyotumia ufundi, umahiri na hisia zake katika kutenda au kueleza jambo fulani. Wamitila anasema pia mtindo ni uteuzi wa msamiati mpya uliopo, miundo na mipangilio ya sentensi, maneno au sauti, uteuzi na matumizi ya tamathali za usemi na jazanda pamoja na sifa za uakifishaji zinazolekea kukiuka njia za uakifishaji.

Dhana ya mtindo ilielezwa pia na mtaalamu mwingine (Senkoro 2011), aliyesema kuwa, mtindo ni upekee wa uundaji wa kazi za fasihi na hutofautiana baina ya msanii mmoja na mwingine kulingana na hisia za msanii huyo. Utufauti huo unaweza kujitokeza kwenye matumizi ya nafsi, uteuzi wa msamiati, mwanzo na mwendelezo wa kazi yake, usimulizi wa mwandishi, uchanganyaji wa tanzu mbali mbali za fasihi, kama vile kuingiza kipengele cha wimbo katika fasihi andishi.

Ufafanuzi huu wa dhana ya mtindo ukiwekwa katika muktadha wa utafiti tulioangazia una maana kuwa mwandishi huweza kuteua msamiati wake maalum kimaksudi au pasi na maksudi. Yaani, yeche huweza kuchagua neno moja na kuacha kisawe chake ili liafiki muktadha anaozungumzia na kufanya kazi yake ifae lengo lake. Kila mwandishi ana mtindo wake wa kuwasilisha kazi yake aliyoibuni na mtindo huu huweza kubadilika na kuimarika zaidi kwani uwanja wa fasihi unakuwa na kupanuka. Katika kazi za kifasihi kuna vipengele mbalimbali vyatya mtindo ambavyo waandishi hutumia kuelezea kazi zao, kama vile mandhari, wahuksika, usimulizi, msuko wa vitushi/ploti na tamathali za usemi.

## **1.2 SWALA LA UTAFITI**

Kazi za wasanii huchukua mitindo mbalimbali inayodhihirisha mabadiliko jinsi wanavyoendelea kuandika kazi tofauti tofauti, mabadiliko haya hudhihirisha kuimarika au kukua jinsi muda unavyosonga. Hali hii huweza kujitokeza katika tanzu tofauti tofauti. Kutokana na kazi zilizoandikwa imedhihirika wazi kuwa mitindo changamano inazidi kutumiwa na waandishi mbali mbali.

Katika chananuzi za hapo awali tanzu za fasihi zimekuwa zikichanganuliwa aidha kama utanzu mmoja au tanzu mbili kwa pamoja. Sisi katika uchanganuzi wetu tulichunguza mtindo hasa kipengele cha tamathali za usemi katika tanzu tatu za mwandishi mmoja kwa pamoja. Sanja ameandika hadithi fupi, riwaya na tamthilia. Kazi hizi alizoandika ni pamoja na *Yasinya* (riwaya), *Zinguo la Mzuka* (tamthilia), “Mwavyaji wa Roho” na “Mimba Ingali Mimba” (hadithi fupi) mtawalia.

Hivyo pengo ambalo tuliliziba katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili ni kuchunguza upekee unaodhirishwa katika vipengele vyatya mtindo hasa tamathali za usemi katika kazi nne teule za Sanja, mwandishi ambaye hajaangaziwa sana na wahakiki kwa mtazamo huu.

## **1.3 MALENGO YA UTAFITI**

Katika utafiti huu malengo yetu yalikuwa kama yafuatayo:

- (i) Kuchunguza iwapo kuna tofauti za kimtindo baina ya tanzu tofauti tofauti za fasihi andishi.

- (ii) Kutambua vipengele vya kimtindo na hasa tamathali za usemi katika kazi nne teule za L. Sanja.
- (iii) Kuonyesha jinsi mtindo unavyoimarisha maudhui katika kazi nne za mwandishi Sanja.
- (iv) Kudhibitisha upekee wa kimtindo wa mwandishi Sanja katika kazi zake nne teule.

## **1.4 NADHARIA TETE**

Somo hili liliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- (i) Mtindo hutofautiana katika tanzu anuai za fasihi andishi.
- (ii) Tamathali mbalimbali za usemi zimetumika kwa njia anuai katika kazi nne teule za L. Sanja.
- (iii) Mtindo umeimarisha maudhui katika kazi nne za mwandishi Sanja.
- (iv) Mtindo wa Sanja katika kazi nne teule ni wa kipekee.

## **1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA**

Uhakiki wa mtindo katika tanzu za fasihi kama vile tamthilia, riwaya, ushairi na hadithi fupi zimeshugulikiwa kama utanzu mmoja mmoja na wahakiki wengi wa hapo awali. Ni wahakiki wachache wameshughulikia tanzu anuai za kifasihi kwa pamoja. Sisi katika utafiti huu tulichunguza tanzu tatu za fasihi ambazo ni hadithi fupi mbili “Mimba Ingali Mimba” na “Mwavyaji wa Roho,” tamthilia moja *Zinguo la Mzuka* na riwaya moja *Yasinya*. Tulishughulikia mtindo hasa kipengele cha tamathali za usemi katika kazi nne teule za mwandishi Sanja.

Katika utafiti wetu tulipata kujua kuwa hakuna uhakiki wa kimtindo uliokuwa umefanyiwa kazi hizi nne kwa pamoja, hii ni Kwa sababu kazi hizi zimechapishwa miaka michache iliyopita kama ifuatavyo: “Mimba Ingali Mimba” (2006) “Mwavyaji wa Roho” (2011) *Zinguo la Mzuka* (2011) *Yasinya* (2014). Kama wachanganuzi tulionelea ni vyema kuzichanganua kazi hizi na kuziba pengo hili katika nyanja ya usomi ili kuimarissha kazi za fasihi ya Kiswahili.

## **1.6 UPEO NA MIPAKA**

Utafiti wetu ulihusu uchunganuzi wa mtindo, mitazamo mbalimbali kuhusu mtindo na jinsi mtindo hudhahirika katika tanzu anuai za fasihi andishi. Tulichunguza kipengele cha mtindo kimojawapo ambacho ni tamathali za usemi, yaani jinsi kilivyotumiwa katika kazi hizi nne za

mwandishi Sanja. Tulichunguza: Hadithi fupi zilizoandikwa na Sanja “Mimba Ingali Mimba” (2006) “Mwavyaji wa Roho” (2011), (tamthilia) *Zinguo la Mzuka* (2011) na (riwaya) *Yasinya* (2014). Ingawa lengo letu halikuwa kuangazia wahusika, lakini hatukuwa na budi kuwaangazia baadhi ya wahusika ili kuweza kudondo luga ilivyotumiwa na wahusika hawa katika kuchanganua mbinu ya majazi, jazanda n.k. Pia tulivieleza vipengele vilivyodhihirisha upekee wa kimtindo wa mwandishi Sanja. Ili kuchunguza kazi za mwandishi huyu kitaaluma tulijikita katika nadharia ya Umitindo.

## **1.7 MSINGI WA KINADHARIA**

Katika utafiti wetu tulitumia nadharia ya Umitindo ambayo ina wataalamu wengi walioieleza kama: Geoffrey Leech (1969), Crystal na Davy (1969), Leech na Short (1981, 2007), Paul Simpson (2004) na wengine. Wataalamu hawa walieleza nadharia ya Umitindo ambayo ilituongoza katika utafiti wetu.

### **1.7.1 Utangulizi**

Mtindo unaweza kuhusishwa na lugha ya maandishi, lugha ya kifasihi au isiyokuwa ya kifasihi ingawa kwa kawaida huwa unahusishwa na matini za kifasihi zilizoandikwa. Katika uandishi wa fasihi, istilahi “mtindo” hutumika kwa maana nyingi: Ni mazoea ya lugha kama wanavyosema Wana-umitindo (Crystal na Davy 1969). Wanasema tunaweza kuhusisha mtindo na mazoea ya matumizi ya lugha ya mtu binafsi au jamii-lugha, na hii ndiyo maana ambayo huwajia watu akilini wanapozungumza kuhusu mtindo wa uandishi wa mtu fulani, mtindo wa kuzungumza, wa kutoa hotuba hadharani, n.k.

Leech (1969) katika kitabu chake *A Linguistic Guide to English Poetry*, alisema yafuatayo kuhusu Umitindo:

Umitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma, unaofungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haijisimamii kivyake. Msamati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi hususan sitiari, taswira, kinyume, kinaya, kejeli, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu. Kwa hivyo, kama msingi wa kutumia taaluma

za kifasihi na za kiisimu, Umitindo ni uwanja ambamo masuala haya hushughulikiwa. (TY) (uk 11)

Kulingana nasi vipengele vya kifasihi na kiisimu ni vigumu kutengenisha wakati wa uhakiki kwa sababu vinaingiliana. Mjadala mkubwa umekuwepo kuhusu neno “mtindo,” ingawa istilahi hii imetumiwa sana katika uhakiki wa fasihi na hasa Umitindo. Istilahi hii imetumiwa katika miktadha mipana. (Leech na Short 2007) wanaeleza sifa za kisanaa zinazopatikana katika fasihi kama taaluma. Wanaeleza kuwa nadharia hii huangazia umuhimu wa lugha katika kueleza maana ya kifasihi. Na pia hutumiwa kurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani, na mtu fulani na kwa lengo fulani. Katika kitabu *Style in Fiction*, Leech na Short walishughulikia suala la mtindo katika kuchanganua matini za fasihi kisayansi kama tutakavyoeleza baadaye.

Kulingana na Leech na Short, malengo ya stadi za Umitindo ni fasihi pamoja na maumbo mengine ya matini zilizoandikwa katika nyanja za fasihi, matangazo ya biashara, utamaduni, siasa au dini. Umitindo hujaribu kubainisha kanuni za kueleza uteuzi uliofanywa na mwandishi katika matumizi yake ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeji wa maana, uhakiki wa kidiskosi na wa kifasihi. Zaidi walitaja kuwa Umitindo huangazia matumizi ya dayolojia au mazungumzo yanayohusisha lafudhi za kimaeneo na lahaja za wazungumzaji, lugha elezi na sarufi k.m sauti, urefu wa sentensi na rejista.

Dhana ya mtindo ilielezwa zaidi na mwanaisimu wa Kiswisi Ferdinand De Saussure (1983) ambaye alioanisha taaluma ya Fasihi na ya Isimu kwa kutofautisha dhana ya “langue” na “parole” katika lugha au “langage” kama alivyoeleza Saussure, “langue” ni utaratibu wa kanuni za lugha zinazojulikana na wazungumzaji wa lugha husika. Yaani, ni mfumo wa lugha ya jamii inayohusika. “Parole” ni matumizi ya utaratibu au kanuni za lugha ya mzungumzaji binafsi. Ni uteuzi wa kanuni ambazo msemaji huzitumia katika uandishi na uzungumzi wake. Kwa hivyo, mtindo ni kama “Parole” kwa kuwa ni uteuzi kutoka katika utaratibu wa kanuni zilizoko za lugha. Kwa muhtasari, lugha inayojulikana na wazungumzaji yaani “langage” inaundwa kutokana na kanuni za lugha (langue) pamoja na matumizi yake katika mazungumzo na maandishi (parole).

### **1.7.1 Sura Tofauti za Nadharia ya Umitindo**

Nadharia ya Umitindo ina viwango ambavyo mchanganuzi wa matini ya kifasihi anahitaji kuvizingatia ili kutekeleza uhakiki kwa njia ifaayo. (Leech na Short 2007) waliorodhesha aina za ukiushi wa kaida za matumizi ya lugha ambayo hutokea katika mtindo wa kazi za kifasihi. Viwango hivi vya ukiushi ni:

- (i) Ukiushi wa kimsamiati/kileksia.
- (ii) Ukiushi wa kisarufi.
- (iii) Ukiushi wa kilahaja.
- (iv) Ukiushi wa sajili/rejista.
- (v) Ukiushi wa kifonolojia.
- (vi) Ukiushi wa kimaandishi/kigrafolojia.
- (vii) Ukiushi wa kimapsi/kihistoria
- (viii) Ukiushi wa kisemantiki. (uk 120)

Kuna viwango vingi muhimu vya kuchunguzwa katika matini kwa kutegemea nadharia ya Umitindo kama wanavyooleza Leech na Short (2007) na pia Simpson (2004). Maoni ya waasisi hawa yameungwa mkono na Wamitila (2008) ambaye anasema kuwa:

Nadharia ya Umitindo inajikita kwenye uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa. Uchunguzi huu wa lugha unapania kubainisha ubunifu uliopo kwenye lugha hiyo na kwa kuutekeleza kwa undani unasaidia katika uelewekaji wa matini au kazi za kifasihi. Wamitila anaendelea kusema, maarifa yanayotokana na isimu hutumiwa ili kubaini sifa za kimtindo za kazi au matini ya kifasihi. Sifa hizi zinaweza kuwa za kifonolojia (ruwaza za sauti, vina, mizani), kisintaksia (miundo ya sentensi, aina ya sentensi), kimsamiati (maneno dhahania na maneno dhabiti, kuwepo na idadi ya nomino, vielezi, vivumishi n.k.) na kibalagha (matumizi ya tamathali za usemi, urudiaji na mbinu za urudiaji huo, jazanda) (uk 115)

Nadharia ya Umitindo ina viwango vingi lakini sisi tulitoa tu maelezo ya viwango vya nadharia hii vilivyohusiana na uchanganuzi wetu. Viwango hivi ni kama vifuatavyo:

#### **1.7.1.1 Kiwango cha Maandishi au Grafolojia**

Kiwango hiki pia huitwa kiwango cha utendaji. Kiwango hiki kinahusu vipengele vya kifonetiki, kifonolojia na kigrafolojia. Kinahusu jinsi lugha inavyotamkwa na kuandikwa. Kwa kawaida, kila kazi ya fasihi huwa katika maandishi fulani na mahsusimtena huwa katika abjadi

zinazoleweka na kuzoleka na walengwa. Hata hivyo, matini za kifasihi huweza kuwa na sifa za kimaandishi ambazo zinachimuzwa na hivyo kutilia uzito kiwango hiki cha ukiushi. Ukiushi huu unahu su kubadilisha matamshi ya maneno, matumizi ya herufi kubwa kwa njia isiyo ya kawaida: Kutumia herufi ndogo mahali pa herufi kubwa, matumizi ya herufi za mlazo/italiki, mpangilio wa aya (au ukosefu wake) na matumizi ya viwakilishi kama koma, alama ya hisi, koloni na vistari. Maelezo haya ni kulingana na; (Leech na Short 2007:104, Wamitila (2008:512) kiwango hiki kilitufaa kwani katika tamathali za usemi tulizochunguza alama za uakifishaji zilichimuza maana tofauti katika maneno ya kawaida kama vile maswali ya balagha. Pia tuliweza kuchanganua herufi za mlazo/ italiki ambazo zilitumika wakati mwandishi alichanganya msimbo na katika kutoa maelekezo katika tamthilia.

### **1.7.1.2 Kiwango cha Umbo**

Matumizi ya lugha kwa kawaida huhusisha uteuzi wa maneno au msamiati maalum. Kwa kuwa fasihi inatumia lugha kujieleza, vipengele ambavyo huhusishwa katika uteuzi huu ni vingi. Kuna kiwango cha kimsamiati (kileksia), matumizi ya lajaja na kiwango cha rejista/sajili. Kiwango hiki pia huhusu kuchanganaya ndimi, kuhamisha ndimi na matumizi ya maneno ya kigeni kama ya Kiingereza au Kilatini.

Suala la uteuzi halihusishwi na maneno peke yake. Mwandishi pia hufanya uteuzi wa wahusika anaowatumia kwenye kazi yake, usimulizi anaoutumia, mtazamo wake, na mada anayoshughulikia. Kwa mfano katika uteuzi wa mhusika, lazima lugha yake iafikiane na mazingira anamopatikana na pia kiwango chake cha elimu. Haya ni maelezo kulingana na; (Leech 2007:105, Wamitila 2008.) Kiwango hiki kilitufaa hasa katika kuchanganua mbinu ya majazi ili kuwaeleza wahusika pamoja na lugha waliyotumia, pia katika kuchanganaya ndimi, sajili, mada ya mwandishi na mtazamo wake.

### **1.7.1.3 Kiwango cha Kisemantiki**

Kiwango hiki kinahusu lugha ya kitamathali na miundo ya lugha ambayo ni sifa muhimu ya kuchunguza matini ya kifasihi tunapotumia nadharia ya Umitindo. Ni jinsi matumizi ya lugha yanavyoathiri maana kwa njia fulani. Ukiushi wa aina hii unahu su matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyofasiriwa katika hali za kawaida. Mara nyingi huhusisha matumizi ya maneno

kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Huwepo matumizi ya tamathali za usemi: Mbinu za kinaya, kejeli, mbinu ya kweli-kinzani (paradoksi,) sitiari n.k. Pia, huhusisha matumizi ya jazanda, yaani lugha ya picha aidha za kimaelezo au za kiishara (ambazo si taswira au picha tu bali zina ujumbe wa ziada). Maeleo haya ni kulingana na; (Leech na Short 2007:101, Wamitila 2008:518). Kiwango hiki kilitufaa sana kwa sababu kama tulivyoeleza, mtindo ni jinsi lugha ilivyotumiwa na kuathiri maana kama inavyotumika kwa njia ya kawaida. Kiwango hiki pia kilituwezesha kuhakiki tamathali za usemi tulizoteua kuzichanganua katika kazi hizi nne teule za Sanja.

Kwa muhtasari mtindo unaweza kueleza kama mazoea ya matumizi ya lugha ya mtu au jamii-lugha fulani. Nayo nadharia ya Umitindo hujihusisha na uhakiki na fasiri ya matini katika mtazomo wa Kiisumu kama taaluma ambaa una uhusiano wa karibu na mtazomo wa Kifasihi. Nadharia hii huangazia umuhimu wa lugha katika kuendeleza maana ya kifasihi, pia hueleza jinsi mtu hutumia lugha katika muktadha fulani na kwa lengo mahsus. Nadharia hii pia tuliona hujihusisha na matumizi ya dayolojia inayohusu lafudhi za kimaeneo na lahaja za wazungumzaji, lugha elezi na sarufi. Pia tunaweza kueleza kuwa nadharia hii hujihusisha na uhusiano baina ya umbo na athari zake katika kiwango fulani cha lugha. Na mwisho tuliona kuwa Umitindo hueleza uteuzi uliofanywa na mwandishi katika matumizi yake ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeaji maana na uhakiki wa kidiskosi wa kifasihi.

## **1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA**

Swala la mtindo limechangiwa na waandishi mbalimbali. Wameshughulikia vipengele tofauti tofauti vya mtindo na pia kumulika kazi tofauti tofauti. Miongoni mwa waandishi hao ni:

Ndung'u (1996) katika tasnifu yake "Uhakiki wa Fani katika Riwaya za *Katama Mkangi*", alichunguza vipengele vya mtindo na kutathmini kufaa kwa matumizi yake. Pia alichunguza maudhui katika *Ukiwa* (1975), *Mafuta* (1984), na *Walenisi* (1995). Kazi yake ilitufaa katika uchanganuzi wa mtindo na wahusika japo ilitofautiana na yetu kwa sababu alitafitia kipengele cha ploti ambacho sisi hatukukitafiti. Sisi tulichanganua mtindo na hasa kipengele cha tamathali za usemi. Mhakiki huyu alichunguza fani katika utanze wa riwaya, sisi tulichunguza tanzu za riwaya, tamthilia na hadithi fupi.

Otieno (2005) alihakiki kipengele cha mtindo katika tasnifu yake “Muumano wa Leksika katika Matini. *Babu Alipofufuka*”. Alisema kwamba, baada ya msanii kutambua maudhui ya kazi yake huchunguza lugha ya matini ili kufafanua utanru wa tamathali za usemi akichanganua upekee wowote ule wa mtindo wa msanii. Alisema kuwa msanii huwa huru kukiuka kaida za lugha ili kuchangia uwiano unaonata. Alitumia nadharia ya usasa na usasaleo, umuundo na nadharia ya Isimu Mtindo. Kazi yake ilitufaa katika kuchunguza upekee wa mtindo wa Sanja, kipengele cha tamathali za usemi katika kazi zake nne.

Ongarora (2007) alishughulikia “Mtindo katika ‘Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine’”. Alishughulikia mtindo kama matumizi ya lugha. Alihakiki ukiushi katika mpangilio wa nomino, vitenzi, vielezi, viunganishi na vihusishi katika sentensi. Tena aliangazia baadhi ya ukiushi wa kisemantiki na mbinu nyingine za lugha katika “Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.” Sawa naye katika kazi yetu tuliangalia ukiushi wa kisemantiki. Tuliangazia kipengele cha mtindo hasa tamathali za usemi tukizingatia lugha ilivyotumika katika kazi nne za Sanja.

Kitali (2011) alishughulikia fani katika tamthilia mbili, *Pango na Mama Ee*. Alichunguza jinsi wahusika wanawake walivyotumia lugha. Katika kipengele cha mtindo, aliangalia mbinu za lugha zilizoteuliwa na mwandishi kama zimemkuza ama kumdunisha mwanamke. Yeye alijikita katika fani na matumizi ya lugha iliyosimulia kazi hizo. Sisi tulishughulikia mtindo katika tamthilia ya *Zinguo la Mzuka*. Lakini zaidi kazi yetu ilikuwa tofauti na yake kwa sababu tulichunguza mtindo katika tanzu zaidi ambazo ni riwaya na hadithi fupi za Sanja. Pia sisi hatukuhakiki lugha ya wahusika wa jinsia fulani kama Kitali alivyofanya bali tulitathmini lugha ya wahusika wa jinsia zote kwa kujikita katika mbinu ya majazi.

Katutu (2013) alishughulikia “Mtindo katika ‘Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine’ ya Said Mohamed”. Alijikita katika matumizi ya msamiati na mtindo kwa misingi ya kisintaksia. Katika matumizi ya msamiati wa diwani hiyo alichunguza pia ukiushi katika baadhi ya kategoria za maneno; sentensi ndefu, fupi na nafasi ya uakifishaji katika sintaksia ya diwani yenyewe. Kazi yetu ni tofauti na yake kwa sababu sisi tuliangazia mtindo hasa kipengele cha tamathali za usemi kilivyotumiwa kuimarisha maudhui na upekee wa mwandishi katika kazi nne za L. Sanja.

Hatukuangazia msamiati kama Katutu alivyofanya katika misingi ya kisintaksia. Lakini tulifaidika sana katika sehemu ya mtindo, hasa matumizi ya uakifishaji katika mbinu ya maswali ya balagha.

## **1.9 MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti wetu ulikuwa wa kimaktaba. Tulisoma vitabu na makala ya mtandao yaliyotoa maelezo kuhusu fasihi andishi hasa tanzu za riwaya, tamthilia na hadithi fupi ambazo tulitafiti. Tulisoma ili kupata mwanga zaidi kuhusu tanzu tulizozitafiti.

Sampuli tuliyoteua ni sampuli lengwa ambayo ni riwaya, tamthilia na hadithi fupi za Leonard Sanja. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999:50) aina hii ya sampuli hutumika katika utafiti unaokusudiwa kupata habari za kina na bila kujumlisha. Kwa kurejelea maelezo haya, tulichagua kimaksudi riwaya ya *Yasinya*, tamthilia ya *Zinguo la Mzuka*, na hadithi fupi “Mimba Ingali Mimba” na “Mwavyaji wa Roho” kimaksudi, kwa sababu zilitusaidia kupata habari za kina za suala tulilochunguza la mtindo wa Sanja hasa kipengele cha tamathali za usemi.

Riwaya, tamthilia na hadithi fupi tulizoteua tulizisoma na kuchunguza ili kubaini mtindo hasa tamathali za usemi zilizomo katika kazi nne teule za Sanja. Pia tulisoma tasnifu za waandishi wengine zilizoandikwa kuhusu mada yetu ili kupata mwelekeo wa kazi yetu.

Data tuliyopata tulichanganua kulingana na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia ya Umitindo. Kwa kutumia msingi wa nadharia hii tulichanganua mtindo hasa tamathali za usemi tulizoteua katika kazi hizi nne, kwa kutumia nadharia hii, tulieleza ni sababu gani dhabiti ambazo tulitoa ili kuainisha maneno au vifungu vya maneno husika kama mtindo hasa tamathali za usemi.

Baada ya kukusanya na kuchanganua data, uwasilishaji wa matokeo ulifanywa kwa njia ya maelezo. Uwasilishaji huu ulihusu maelezo ya mtindo hasa kipengele cha tamathali za usemi kwa kurejelea kazi nne tulizoteua.

## **SURA YA PILI**

### **MTINDO NA TANZU ZA FASIHI ANDISHI**

#### **2.1 Utangulizi**

Katika utafiti wetu tulichunguza tanzu tatu za fasihi andishi. Katika sura hii, tulitoa maelezo kuhusu mtindo na tanzu za fasihi andishi, lakini tulitilia mkazo tanzu tatu ambazo tulichanganua ambazo ni: Riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Nia yetu ilikuwa kuonyesha kuwa swala la tanzu na mtindo linaweza kusemekana kuwa la mtu binafsi.

Kama wanavyosema (Njogu na Chimera 1999) mtindo ni dhana inayotumiwa kurejelea mbinu tofauti za kifasihi na ambazo zinadhamiriwa kuwa na athari fulani za kiujumi wa msanii. Wanaendelea kueleza kuwa mtindo ni mseto wa fani na maudhui. Hii inamaanisha kwamba mtunzi wa kazi ya sanaa ana namna yake ya kuijenga kazi yake ili kuzioanisha fani na maudhui kivyake katika ubinafsi wake. Pia wanaeleza kuwa mtindo ni ujuzi wa kujieleza na kuwa vipengele vyake ni kama vile: Tashbihi, tashhisi, tasfida n.k. Mtindo hutumiwa kupeleka mbele maudhui, dhamira na ufasaha wa msanii.

Kuna maelezo mengi ambayo yametolewa na waandishi wengi kuhusu mtindo. Zaidi kuna mitazamo kadha ambayo imetumiwa kueleza dhana ya mtindo. Mitazamo hii ni kama: Mtazamo wa kiisimu, mtazamo wa kifasihi, mtazamo wa kifasihi na kiisimu na mtazamo wa mtindo kama swala la mtu binafsi.

#### **2.1.1 Mtazamo wa Kiisimu**

Kabla ya Umitindo kutumiwa katika fasihi, ulijaribiwa na mwanaisimu Ferdinand de Saussure. Katika kuzungumzia muundo wa lugha, De Saussure (1983) anadai kuwa lugha ina sehemu mbili zinazodhahirika katika usemajji yaani, lugha dhahiri na lugha dhahania. Lugha dhahiri hutumika katika mazungumzo ya kila siku, nayo lugha dhahania ni lugha ambayo daima haibainiki wazi, ijapokuwa baadhi ya kanuni zake hudhahirika katika maongezi ya kila siku. Lugha hii pia aliita lugha tumikizi ambayo huonyeshwa katika uwezo wa mtu wa kuunda idadi yoyote ile ya sentensi kadiri anavyotaka. Hata hivyo mtu hawezi kutunga sentensi zote zinazoweza kutungwa duniani kwa sababu jambo hili haliwezekani.

Mwanaisimu huyu pia alisema kwamba licha ya kuwa si rahisi kufahamu tabia ya lugha kwa jumla, maongezi ya kawaida yanategemea miundo na tabia za lugha. Yaani lugha ni mfano wa muundo unaojitosheleza na unaojieleza. Matawi mbali mbali hayawezi kutafsiriwa nje ya mipaka ya muundo huu wa lugha. Dhima ya kila tawi hutegemea kuwepo kwa matawi mengine. Matawi haya ni: Fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmantiki. Tulijadili mitazamo hii ili kuweza kuieleza dhana ya mtindo kwa kina kama ifuatavyo:

### **2.1.2 Mtazamo wa Kifasihi**

Kulingana na maoni yetu mtindo hutumiwa kueleza jinsi mwandishi alivyotumia vipengele kama: Usimulizi, msuko wa matukio, mandhari, wahusika na tamathali za usemi ili kuiwasilisha kazi yake kwa hadhira yake.

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza mtindo kifasihi kuwa: Mtindo huelezwa kwa kuainishwa na madhumuni ya msanii. Madhumuni ni dhamira na mtindo ni jinsi dhamira inavyowasilishwa. Kauli hii inaweza kuchukuliwa kwamba wazo kwanza huota katika fikra za mwanasanaa au msemaji yejote wa kifasihi. Wadhifa wa mwanasanaa ni kuainisha na kutumia lugha inayofaa na kulieleza wazo hilo.

### **2.1.3 Mtazamo wa Kifasihi na wa Kiisimu**

Wataalamu katika taaluma ya Fasihi na Isimu wamekuwa na mvutano kutokana na upekee wa taaluma hizi mbili, lakini kuna wale wanaokubaliana kuwa taaluma hizi mbili hukamilishana na kutegemeana.

(Leech na Short 2007) katika kitabu chao *Style in Fiction* walitoa mchango wao kuhusiana na uhusiano uliopo kati ya taaluma hizi mbili. Waandishi hawa wanasema kuwa tunaweza kuchanganua matini kulingana na jinsi maneno au miundo imeteuliwa na kuyaacha mengine. Wanaendelea kusema kuwa mtindo ni sifa bainifu za lugha. Yaani, kutegemea kinachosemwa na jinsi kinavyosemwa. Kulingana na wataalamu hawa kuna uhusiano wa karibu kati ya fani na maudhui kwa sababu vipengele hivi viwili hukamilishana na kujengana.

Mtaalamu (Flaubert 1964) alitoa mchango wake kuhusu mtazamo huu na akasema kuwa fani na maudhui ni kama ‘mwili na roho’ yaani, sio rahisi kutenganisha fani na maudhui kwa sababu

taaluma hizi mbili zinahusiana na hukamilishana. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa tofauti ya kile mwandishi anasema na jinsi anavyo iwasilisha kazi yake kwa msomaji ina msingi wake katika wazo la kijadi kuwa mtindo ni ‘vazi la mawazo’ yaani, haviwezi kutenganishwa. Hata ingawaje msemo huu una maana ya ‘kupamba’ au ‘kufunika’ wazo hili limekubalika kwa muda hivyo kufaa kwake hakuwezi kutupiliwa mbali. Katika mkabala huu huwa tunasoma kazi ya mwandishi na kuichanganua kwa muktadha alioandika ili kutadhmini kama alifaalu kuteua maneno yake kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake au la.

(Spitzer 1948) alitoa mchango wake kuhusiana na mtazamo huu. Katika maelezo yake alibuni alichokiita ‘philological circle’ yaani mzunguko wa kuuelewa uhusiano kati ya isimu na fasihi. Spitzer anasema kuwa hakuna njia za kisayansi za kutambua mpaka kati ya taaluma ya Fasihi na ya Isimu. Anaeleza kuwa uhusiano huu ni wa mzunguko kwani hakuna mipaka iliyowekewa taaluma hizi mbili yaani, ya kuonyesha kuwa Fasihi inaanza hapa na kuishia hapa na Isimu inaanza hapa na kuishia hapa. Hivyo maoni yake yanashabihiana na ya Leech, Short na Flaubert kuwa sio rahisi kutenganisha taaluma ya Isimu na ya Fasihi kwani zina uhusiano na hutegemeana.

Hatuwezi kuhitimisha maelezo ya mwelekeo huu wa mtindo bila kumtaja mwanaisimu Mswizi De Saussure (1983), ambaye alioanisha dhana ya ‘langue’ na ‘parole’ kueleza mtindo. Kulingana naye ‘langue’ ni utaratibu na kanuni za lugha zinazojulikana na wazungumzaji wa lugha husika, yaani mfumo wa lugha ya jamii-lugha husika. ‘parole’ nayo ni matumizi ya utaratibu wa lugha ya mzungumzaji binafsi. Mtindo hapa unalinganishwa na ‘parole’ kwani mzungumzaji au mwandishi huteua kutoka katika utaratibu wa kanuni zilizoko za lugha (langue) na kuzitumia katika uandishi au uzungumzi wake (parole).

Kulingana na maelezo ya wataalamu hawa ni wazi kuwa sio rahisi kutenganisha taaluma hizi mbili yaani, Fasihi na Isimu. Kulingana na maoni yetu kila mwandishi huwa na wazo la kuwasilisha kwa hadhira yake na lazima mwandishi huyu abuni njia ya kuwasilisha kazi yake. Ili lengo lake liafikiwe mwandishi huyu hulazimika kubuni mtindo atakao tumia kuiwasilisha kazi yake, hivyo sio rahisi kutenganisha taaluma hizi mbili za Fasihi na Isimu.

## **2.1.4 Mtazamo wa Mtindo kama Mtu Binafsi**

Mtazamo huu husisitiza uhakiki wa mtindo wa mwandishi binafsi. Kulingana na (Galperin 1981) anasema kuwa mtindo wa mwandishi ni muungano wa vipengele maalum vya lugha - njia za kujieleza na njia za uchanganuzi ambazo ni za kipekee kwa mwandishi fulani ambazo huifanya kazi ya mwandishi au matamshi yake kutambulika kwa urahisi. Kwa hivyo mtindo wa mwandishi unaweza kulinganishwa na jina la kipekee (*proper name*). Katika mtindo fulani tunaweza kupata mtindo wa kijumla - unaopatikana katika kazi za waandishi wengi na ule mahsus - ambao hujitokeza katika kazi ya mtu binafsi. Jinsi mwandishi anavyoimarika katika uandishi ndivyo mtindo wake huwa dhahiri.

Galperin anaendelea kusema kuwa, tunapofaulu katika kutenga na kuchagua mtindo ambao mwandishi hupendelea, tunaweza kueleza vile vipengele vinavyomtaubulisha kama mtindo wa mwandishi fulani. Kwa upande mwingine mtindo wa mwandishi huhusishwa na uteuzi na ubunifu wake binafsi kutoka kwa ukwasi wa lugha. Mtindo wa Mwandishi unaweza kudhihirisha ufasaha, uchangamano, usahili, unaoficha maana na kadhalika. Pia tunaweza kusema kuwa lugha fulani imepambwa sana au ni ya kusisimua, kushawishi au kupendeza na ndilo jambo huwapelekea wasomaji kijiuliza maswali kama, kwa nini mwandishi akatumia njia hii kujieleza na kuiacha nyingine.

Dhana hii ya mtindo kuwa ni swala la mtu binafsi imetiliwa mkazo na (Senkoro 1982), anayesema kuwa mtindo katika kazi ya fasihi ni ile namna ambayo msanii hutunga kazi hiyo na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni au kaida zilizofuatwa (za kimapokeo) ama ni za kipekee. Anaendelea kusema, mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hutokeza au huonyesha nafsi na labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo. Katika fasili hii tunaweza kuona anachokieleza mtaalamu huyu ni kwamba mtindo huhusisha upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi ambapo upangaji huu hutegemea upekee alionao msanii kwa maana nyingine, unaposoma kazi fulani ya fasihi unaweza kumwona mtunzi wa kazi hiyo kulingana na jinsi alivyoandika, kwa maana kwamba jambo moja linaweza kuongelewa na wasanii wawili tofauti lakini namna linavyowasilishwa likatofautiana, na hii ni kulingana na upekee wao.

Mtindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Mtindo huelezea jinsi mwandishi anavyounda kazi yake. Anaendelea kusema, dhana ya mtindo hurejelea sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha kwenye fani yake. Mazoea hayo ya mwandishi ya kuandika, kuteua msamati, tamathali za usemi, taswira, uakifishaji, sentensi n.k. ndio yanayompambanua mwandishi huyu na mwenzake kiasi kwamba msomaji anaweza kusema “hii ni kazi iliyoandikwa na fulani” kwa kuisoma tu. Maelezo haya ni kulingana na (Wamitila 2003)

Kitu anachokisema hapa Wamitila hakitofautiani na kauli ya Senkoro, kinachoongelewa hapa ni upekee wa mwandishi husika lakini Wamitila kasema kitu kimoja zaidi, kwamba msanii anaonekana kuwa na mtindo fulani kwa sababu amezoea kutunga kazi zake za fasihi kwa namna fulani ambayo inadhihirisha upekee wake. Kutokana na kauli hii ya Wamitila tunaweza kusema kwamba mtindo wa mtunzi huonekana baada ya mwandishi kuandika kazi kadhaa na kimsingi hii ndio huleta maana halisi ya mazoea.

Tulikubaliana na kauli hii, hata hivyo msomaji hawezi kuhitimisha kuwa mtunzi fulani mtindo wake ni huu kama amesoma kazi yake moja tu, kwa hiyo mtindo (upekee) wa mwandishi huweza kubainishwa baada ya kupitia kazi zake kadhaa na ndipo tunaweza kuona mazoea ya mwandishi huyo katika kuandika kazi zake. Kwa muhtasari tunaweza kusema kuwa, mtindo ni ule upekee alionao mtunzi wa kazi ya fasihi katika kuipa kazi yake sura fulani kifani na kimaudhui ambapo mtunzi mwingine hawezi kufanya hivyo hata kama kitu kinachoongelewa ni kilekile.

Mtu anaweza kujuliza, nitawezaje kubainisha mtindo wa mtunzi katika kazi ya fasihi? Swali hili linaweza kujibiwa kwa kuangalia vipengele fulani fulani. Kulingana na Wamitila (2003) na wataalamu wengine mtindo wa mwandishi unaweza kubainishwa kwa kuchunguza vipengele vifuatavyo:

- Matumizi ya lugha: Je, lugha ni rahisi au ngumu, je, kuna matumizi ya maneno ya kiufundi? n.k.
- Matumizi ya dayolojia: Je, ni kwa kiasi gani mtunzi ametumia dayolojia, ni kwa kiasi gani dayolojia husimulia hadithi?

- Namna ya usimulizi: Je, anatumia nafsi ya kwanza, ya pili, ya tatu au nafsi mbalimbali zinazopishana katika usimulizi wake n.k.
- Ukuaji wa wahusika: Kwa vipi mtunzi anawatambulisha wahusika na kwa vipi wanabadilika katika hadithi.
- Hisia za mwandishi: Je, hisia zake zinaonekanaje katika hadithi? Je, anaonekana ni mwenye mapenzi, mwenye matumaini, kejeli n.k.
- Namna anavyopanga sura au matukio katika hadithi: Je, sura ni fupi au ndefu? Ni nyingi kiasi gani, zimepangwaje? Na kwa nini zimepangwa hivyo?
- Tamathali za usemi: Je, mwandishi ametumia kwa kiasi gani tashbiha, sitiari, tashihisi au alama za uakifishaji?
- Mandhari: Je, mandhari yaliyotumika ni halisi au ya kubuni?
- Uteuzi wa msamiati: Je, ni kwa kiasi gani msamiati uliotumika unaleta mvuto kwa msomaji? (uk 192)

Mtindo hutambulisha mtunzi wa kazi ya fasihi: Watu hupenda kazi ya mtunzi fulani kwa sababu mtindo anaotumia huwavutia wasomaji wake. Kwa hivyo tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa, tunapozungumzia dhana ya mtindo tunarejelea mwandishi husika, kwa maana kwamba ubinafsi wake ndicho kile kinachoonekana kwenye kazi yake. Tunaposema hadithi fulani ina taswira nyingi, ina sitiari nyingi au lugha yake inavutia n.k. tunakuwa tunarejelea mtindo wa mtunzi husika kwa ujumla. Lakini tunapotambua namna mwandishi fulani anavyotumia istilahi kwa njia ya kipekee basi tutakuwa tumegundua mtindo wake.

### **2.2.1 Mtindo katika Tanzu mbalimbali za Fasihi Andishi**

Tanzu mbali mbali za kifasihi pia zina miundo tofauti ambayo inaweza kuchukuliwa kama mtindo.

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake. Kama anavyoeleza (Wamitila 2003) fasihi huathiri, hugusa au huacha athari fulani na hupatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii fulani. Sanaa ya fasihi imegawika katika makundi mawili yajulikanayo kama Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. Katika ‘tamaduni andishi,’ fasihi Simulizi zimeathiriwa na mfumo wa kimaandishi, sio simulizi tena bali

inahifadhiwa kwa njia mbalimbali kama kwa vinasa sauti, kanda za video na kompyuta. Isitoshe kuna vitabu vingi vinavyokusanya methali, vitendawili, nahau, semi, mashairi, tendi au nyimbo ambazo hapo kabla zikihusishwa tu na fasihi simulizi.

Wamitila anaendelea kusema kuwa: Kutokana na kuwako kwa mfumo wa maandishi na uhifadhi mpya wa teknolojia, fasihi andishi imesambaa sana katika jamii nyingi kwa tanzu kama: Riwaya, tamthilia, hadithi fupi, wasifu, tarihi, insha, tawasifu na kadhalika. Kila utanzu wa fasihi Andishi una mtindo wake maalum ambao huutofautisha na mwagine. Tuliangazia mtindo wa tanzu tulizochunguza kama ifuatavyo:

### **2.2.2 Riwaya**

Riwaya ni hadithi ndefu ambayo ina visa na vitushi, migogoro na inayosimulia mambo yanayohusiana na jamii. Riwaya ni kazi ya kubuni na huhusisha binadamu au wanyama (wahusika) ambao wanatenda mambo fulani kwa ukamilifu na matukio yake huhusisha kipindi au wakati fulani. Katika riwaya huwa kuna mambo kadha ya kuangalia kama: Dhamira na maudhui, wahusika, migogoro na mivutano, muundo na mtindo na mandhari. (Wamitila 2003: 187).

Riwaya ni kazi ilioandikwa kwa mtindo wa kinadhari ambayo ina urefu wa kiasi fulani na uchangamano wa kimtindo na kidhamira na inashughulikia maswala kadha katika mtazamo mpana wa wakati na matumizi mapana ya mandhari. Riwaya pia ina sifa ya kuwa na kina cha uhusika kinachohusisha undani wa kisaikolojia na ubainishaji wa misukumo ya kitendaji. Haya ni kulingana na (Wamitila 2008:114). Kuna aina mbalimbali za riwaya kama: Riwaya ya kijasiri, riwaya ya maendeleo, riwaya ya wakati/kiwakati n.k. na huwa na wasifu mbali mbali kama ifuatavyo;

Kulingana na Wamitila (2008) kazi za riwaya huweza kudhihirisha kipindi fulani cha wakati. Usimulizi wa riwaya huwa unaonyesha wahusika wanaotenda matendo yao katika kipindi mahsusini cha kiwakati. Kazi za riwaya wakati mwagine hueleza maisha ya wahusika kutoka utotoni hadi utu uzimani. Kwa msingi huu, wakati unaweza kuangaliwa kwa misingi ya usimulizi wa muhtasari pale ambapo wakati mrefu (kwa matukio) unashughulikiwa kwa wakati

mfupi (kimaelezo). Kuna riwaya pia ambazo hudhihirisha wakati fulani wa kihistoria kwa sababu huwa zina maudhui yanayolingana na kipindi cha kihistoria k.v. maudhui ya ukoloni, ukombozi, uongozi mbaya n.k.

Wamitila pia anaeleza kuwa: Riwaya yoyote ile hutawaliwa kwa kiasi kikubwa na msuko na muundo. Msuko wa riwaya huwa changamano. Uchangamano hutokea pale ambapo mkondo asilia wa matukio hukiukwa katika kutumia mbinu ya kisengere nyuma/mbinu rejeshi na kisengere mbele/mbinu elekezi. Mbinu hii hutumiwa ili kuchochea tataruki na hamu kwa upande wa msomaji.

Vile vile Wamitila anasema kuwa mandhari katika riwaya ni mahali au wakati wa hadithi au kisa. Kutokana na urefu wa kazi ya riwaya mandhari hufafanuliwa na humwezesha mwandishi kuendeleza dhamira na ukuaji wa wahusika. Mandhari hubadilika badilika kutoka yale ya mashambani, mjini, shulen, ofisini, uwanjani n.k. kwa sababu riwaya huzungumzia matukio mbalimbali.

Kulingana na Wamitila riwaya huendeleza wahusika kwa undani na kisaikolojia na ukuaji wao huelezwa kutoka utotonu hadi utu uzimani kutokana na urefu wa kazi. Wahusika wanaweza kuwasilishwa kwa uzungumzinaksi, majazi, ulinganuzi/mgotanisho, urazini/ung'amuvi, mwingilianomatini, udukuzi/upenyuzi wa mwandishi, maelezo ya msimulizi/mwandishi n.k.

Kulingana na mtaalamu huyu riwaya huhusisha usimulizi wa matukio kwa mapana kutokana na wakati mrefu, usimulizi huu unaweza kufafanua aidha wahusika, mahali, wakati na matukio. Mambo haya ndio huzua aina mbali mbali za riwaya. Usimulizi katika riwaya unaweza kuwa wa mwandishi (nafsi ya tatu), wa mhusika (nafsi ya kwanza) au wa nafsi mbali mbali kupishana katika usimulizi.

Kwa kuhitimisha ni maoni yetu kuwa riwaya huzungumzia mambo mbalimbali au maudhui mbali mbali kwa sababu ya wakati mrefu na pia kwa sababu kazi za riwaya huzungumzia mambo au matatizo yanayowakumba wanajamii. Urefu huu humwezesha mwandishi kuyaeleza mandhari na wahusika kwa mapana na huchangia katika kuboresha mtindo wa mwandishi.

### **2.2.3 Tamthilia**

Tamthilia ni fani ya fasihi iliyokusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira fulani. Hivyo kwa lugha ya kawaida tamthilia huitwa mchezo wa kuigiza. Tamthilia huwa na masimulizi ambayo huigwa na wahusika wa pande mbili au zaidi zinazogongana. Maeleo haya ni kulingana na Mulokozi (1996:188).

Utanzu wa tamthilia umeelezwa pia na Wamitila (2003) ambaye aneleza kuwa ni utanzu ambao hutegemea mazungumzo na uigizaji ili kuwasilisha ujumbe wake. Huu ni utanzu ambao huandikwa kwa mtindo wa mazungumzo ya wahusika. Mazungumzo hayo sio majibizano ya usemi au kauli tu bali ni msingi mkuu wa kuendelezwa na kukuzwa kwa tendo kuu la kidrama katika tamthilia fulani. Baadaye Wamitila alitoa wasifu wa utanzu wa tamthilia ambao huufanya utanzu huu kuwa wa kipekee ukilinganishwa na tanzu zingine za fasihi andishi, sifa hizi ni kama zifuatazo:

Kulingana na Wamitila (2008), drama haishii kwenya utunzi tu bali pia huhusisha maswala yanayofungamanishwa na uigizaji, uangazaji wa jukwaa, mitagusano ya waelekezi, maleba, waigizaji, muziki, na jukwaa. Kwa msingi huu ni rahisi kusema kuwa riwaya inaisha tu iandikwapo ilihali drama inaanza tu baada ya kuandikwa kwani lazima iigizwe.

Wamitila pia anaeleza kuwa mwandishi wa riwaya ana uhuru mpana wa upenyezaji wa kisimulizi na wa kuweza kuingia kwenye akili za wahusika wake na labda hata kuelekeza kwa njia wazi lengo au dhamira yake. Mwana-drama kwa upande wake anaweza tu kuwasiliana na hadhira kupitia kwa wahusika wake (waigizaji).

Mtaalamu huyu alieleza kuwa mipaka ya kibunifu aliyo nayo mwandishi wa drama ni finyu anapolinganishwa na mwandishi wa riwaya ambaye ana uhuru mwingi na labda hadhibitiwi sana na kaida za utanzu. Mwana-drama analazimika kuwazia uwasilishaji wa anachokishughulikia jukwaani.

Vilevile Wamitila anaeleza kuwa wakati humbana mtunzi wa kidrama na kwa njia hii kuubana mwanda wake wa kidhanifu (*imaginative space*) anapolinganishwa na mwandishi wa riwaya

ambaye halazimiki kubana au kudondo mambo mengi kwenye msuko wa kazi yake. Hii hasa ndiyo inayowafanya wahakiki kushikilia kuwa ‘tamthilia ni hadithi fupi inayowasilishwa jukwaani.’

Kwa malelezo ya Wamitila tamthilia huwa na mwelekeo mkubwa wa athari kubwa ya mkokotezo wa hisia katika drama kuliko katika riwaya. Kwanza, riwaya huwa ndefu na huweza kuchukua muda mrefu kusomwa. Hali hii inaathiri kule kuwepo kwa mshindilio wa kihisia kwa sababu, kisaikolojia, haimkiniki kuurefusha mshindilio huo sana.

Wamitila alieleza pia, ingawa kazi zozote za fasihi hutegemea kuwepo kwa mgogoro (na ipo migogoro ya aina tofauti) mgogoro unachukua nafasi kubwa sana katika drama kwa kuwa ndio msingi mkuu wa kuwepo kwa tendo la kidrama ambalo huisukuma drama mbele.

#### **2.2.4 Hadithi Fupi**

Hadithi fupi ni masimulizi yaliyoandikwa kinathari, juu ya tajriba fulani ya maisha. Aghalabu mwandishi huwasilisha tajriba hiyo kwa kujikita katika tukio moja. Utu wa mgongo wa utanzu huu ni hadithi. (Mbatia 2000)

Utanzu huu pia umeelezwa na (Wamitila 2002), ambaye anasema, hadithi fupi ni utungo mfupi wa kinadhari unaojishughulisha na suala fulani kuu, wenyewe wahusika ambao hawakuzwi kwa kina na unaotumia mbinu za kimaelezo za kibarifupi, zenye uelekezi wa kiwango cha juu. Utungo huo hautumii mandhari kwa upana na una athari kuu ya umoja. Unaweza kusomwa kwenye kikao kimoja kifupi. Kulingana na (Wamitila 2003), utanzu wa hadithi fupi huwa na wasifu wa kimsingi unaoutofautisha na tanzu zingine, wasifu wenyewe ni kama ufuatao:

Wamitila (2003) anaeleza kuwa mwandishi wa hadithi fupi huhusisha kazi fulani na kipindi fulani cha kiwakati: Kwa sababu ya muda na upana wake, mwandishi wa hadithi fupi hana wakati wa kuelezea mambo, matukio, wahusika na migogoro kwa undani. Riwaya inaweza kuhusishwa na kipindi kirefu kwa sababu ya urefu wa muda alionao mwandishi.

Wamitila anaendelea kusema kuwa ufupi wa utanzu huu unaathiri uteuzi wa mwandishi wa mbinu za uandishi, uwasilishaji wake pamoja na athari nzima ya uandishi wenyewe kwa wasomaji. Kama tulivyotaja jambo hili ni kweli kwani kazi hii husomwa kwenye kikao kimoja kifupi ikilinganishwa na riwaya ambayo msomaji anahitaji vikao kadha kuisoma. Riwaya hujumlisha mbinu anuai za uandishi kutokana na urefu wake.

Wamitila (2003) anasema kuwa hadithi fupi pia huwa na idadi ndogo ya wahusika: Hadithi fupi aghalabu hujifunga kwa tukio fulani tu. Ili kulikuza tukio au tendo hilo, wahusika huwa wachache. Kuwapo kwa wahusika wengi huhitaji muda, kipindi na wakati wa kuwakuza, kuwaendeleza n.k. Mwandishi wa hadithi fupi hana wakati huo. Wahusika wa riwaya huwa wameelezwa ndani na nje kwa sababu ya urefu wa kazi.

Kulingana na mtaalamu huyu mandhari ya hadithi fupi si mapana: Aghalabu matukio ya hadiithi fupi hutokea mahali pamoja tu; yaani hayahusishi sehemu nyingi. Kwa sababu msisitizo mkubwa uko kwenye nini sio wapi yaani, tendo sio mahali. Tukilinganisha utanzu huu wa hadithi fupi na tamthilia na riwaya tunaona kuwa mandhari ya riwaya na tamthilia huwa yanabadilika badilika kulingana na kinachozungumziwa, yaani kinachotendeka kinatendeka wapi.

Kulingana na Wamitila, mwandishi wa riwaya anaweza kutumia usimulizi mgumu au changamano unaohusisha wahusika kadha. Katika hadithi fupi, usimulizi huwa sahili kwa kuwepo kwa masimulizi ya moja kwa moja au mhusika ambaye anatumwiwa na mwandishi kama jicho la kuangalia na kupima yanayotendeka, yaani mtazamaji.

Ni maoni ya Wamitila kuwa, mgogoro wa hadithi fupi unakuzwa mapema na kwa njia wazi. Katika hadithi fupi yoyote ile, kuna mhusika anayetaka kitu fulani, kuna mwingine anayempinga au anayemzuia. Kati yao kuna mvutano wa aina fulani. Mvutano huu ni msingi wa mgogoro. mgogoro huo ndio unaotutia hamu ya kusoma (kuleta tataruki) ili tujue ni nani atakayefanikiwa. Katika riwaya wahusika wanaovutana ni wengi yaani, huwa wamegawika katika makundi mawili na mwishowe kikundi kimoja hushinda. Kutokana na wingi wa matukio haya ya mvutano basi hadithi huwa ndefu.

Pia hadithi fupi huanza karibu na upeo wa hadithi, yaani mwandishi hana wakati, nafasi wala uhuru wa kutoa maelezo ya kujenga matukio hadi kwenye kilele. Tofauti na riwaya ambayo mwisho wake huwa ni kama mwachilio (*let-up*), mwisho wa hadithi fupi huwa na mkokotezo na msisitizo fulani. Wamitila (2003)

Wamitila pia anaeleza kuwa mwandishi wa hadithi fupi hana wakati wa kutoa maelezo mengi ya ufunguzi yanayouweka msingi wa matukio, wahusika au mandhari. Mwandishi anatoa maelezo mafupi tu ya mandhari, yanayotosha tu kama msingi wa tukio au tendo kuu. Inapotokea kuwa mandhari yamemulikwa sana huwa pana umuhimu mkubwa sana. Riwaya hutoa maelezo mapana kuhusu mandhari ambapo tukio linatendeka.

Mtaalamu huyu pia ameeleza kuwa mwandishi wa hadithi fupi husimulia na kutoa maelezo yake kwa njia ya uelekezaji kuliko uelezaji wa moja kwa moja kama ilivyo katika riwaya. Muda alio nao ni mfupi, kwa hivyo inambidi kuyaacha mambo mengi bila kuyasema waziwazi. Mwandishi humwachia msomaji nafasi kubwa ya kudhani.

Kulingana na maoni ya Wamitila hadithi fupi huweza kusomwa katika kikao kimoja. Kwa kuwa si ndefu msomaji anaweza kuisoma kwa dakika kadha tu. Huku kusoma kwa kikao kimoja ni muhimu sana kwa sababu msomaji anatia mkazo wake kwenye tukio linalotendeka bali hatui na kuanza kutafakari juu ya hali kama ilivyo anaposoma riwaya. Tunaposoma hadithi fupi hatutui kwa kipindi kirefu kuanza kutafakari tunayoyasoma kama tufanyavyo tuisomapo riwaya ambayo aghalabu huwa ndefu.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa badala ya kuwaonyesha wahusika wakiendelea na kukua kimawazo kama ilivyo katika riwaya, hadithi fupi huwaonyesha wahusika katika kipindi fulani tu cha mvutano, uwe wa nje (kuhusiana na wahusika wengine, hali fulani, tukio jingine) au wa ndani (kuhusiana na mhusika mwenyewe). Ingawa mwandishi wa hadithi fupi hana wakati wa kuwaendeleza wahusika, huwawasilisha kwa njia inayowafanya waonekane kama wahusika waliokuzwa kikamilifu. Kwa hivyo, hata kama tunawaona kwa kipindi kifupi tunahisi kuwa wamekamilika kabisa.

Mtaalamu huyu pia anaeleza kuwa mpangilio wa matukio ya hadithi, yaani msuko wa hadithi fupi ni sahili, sio changamano. Si ajabu matukio yakatiririka na kufululiza moja kwa moja kuanzia mwanzo hadi mwisho bila ya kwenda mbele (mbinu elekezi) au kurudi nyuma (mbinu rejeshi) kama ilivyo katika riwaya.

Vilevile Wamitila anaeleza kuwa mara nyingine mwandishi wa hadithi fupi hutumia mbinu zinazomfikirisha msomaji na labda hata kumshtua. Mwandishi hufanya hivi ili msomaji ayafikirie matukio fulani. Mbinu hizi ni kama mwisho ambao haukutazamiwa, mshtukizo wa kumalizia hadithi, ugeukaji fulani wa matukio au msuko n.k.

Kwa kuhitimisha Wamitila anaeleza kuwa mwandishi hana uhuru wa kuyapoteza maneno, kila neno au maelezo anayotoa lazima yachangie kwenye athari nzima ya hadithi fupi yenewe. Mwandishi hana uhuru wa kutoka nje ya maelezo au mkondo wa hadithi na kusimulia mambo ambayo hayahusiani na tendo kuu kama ilivyo katika riwaya. Sifa muhimu ya hadithi fupi ni: Ufupi na mkokotezo, uwazi na uwezo wa kuathiri.

### **2.3 Hitimisho**

Katika sura hii tulijadidili mitazamo mbalimbali kuhusu dhana ya mtindo yaani mtazamo wa Kiisimu, wa Kifasihi, wa Kiisimu na Kifasihi na wa mtindo kama mtu binafsi. Tuliunga mkono dhana kuwa fani na maudhui ni taaluma zenyе uhusiano kama wa ‘roho na mwili’ yaani zinategemeana, kwa sababu sio rahisi kwa mtaalamu kutenganisha kinachosemwa na maana iliyokusudiwa kuwasilishwa na mwandishi. Pia katika sura hii tulidhihirisha kuwa kila mwandishi ana sifa yake ya kuwasilisha kazi, sifa hizi hudhihirisha upekee wa mwandishi fulani. Sifa hizi tulizotaja ni kama zifuatazo: Lugha, dayolojia, usimulizi, wahusika, hisia za mwandishi, tamathali za usemi mandhari na uteuzi wa msamiati.

Tanza tulizochanganua zina sifa anuai zinazoufanya kila utanza kuwa na upekee wake ukilinganishwa na utanza mwengine kama tulivyozichanganua. Na mwisho tuligundua kuwa ili kuweza kueleza upekee wa mtindo wa mwandishi fulani, sharti mchanganuzi awe amesoma kazi zaidi ya moja za mwandishi huyo. Kazi hizi ndizo humwezesha mchanganuzi kuelewa mazoea ya mwandishi husika na ndio hudhihirisha upekee wa kazi yake.

Kwa hivyo kulingana na tanzu tulizoangazia ni wazi kuwa kila utanzu una upekee wake wa kimtindo utanzu wa riwaya una upana wa maudhui, wahusika ni wengi, mgogoro, mandhari, na tamathali za usemi huwa nyingi. Kwa upande mwingine tamthilia ina ufinyu wa maudhui, wahusika, mgogoro, mandhari na tamathali za usemi ikilinganishwa na riwaya, japo hatuwezi kusema kuwa ni wachache ikilinganishwa na hadithi fupi. Katika utanzu wa hadithi fupi wahusika ni wachache, maudhui, ngogoro, mandhari na tamathali za usemi ni chache ikilinganishwa na riwaya na tamthilia.

## **SURA YA TATU**

### **UCHANGANUZI WA TAMATHALI ZA USEMI KATIKA “MIMBA INGALI MIMBA”, “MWAVYAJI WA ROHO”, ZINGUO LA MZUKA NA YASINYA**

#### **3.1 Utangulizi**

Tulichunguza tamathali za usemi na hivyo tuliegemea upande wa tawi la semantiki kwa sababu ndilo tawi huchunguza lugha katika kiwango cha maana. Huchunguza maana ya maneno yanayopatikana katika lugha husika, iwe ya kifasihi au ya kiisimu. Pia tulizingatia viwango vingine viwili vya ukiushi ambavyo ni: Kiwango cha maandishi/grafolojia na kiwango cha umbo. Katika sura hii, tulishughulikia jinsi mwandishi alikiuka matumizi ya lugha ya kawaida ili kuleta maana mbalimbali katika kazi zake, na pia matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo ilivyofasiriwa. Tamathali za usemi tulizoangazia ni pamoja na: Majazi, jazanda, kinaya, njozi/ndoto na maswali ya balagha. Pia tuliangazia ujumbe uliojitekeza kutokana na maana iliyoibuliwa na ubunifu huu wa uteuzi wa tamathali hizi za usemi. Katika utafiti wetu, tuliangazia zile mbinu ambazo zilitufaa zaidi katika kuichanganua mada yetu.

##### **3.1.1 Majazi**

Majazi ni mbinu mojawapo ya kuwasawiri wahusika kando na mbinu ya: Maelezo ya mwandishi, maelezo ya wahusika wengine, matumizi ya mazungumzo, mwngiliano matini, ulinganuzi na mgotanisho. Mbinu hii pia hutumika kutaja mahali kulingana na kunavyoonekana au wakazi wake. Katika fasihi ya Kiswahili, majina huwa na msingi muhimu wa uhusika na pengine kutajia mahali wahusika hawa hupatikana. Kwa upande wa wahusika, mtunzi hutumia majina ambayo yanafumbata tabia, sifa au matendo ya wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi zinazohusika. Kwa njia hii, msomaji huweza kuifahamu tabia na wasifu wa mhusika kwa urahisi zaidi. Vilevile, mtunzi huweza kuchimuza mtazamo na mwono wake kuwahuwu wahusika fulani na hata mwelekeo wa hadithi nzima. (Wamitila 2008)

Mtaalamu huyu pia anaeleza kuwa, kuna udhaifu hivi kwamba msomaji hulazimika kuridhika na maoni ya mwandishi kwani hahushishwi katika uteuzi huu wa majina aidha ya wahusika au ya mahali. Mwandishi kwa upande wake ana uhuru wa kuteua majina kulingana na anavyoona

inafaa bila kufungwa na maoni ya wengine. Yaani, ana uhuru wa kifasihi. Majazi huweza kuainishwa katika aina mbili kuu ambazo ni:

- (a) Majazi bayana
- (b) Majazi fiche

Mifano ya mahali au wahusika waliopewa majina ya majazi ni mingi katika kazi hizi vinne kama tulivyoyachanganua.

### **3.1.1.1 Majazi katika “Mwavyaji wa Roho” (2011)**

Baadhi ya wahusika wana majina ya majazi. Mhusika mkuu katika hadithi hii ni Kitambi. Kitambi ni tumbo lililochomoza mbele kutokana na unene. Mwandishi alimpa mhusika huyu jina hili kutokana na tabia yake ya kujilimbikizia mali na kuwa na pupa ya kila kitu. Kitambi alikuwa daktari, mmiliki wa asilimia sitini ya maduka ya kijumla katika mji wao, mwanasiasa, mlanguzi wa mihadarati kupitia kwa mpwa wake Jael, mkubwa wa soko la uuzaaji na ubadilishaji wa hisa, alimiliki magari mengi na makubwa ya uchukuzi ya umma. Alikuwa na pupa ya vitu vingi vikiwemo biashara kama alivyoelezwa na msimulizi:

Niliyazuia mawazo yangu kuibwa na zogo hilo na kurejelea pale afisini kwa bwana Kitambi. Afisi kubwa na iliyomfaa mkurugenzi na mmiliki wa asilimia sitini katika maduka makuu yaliyokwenda kwa jina la Nionepaa. (uk73)

Sio tu maduka ya jumla bali Kitambi alimiliki biashara zaidi katika mji huo. Msimilizi alitueleza walipoenda kwa soko kuu na ofisi ya ubadilishaji wa hisa na uuzaaji, wakiwa na Jael, alisikia jina mzee na hakujua alikuwa nani lakini baadaye alipata kujua mzee ni nani kama alivyoeleza:

Nilisikia kila wakati jina la mzee. Sikujua alikuwa nani. Nilitanika kwa kuwa tangu awali nilijua jina mzee lilitumika na marehemu aliyejikuwa rais wetu mwasisi wa taifa letu tukufu. Lo! Mambo kangaja huenda yakaja. Mkubwa wa soko la uuzaaji na ubadilishaji wa hisa alikuwa Kitambi! Ndiye alikuwa mzee? (uk 75-76)

Kitambi alimiliki magari mengi ya uchukuzi ambayo yalikuwa makubwa na yaliyokiuka sheria au maagizo yaliyokuwa yametolewa na Wizara ya Uchukuzi, pengine ili yaweze kuwabeba

abiria wengi ili Kitambi apate faida nyingi. Magari haya hayakuwa na mikanda, dereva na makanga hawakuva sare na hayakusimamishwa kuangaliwa na maafisa wa trafiki kwa sababu wote walimfahamu ‘mzee’, kama tulivyoelezwa na msimulizi:

Kupitia pale kuliteka fikra zangu hata zaidi maana Wizara ya Uchukuzi ilikuwa imetoa tangazo kuwa magari ya abiria madogo yataondolewa mijini na badala yake mabasi kuchukua nafasi, ghafla bin vu kulikuwa na mabasi kama mia tatu katika mji. Yote kutoka kwa kampuni moja! Pia jina la mzee lilitajwa. Kazi ya mzee vile vile. (uk 76).

Bwana Kitambi pia alijihuisha na ulangazi wa miadarati kupitia kwa mpwa wake Jael. Madawa haya ya kulevyo waliyauzia vijana wa umri wowote. Naye Jael aliwatumia vijana wa miaka anuai kusambaza madawa haya kwa mashule kama alivyoeleza msimulizi:

Jioni hiyo Jael alikuja na marafiki zake kutoka mjini na wengine waliotoka katika miji na vyuo vingine katika miji tofauti. Kilichonizubaisha ni kwamba kulikuwa na wengine waliotoka katika shule za upili na hata waliodai walikuwa katika shule za msingi. Wote Jael aliwaita marafiki zake! Aliwapanga foleni kama wasichana wa maonyesho na utii wao ungemfanya rais fulani kuona wivu. Kwa kipindi fulani, kila mmoja alitoa maendeleo yake, changamoto na hatimaye mabunda ya noti yaliyositiriwa barabara. (uk 78)

Biashara ya ulangazi wa madawa ya kulevyo ilinoga na athari ya miadarati kwa vijana na jamii ikawa janga la kitaifa. Jambo hili lilzungumziwa hata kwenye vyombo vya habari, akina mama walikuwa wametamaushwa na hali ya kuatua moyo ya vijana wao iliyokuwa imesababishwa na matumizi ya miadarati. Haya yote yalisababishwa na ulafi wa Kitambi wa kutaka kupata pesa nyingi bila kujali kama alichokifanya kiliathiri jamii au la. Katika mahojiano ya vijana waliokuwa wanatumia miadarati na wanahabari, vijana hawa walikiri kuwa hawangeweza kukaa bila kutumia dawa za kulevyo na walikuwa wakinunua kucha ya madawa hayo kwa shilingi mia mbili. Walisema pia walipotumia dawa za kujidunga walitumia sindano moja, hivyo uwezekano wa kuambukizwa virusi vya ukimwi na magonjwa mengine ulikuwa juu sana. (uk 78)

Isitoshe Kitambi aliwania nafasi ya uongozi na kilichodhahirisha ulafi wake ni jinsi mama mmoja alivyopita mahala Kitambi alikuwa akifanya mkutano wake wa kisiasa, mama huyu alikuwa na bango la mheshimiwa mwengine, alipewa kichapo cha mbwa na wafuasi wa Kitambi. Zaidi kulikuwa mtoto mdogo, vijana saba na wakongwe kadhaa walioaga dunia wakati huo wa kampeni za uchaguzi, pia nyumba kadhaa ziliteketezwa moto. (uk 82) Mwandishi alikuwa akiwafungua wanajamii macho ili waelewe tabia ya viongozi wao. Waelewe jinsi viongozi walivyotawaliwa na unafiki katika maongezi yao, biashara zao na nia yao kwa wananchi. Wao walikuwa wakiwatumia wananchi ili waweze kufika wanakotaka kufika.

Mhusika Chumo alitumiwa na mwandishi kama msimulizi wa hadithi hii. Neno chumo ni sawa na pato, ni kitu ambacho mtu anaweza kuwa nacho baada ya kufanya kazi au biashara. Sawia na jina lake Chumo alizoea kujichumia kwa njia iliyohalali. Hata kama alikuwa rafiki wa karibu wa Jael (mpwa wa Kitambi aliyefanya biashara ya kuuza mihadarati kwa niaba ya Kitambi) msichana huyu (Chumo) alikuwa na msimamo dhabiti, hakugeuzwa na ushawishi wa Jael. Hata baada ya kupewa nyumba kwenye mtaa wa Ukwasini, alimrejeshea Jael funguo na kwenda kuishi vibandani, alipogundua kwamba Jael alikuwa akifanya biashara ya kuuza madawa ya kulevyo. Hakufuata tabia na mienendo ya Jael. Msimulizi alieleza ifuatavyo:

Mheshimiwa sijamwona tena. Tunapanda milima ya taka na kuruka majitaka asubuhi na jioni na wenzangu. Sote tukijivunia kuwa wafanyakazi wa bidii na waaminifu. Tena walipa ushuru. Ndio maana kila mwisho wa mwezi mimi na wenzangu hatunung'uniki wala kulalamikia kipato chetu. Fahari yangu ni kwamba mimi ni mlipaji wa mshahara wa mheshimiwa Kitambi. Basi, mimi ndiye mzee. Mimi Saida na wengine. (uk 82)

Mwandishi alikuwa akiieleza jamii kuwa kulikuwa na uwezekano wa kuwa na watu wazuri waliowajibika mionganoni mwa watu waovu. Pamoja na kuwa Chumo alikuwa mwandani wa Jael, alipata kipato chake kwa njia ya haki. Mwandishi alikuwa akiionyesha jamii kuwa sio lazima mtu afanye wafanyavyo wafisadi ili afanikiwe, hata wao wanaweza kuitwa 'mzee.'

Kulikuwa na maduka makuu yaliyorejelewa kwa jina Nionepaa. Msemo huu hutumika kumfukuza mtu katika nyumba. Katika matumizi yake mtu huambiwa, "nyumba yangu uione

paa.” Maduka haya yalimilikiwa na bwana Kitambi. Jina hili ni la majazi na lilitumiwa kuwakejeli wananchi wa kawaida, kuwa hawangeweza kuwa katika kiwango kimoja na bwana Kitambi au kupata maduka kama hayo na hawangeweza kufanya chochote ila tu kuyaona paa. Katika mji mzima, mtu binafsi kumiliki asilimia sitini katika maduka makuu ni kama ndoto kwa mwananchi wa kawaida. (uk 73)

Hoteli Nipewe ni jina la majazi, hapa ndipo wakubwa kama Kitambi na wenzake walipopatana ili kutimiza miadi yao. Kama tulivyoelezwa na msimilizi, Jael alitiwa ndani kwa sababu ya ulanguzi wa mihadarati. Baada ya Jael kuachiliwa, bwana Kitambi alimwagiza afisa mkuu wa polisi kutoka kituo ambako Jael alitiwa ndani, wakutane katika Hoteli Nipewe na alipewa kitu kama alivyoeleza msimilizi:

...Mzee alimpigia simu afisa huyo na kuagiza waonane katika Hoteli Nipewe jioni hiyo. Kama alivyosema baadaye Jael, afisa aliambiwa kauli moja tu, ‘chunga kazi isipotee.’ Kisha alipewa kitu ambacho angefanya kazi miezi kumi na miwili kabla ya kukipata kama hicho. Afisa alikubali kuwadhibiti vijana wake. (uk 77)

Mtaa wa Ukwasini ni jina la majazi, lilikuwa eneo waliloishi watu wakwasi. Ukwasi ni hali ya kuwa na mali nyingi sana au utajiri mwingi. Chumo alikuwa mtu wa pato la chini lakini, ili kuzilinda siri za biashara za Kitambi na mpwa wake Jael, alipewa nyumba ya kifahari katika mtaa wa Ukwasini. Msimilizi alitueleza yafuatayo:

Jael alinionya dhidi ya kupanua kinywa changu ovyo. Nilikuwa na uhuru wa kuagiza haja yoyote, hata gari la kifahari. Ndivyo nilivyoipata nyumba katika mtaa wa Ukwasini. Ulikuwa uthibitisho wa msemo, mgaagaa na upwa hali wali mkavu. (uk 77)

Mwandishi alikuwa akielimisha jamii kuwa viongozi fisadi au waovu wanaweza kufanya lolote ili kujifaidi na kuzificha siri zao, hata kama siri hizo zinayavizia maisha na uhai wa wengi kama walivyofanya Jael na Kitambi.

### **3.1.1.2 Majazi katika *Zinguo la Mzuka* (2011)**

Mwandishi aliwapa wahusika Mweusi na Mweupe majina ya kimajazi katika utangulizi wa maonyesho. Mwandishi alitueleza kuhusu ukoloni katika bara la Afrika, alikuwa akieleza kuwa Waafrika waliamini kuwa Mweupe (mkoloni) alifurushwa na Waafrika walikuwa huru, lakini hilo halikuwa kweli kwa sababu Mweupe ndiye waliywatawala Waafrika, kama walivyozungumza Mweupe na Mweusi:

**Mweusi:** (Kwa msukumo.) Nataka kuwa mimi! Mimi mwenyewe! Mimi ngozi, damu na nyama. Haya madhabahu ni yangu na watu Wangu! Wewe mbona unajirejesharejesha na kuyaingilia.

**Mweupe:** (Akicheka kicheko cha kusuta.) Nilikuweka pale. Nilienda mwili tu, roho ingalipo. Inaishi ndani yako. (uk 6)

Mweupe aliendelea kujishaua kuwa yeye ndiye aliyemtoa Mweusi matongo machoni, akamvisha nguo na kuyapanga madhabahu (serikali na uongozi wake.) Alindelea kumkejeli Mweusi kwa kumuuliza kama mwaafrika mweusi alijua uhuru au uongozi. Mwandishi alikuwa akiizindua jamii kuwa isiwe ikijiponza kuwa iko huru kwani viongozi wao ni Waafrika lakini Mweupe (mwakilishi wa nchi za magharibi) kwa mizuka yake alikuwa akimzingua Mweusi (mwakilishi wa viongozi wa nchi za bara la Afrika), na kuzitawala nchi za Kiafrika huku akizipora alivyonaka. (uk 6)

Tuliangazia mada *Zinguo la Mzuka*. Zinguo ni tendo la kumsomea mtu kurani, kumwombea kwa Mungu na kutoa sadaka ili asipate balaa, hasara au madhara. Mzuka ni kiumbe kisichoonekana ila hudhaniwa kuwa kinaishi na huweza kutokea mtu: pepo. Mwandishi alimlinganisha Zinguo na viongozi waafrika ambao walifaa kufanya tambiko katika madhabahu yaliyoltinganishwa na mamlaka au uongozi wa nchi na pia alikuwa na jukumu la kumfukuza Mzuka ambaye aliwadhulumu Waafrika, naye Mzuka alilinganishwa na viongozi wa nchi za kimagharibi ambao walizitawala nchi za Afrika kwa hila, utapeli na unafiki.

Mzuka alisawiriwa kama mwenye nguvu hivi kwamba Zinguo hangeweza kumshinda kwa chochote, alichotaka Mzuka alipewa kwa kumlaghai au kwa kumzingua Zinguo. Zinguo alifanya tambiko kumfukuza Mzuka, alibeba maji kwenye chupa, beseni, mkia na vikuku na alipojiandaa kufanya matayarisho haya ya tambiko, Mzuka alikuwa akimwangalia, tulielezwa kuwa Mzuka hakutishwa na tambiko. Zinguo alicheka kicheko kikubwa na kugaragara, ambacho kilidhihirisha ujinga wake kwani alitumia mbinu zilizopitwa na wakati na zilizotambulika na adui wake Mzuka. Tulielezwa yafuatayo:

**Zinguo:** (Akisimama barabara.) Tayari. Tayari sana! Hii ndiyo dawa yake! Kuanzia sasa hamtamsikia, hamtamuona, hamtamhisi katu! Mimi si wale wasemao bila kutenda nilimshinda baba yake, yeye ni nani? (Hadhira inanung'unika. Amesikia!) haya!...

Toka! Toka zimwi mla watoto wetu. Toka! jini mwiba mali yetu. toka! Nakuondoa kwenye ardhi yetu. Toka! Hutakaa tena ndani ya nyumba na afisi zetu. Toka! Naimarisha ngome ya uongozi!... (uk 11-12)

**Mzuka:** (Taratibu.) Bado hujakua! Bado hujakomaa na mbinu mufti za kujihami dhidi ya mibabe. Mizinga ya kukopesha. Mtandao huna! Angani hujafika. Elimu ya kupigana unayo? Mbinu zako zanuka! Dhaifu! (Anatema.) (uk 15) (Mzuka anacheka. Taratibu anaenda na kuketi alikokuwa ameketi Zinguo)... (uk 16)

**Mzuka:** Unahitaji moto. Moto ndio uangamizao. Hebu nitazame, (Anaamka na kujisheua jukwaani). Umeniondolea vumbi na sasa siha yangu ni imara... (uk 16)

Mwandishi alionyesha jinsi jamii za Waaafrika zilivyotawaliwa na Mzuka (mwakilishi wa nchi za magharibi) aliyezifilisi nchi za bara la Afrika hivyo kuwalazimu Waafrika kukopa, hawakuwa wameimarika kiteknolojia na mbinu zao za vita ziliwuwa dhaifu. Kama alivyosema Mzuka, maji hayajawahi kumuua mtu bali humsafisha mtu. Baada ya kujua haya viongozi wa Afrika bado waliendelea kung'ang'ana na Mizuka ya wakoloni, badala ya kutafuta njia mwafaka ya kujikomboa. Jamii pia ilikuwa ikizinduliwa ili iimarishe nchi kiuchumi na kiteknolojia. Imani potovu ya kutaka kukabiliana na mzungu mkoloni kwa kutumia maji yaliyoaminika kuwa na uwezo wa kuwakinga dhidi ya adui, ndio iliyowaangamiza Watanzania chini ya uongozi wa shujaa wao Kinjeketile walipokuwa wakiwapigana na Wajeruman. Mawazo ya Sanja yaliwiana na ya mwandishi wa tamthilia ya *Kinjeketile* (Ebrahim 1969), ambapo mbinu zao za kumpiga na kumfukuza adui ni duni, Waafrika ndio walioangamia badala ya adui zao.

Zinguo alichangia katika kuifisadi nchi ya Kusinyika kwa ujinga wake, alivishwa suti, kofia na kupewa fimbo, badala ya kuona unafiki katika uhusiano huo, Mzuka alijaribu kuujenga kwa kumpa Mzuka zawadi alizomwitisha, na pia Zinguo aliona utukufu. Alipomtimizia Mzuka mahitaji yake alivuliwa nguo zote na kuachwa uchi na wakati mwingine aliachwa amevalia mararu. Alipojipata uchi hakuwa hata na majani ya kujisetiri kwa sababu aliquwa amedanganywa na mzuka akayachoma majani yote kuvukiza vumba. Lakini Mzuka aliquwa akiyahifadhi yake kwa ajili ya kesho. Mwandishi alitueleza kuitia kwa sauti kutoka kwenye hadhira kuwa Zinguo alidhihirisha mjinga kama ifuatavyo:

**Sauti:** ...ukichoma yako, Mzuka amekueleza anafanya nini na yake: Anayahifadhi kwa matumizi ya kesho! Ndio maana huku hatoki. Kusumbuana ni mchezo unaompendeza, Unampa maarifa ya kusuluhisha matatizo ya kwao. (uk 41)

Waafrika walichukulia uongozi kama jambo la mzaha lakini Weupe waliutumia huo uongozi (mchezo) wao kusuluhisha matatizo ya kwao, walijifunza kwa makosa ya Waafrika. Afrika ilikuwa kama uwanja wa majoribio, wakati mchezo huo uliwharibikia Waafrika, kwa Weupe uliwaimarisha kwa sababu Weupe hawakurudia yale makosa Waafrika walikuwa wamefanya na kujipata mashakani. Weupe walilifili bara la Afrika na kuzinufaisha nchi za ughaibuni. Wananchi walipoerevuka na kujua haki yao waliwatafuta Mzuka, Zinguo na Kaza (mfanyakazi wa Zinguo) ili wawaadhibu kwa makosa yao, Mzuka alitorokea kulikokuwa na madini, viwanda na mashamba ya kunyakua, na kumwacha Zinguo mashakani. Hili liliwekwa wazi na Kaza alipokuwa akimweleza Zinguo walipofumaniwa na Wanakusinyika na kuwekwa jela. Alisema yafuatayo:

**Kaza:** ... hao marafiki zako, si sasa wako na watu wale wale, wakikushajiisha uwakalie? Hao ni mizuka na Mzuka kazi yake ni kula! Hajali anayemlisha! Kuliko na mlo ndiko anakotetea. Wewe sasa umechunjuka! (uk 85-86)

Mhusika Kachangia alihusika pakubwa katika kutatua mzozo wa Zinguo, Kaza na Wanakusinyika. Changia ni kusababisha ubaya au uzuri katika kitu. Aliielekeza jamii katika mwamko mpya kwa kuwapatia wosia wenye busara. Aliwaonya Wanakusinyika wasiyarudie makosa waliyofanya kina Zinguo na Mzuka kwa kuwaambia yafuatayo:

**Kachangia:** (Akicheka.) Siku zimebadilika. Tulibaguana  
kitambo sasa hakuna moto isipokuwa mnaowasha  
nyinyi. (uk 80)

Polisi Dira na Tumaini walipewa majina ya majazi yaliyobashiria jamii mpya yene mweleko na matumaini. Dira ni kifaa chenyehakrabu moja kinachomsaidia msafiri kutambua upande anaotaka kuelekea. Maana nyigine ya dira ni mawazo ya kufikiria na kupanga juu ya mambo ya baadaye. Tumaini ni imani kuwa upo uwezekano wa kufanikiwa au kupatikana kwa jambo fulani. Dira alimweleza Tumaini kuwa jamii ingepata mwelekeo mpya kwa kutumia ishara ya mtoto wa kike kuzaliwa (kiumbi wa kike huzaa na kutunza viumbe). Nayo maneno ya Tumaini yalidhihirisha matumaini katika nchi ya Kusinyika, aliposema kuwa jipu lingepasuka siku hiyo. Alimaanisha kuwa viongozi dhalimu wangeondolewa kwa makosa ya kufuja mali ya umma na tuhuma zingine nydingi za ufisadi. Tulielewa haya katika mazungumzo yao walipowaona Zinguo na Kaza wakikamatwa:

**Dira:** Mtoto wa kike amezaliwa. Tumaini kweli nakwambia.

**Tumaini:** Ulijuaje nawe Dira.

**Dira:** Huwasikilizi hao ndege? (Mwenzake anatega sikio.)

**Tumaini:** Leo jipu litapasuka! Wimbo utabadilika.

**Dira:** Tayari. (Anamwonyesha Kaza na Zinguo) (uk 88)

Mwandishi alitumia nchi ya Kusinyika kueleza matatizo wanayokumbana nayo wanajamii, mwandishi aliwarejelea kama Wanakusinyika. Sinya ni hali ya kutofurahia jambo, kitu au mtu; kuchukiza au kukirihi. Mwandishi aliwasawiri Wanakusinyika kama hadhira ambayo ilikuwa kimya wakati wa kuigiza hata wakadhaniwa kuwa wafu. Wakati Zinguo aliifilisi nchi, wao walikuwa kimya walinung'unika tu wala hawakuchukua hatua yoyote. Baada ya mambo kwenda kombo na hakuna kilichobaki cha kutoa kafara ndipo walizinduka. Walielewa fika kuwa ni Mzuka aliyenonya raslimali zao kwa nguvu, kwa unafiki na kwa kumzingua Zinguo, hivyo aliweza kujitwalia alivyopenda. Wanakusinyika walizinduka, walikuwa wenye hasira na wenye kusinyika. Tuliezwa ifuatavyo:

**Mtu 1:** Akafanya karamu za kula na kunywa! Sisi watu,  
alitukumbuka? (Watu wanaonyesha hasira. Wanasonya.)  
Huo ulikuwa moto wa Mzuka aliotutishia? Hatukuona  
wanaolia kwa ajili ya magonjwa? Hatukuona wanetu  
wanaogaragara chini. Tukampa Mzuka akameza viwanda,

akauza vyake huku na vyetu kwao tukafungiwa! Hata kuuza chondo huko ni sawa na jongoo kukwea mlima kwa siku moja! Vuguu vingi tu! (uk 81)

Mwandishi alikuwa akionyesha kuwa wananchi ndio wenyewe uwezo wa kujikomboa kutokana na minyororo ya viongozi dhalimu. Wanakusinyika walionyesha mabadiliko kwa kuyang'oa madhabahu na kuyasafisha (kuwachagua viongozi wapya.) Walikabiliana na kundi la Zinguo na kulishinda. Mtu 1 alitema akiwatania kina Zinguo na kusema kuwa ubinafsi na ukiritimba ulikuwa umeuua usisi. Mwandishi alikuwa akiieleza jamii kuwa 'sisi' ni kila mwananchi bila kujali kabilia au tabaka, lakini sio mtu na watu wao. (uk 81-82) Jambo lingine lililojitokeza hapo ni kuwa si vyema kwa wananchi kunyamaza hadi viongozi kuifilisi nchi na raslimali zake. Hivyo wananchi walikuwa wakihimizwa kuchukua hatua mapema. Wanakusinyika walipozinduka ndipo mama katika kijiji chao alijifungua mtoto, ishara ya matumaini na mwanzo mpya. (uk 98) Baadaye, Mtoto 1 na Mtoto 2 walipokuwa wakicheza wakati Zinguo na Kaza walikuwa wameshikwa waliipatia nchi yao jina jipya la Kusifika ishara ya mabadiliko. Sifika ni hali ya kupata sifa kwa mafanikio mazuri au utendaji mzuri wa jambo. Tulielezwa kuwa watoto hawa walikuwa wakishindwa kukimbia kwa sababu ya shibe, nchi ilikuwa imeimarika na chakula kilikuwa tele kinyume na hali ya hapo awali ya ufukara na njaa.

### **3.1.1.3 Majazi katika Yasinya (2014)**

Majina ya wahusika katika riwaya hii yalissawiri sifa, tabia au mazoea ya watu au mahali. Kusinya ni kuchukiza, kutofurahisha au kukirihi. Matendo ya viongozi wa Mabonde yaliwasinya Wanamabonde. Jamii hii ilikuwa imegawika katika makundi mawili: Kundi la kwanza lilikuwa la tabaka la juu la mabwanyenye fisadi na wezi wa mali ya umma, hawa waliishi katika mtaa wa Mabonde na Bwenyenye, kundi la pili likuwa la tabaka la chini na wale wa tabaka la kati amba walikuwa na utu, na waliishi katika mitaa ya Changu Kidogo, Umachocholeni, Kibisuswa na Kichochole. Mbinu ya majazi ilitumiwa kuendeleza ujumbe wa mwandishi kuptitia wahusika na mahali kama ifuatavyo:

Kulikuwa wahusika wakuu kadhaa, mmoja wao alikuwa Kijasiri. Jasiri ni mtu asiyekuwa na hofu, asiyegopa au mwenye kufanya mambo ya kishujaa. Alikuwa mke wa marehemu Halili, (halili ni mtu wa kuheshimika.) Kijasiri alikuwa mamake msichana Tumaini na mwanamke

jasiri. Ujasiri huu alidhihirika wakati aliwakabili dereva na taniboi waliompata njiani akiwa na mwanawe Tumaini wakielekea sokoni. Dereva alimsalimu ‘Hi sweetie’ naye taniboi akadai ‘Hallo’ wewe ni supuu.’ Kijasiri alisimama na kuwakazia macho na kusema yafuatayo: “Wanawake sio mikokoteni wala matambara ama jaa ya kutupwa taka. Ni watu na watu wanastahili heshima. Wana hadhi yao.” (uk 40)

Kijasiri alitumiwa na mwandishi kuwaadilisha wanawake kuiheshimisha jinsia ya kike. Pia aliwahimiza wanaume kuwaheshimu wanawake kwani hata wao wana hadhi yao katika jamii. Kijasiri na Asisi walitembelea afisi ya bima ili кудай malipo ya mumewe, alikuwa alipwe fidia hiyo baada ya mumewe kufa akiwa katika shughuli za kazi. Walimkuta mhazili pekee. Ingawa mlango wa mkurugenzi ulikuwa wazi, hawakuruhusiwa kuingia. Kijasiri alijua kuwa alikuweko lakini walikatazwa tu kuingia. Tulielezwa Kijasiri kwa ujasiri wake alitaka kuingia kwa nguvu:

Kijasiri alishikwa na ghadhabu akataka kuingia kwa mabavu lakini Asisi akamkamata... Ghafla wakili wa kampuni hiyo alichomoka kutoka ofisini humo. Asisi alijaribu kumsimamisha (Kijasiri) ili asiseme naye (wakili) lakini hakusimama. “Nilikwambia! Unaona walivyo?” Kijasiri alimwambia Asisi. “Siku ya siku itafika. Siku ya kufa kwa nyani miti yote huteleza,” Asisi akajibu. (uk 109)

Mwandishi alikuwa akiwazindua wanajamii kuwa wasiogope kuwakabili wanaowanyima haki yao, kwa sababu ni haki yao kuhudumiwa. Pia aliwajuza kuwa lililo na mwanzo lina mwisho na siku moja haki itatendeka. Kijasiri aligundua kuwa Kifuja, Mayowe, Dkt. Balaa na afisa Angusha walikuwa na kampuni iitwayo Maba ambayo walidai walichapisha vitabu pale, lakini kupitia kwa mvulana Kioshi aligundua kuwa walifanya biashara ya ulanguzi wa madawa ya kulevyta. Hili ndilo lililompelekea Kijasiri kuwekwa jela kwa sababu, kuna mtu aliyewajuza akina Kifuja kuwa Kijasiri alikuwa akichunguza biashara waliyokuwa wakifanya katika kampuni hiyo. Kijasiri alikamatwa kwa amri ya kina Kifuja na kutiwa ndani, akiwa jela alimwandikia mamake barua ambayo ilidhihirisha ujasiri wake. Alimweleza mama yake maneno yafuatayo:

*...naomba jambo moja. Usiseme napitia haya kwa sababu mimi ni mwanamke. La, mama. Sote tuna vivuli vinavyoning’inia kwetu kila tuamkapo na kukanyaga nje. Nashukuru kwamba kumbe katika kivili pia kuna kusitirika... (uk 120)*

kijasiri hakutaka mamake kudai kuwa yeye alikuwa akitendewa madhila haya kwa sababu ni mwanamke. Yeye alikuwa mkakamavu hivi kamba hakuruhusu fikra za taasubi ya kiume kumtawala. Mwandishi alikuwa akiizindua jamii kuhakikisha kuwa kuna usawa katika jamii, bila kuwagawanya watu kwa misingi ya kijinsia. Mwandishi pia alikuwa akiwahimiza wanawake kusimama kidete wakijua kuwa wao ni viumbe muhimu katika jamii sawa na wanaume.

Baada ya Kijasiri kuwa jela kwa muda mrefu ni kana kwamba hakukuwa na matumaini ya Kijasiri kuachiliwa huru. Kifuja na Mayowe ndio walikuwa wametoa amri ya Kijasiri kutiwa ndani na ndio waliotarajiwa kumtoa kwa ushahidi wao, lakini wote waliaga dunia. Kila mtu alikuwa ametamauka ndipo Asisi akawaza kumhusu Kijasiri na ujasiri kama ifuatavyo:

“Uliwapatanisha wangapi Kijasiri? Nyumba ambazo zilikuwa zinatoa cheche na ndimi za moto uliotokana na njaa, ukosefu wa karo au matibabu: Ukaleta huko amani na imani. Uliwafadhili wangapi wakati wewe na Tumaini mlikuwa hamna? Wangapi walikuja mikono mitupu wakaenda imefurika? Wakafumba na kufumbata ukarimu wako, mkawaondolea makunyanzi yaliyowazeesha hata vijana wadogo?”(uk 162)

Mawazo haya ya Asisi yaliudhihirisha ujasiri wa Kijasiri wa kung’ang’ana na hali ya umaskini ya Wanamabonde wenzake. Mwandishi alikuwa akiwahimiza wanajamii kuwa walinzi wa ndugu zao na wanaposhiba wajue kunao wanaolala njaa, hawana mavazi wala makao.

Kuna mhusika mwingine mkuu aliyeitwa Asisi, alikuwa mwana wa Mahiri na Emali, alimchumbia Kijasiri baada ya mumewe Halili kuaga dunia, alikuwa mtetezi wa haki za binadamu. Jina lake liliashiria falsafa yake maisha, kuwa watu walifaa kuishi kama jamii moja ya sisi na wala sio kuishi maisha ya ubinafsi. Alidumisha uhusiano mwema na wenzake kwa sababu alipotiwa ndani na Kifuja kwa tuhuma za kumuua mhadhiri, alitembelewa na marafiki wengi sana kama vile Kijasiri, Kipokeo, mamake (Emali) na babake (Mahiri), Alua, Juma, Ali, Anao, Mtaje, Kiulizi, Kipate, Sifichi, Liwazo na mkewe, Gwiji na mkewe na wengine. Asisi alilijali bara la Afrika na wana wa Afrika ndio maana alijipata mara kwa mara akiathiriwa na mawazo kuhusu maswala na matatizo yaliyozikumba nchi za bara la Afrika.

Baada ya Asisi kuachiliwa na kurudi nyumbani kwao, siku moja aliwaona ndugu zake wadogo baada ya shule wakijiunga na kundi kubwa la watoto ambalo lilikuwa limejiuanga na kufanya kundi kubwa – taifa. Alijiuliza kama walijua hatima yao siku za usoni. Mwandishi alitueleza yafuatayo:

Asisi alipowatazama, aliona tamaa, ari, nguvu na juhudzi za watu ambao walitaka kufanya mengi lakini wakakosa kuongozwa na cha kufanya. Kila mchezo walioucheza waliuchezatu. Lengo likawa ni kucheza tu. Humo mchezoni mkafichika talanta na vipawa kochokocho. Kwingineko wenyewe wangkuwa wamefaidi si haba. (uk 72)

Mwandishi katika sehemu hii alionyesha kuwa Waafrika wangepata viongozi waliokuwa na msukumo wa kuleta mabadiliko barani Afrika basi hawangeongozwa tu (hawangecheza ili wacheze tu) bali wangefaidi kutokana na uongozi huo. Nazo talanta na vipawa vilivyofichika mionganoni mwa wananchi vingetambulika. Asisi aliendelea kuwaangalia watoto wakicheza na hapo akawaza yafuatayo:

Alimwona mama ambaye alikuwa akgombana na watoto wake wachanga. Alikuwa amelala chini amewezwa na pia mgonjwa. Alikuwa akilalamika kwa uchungu. “Chuchu nimewapa mnyonye, mbona mnapigana? Mnaufanyia uadui mwili huu wangu, nani kati yenu anaweza kusema ana haki kuliko mwengine?” “Tamaa yenu ndio inawafanya mpigane. Na kila mkipigana mnaumiza mwili wenyewe ambao mnataka uwalishe. (uk 73)

Mwandishi alikuwa akisisitiza kuwa ilikuwa vyema kwa viongozi Waafrika kuelewa kuwa bara hili (mwili wa mama M A) lilikuwa la Waafrika wote, wakati walikuwa waking’ang’ania kilichomo (raslimali za nchi) basi walikuwa wakizirudisha nchi hizi nyuma kimaendeleo. Ilikuwa muhimu waelewe kuwa umoja ni nguvu na mali hii ilikuwa yao, kile walichokihitaji ni mwelekeo ili waache kuziharibu nchi za bara la afrika. Asisi alibaki pale na kuendelea kuwaza akilini mwake na ndipo alimwona mama akijikaza kujaribu kuwasaidia watoto wake hata akiwa katika hali ile ya unyonge na kugonjeka. Tulielezwa ifuatavyo:

Mama alijizoazoa kwa unyonge wake akakusanya maji beseni tano na kuwawekea pale. “Tumieni pamoja!” Aliamuru. Haikuchukua muda hata hivyo watoto wenyewe walianza ugomvi tena. “Hili ni langu! Huoni liko upande wa kwangu.” Mara kila

mtu alidai kumiliki lake au yake. Mwanzo maneno, kelele halafu yowe na hatimaye kibunga cha kurushiana. Mateke na mangumi... Walianza kuyavunja mabeseni na maji yakaanza kupungua nao wasione wala kutazama. Kila mmoja akamwekea mwenzake macho na kudhani wajibu wa kuzuia uharibifu zaidi ulikuwa kazi ya yule mwenzake na wala sio yake yeye. Ndio kweli panya wengi hawachimbi shimo? (uk 74)

Mwandishi alionyesha athari za matendo ya viongozi wa nchi za Afrika ya kutowajibika na ya ufisadi, badala ya kuleta maendeleo walisababisha mafarakano ambayo hakuna aliyetaka kuyawajibikia na kuyarekebisha. Mwandishi alionekaka kuashiria kuwa, kama nchi hizi zingekuwa na umoja na kutambua kuwa wao walikuwa Waafrika na walikuwa wakiliharibu bara lao, basi hakungepatikana hasara. Waafrika walikuwa wakijulishwa kuwa ni Afrika tu ambako ushirikiano ulizua mafarakano badala ya ufanisi mkuu. Katika usingizi Asisi aliona jinsi wana wa Afrika walikuwa wameshindwa kukiteguu kitendawili cha ‘sisi’ hata walipogawiwa ardhi walizozana na kuishia kupigana. Hali hii ilimfanya Mama Afrika (M A) kuwa taabani, siku zote aliishi katika uchungu kwa kuona jinsi watoto wake walivyofarakana. Mwandishi alitueleza yafutayo:

Asisi alihisi uzito wa mama mzazi. Mama mbebaji wa mimba, bila shaka mzigo unaouguza, unaotapisha na kutaabisha, unaomnyima mama usingizi na kumnyima kula aina fulani ya vyakula. Mama: Mlezi asiyechoka, aliye mtoto akilia... (uk75)  
Watoto wale walikuwa kana kwamba hawakumsikiliza mama yao. Waliendelea kukabiliana tu. Mara Asisi alimwona M A akigaragara kwa maumivu makali. Alishawishika kwenda Kumsaidia. (uk 77)

Alichokuwa akieleza mwandishi ni kuwa bara la Afrika lilikuwa taabani, nao wana wa Afrika hasa viongozi walikuwa kama viziwi hawakuisikia sauti ya mama yao aliyekuwa akiwarai kushirikiana lakini waliendelea kufarakana. Basi hali ya nchi za Afrika ilibaki kuwa ya kusikitisha (kugaragara kwa maumivu) yaliyosababishwa na wanawe. Asisi alikiwakilisha kizazi kipyu ambacho kilikuwa kimezinduka na kilikuwa tayari kulikomboa bara la Afrika. Zaidi Asisi alinukuliwa akimwomba mama M A ushauri kuhusu uongozi wa bara. Kama ifatavyo:

...alijipata kasimama mbele ya M A. “Hatima yako kuhusu konde na bonde hili?” Aliulizwa.

“Samahani mama. Naomba usichukulie ni mapuuza. Bado nahitaji Kuongozwa,”alijibu.

“Vizuri, vizuri kwani hutegemei nguvu za ujana wako na hekima ya dunia,” akajibu.

“Sikiza mwanangu: uhuru ni kujituma, kujinyima, ni kujinyima wengine wafaidi. Je, umewazia kuwapa wenzio kwanza mahali pa uchache?” M A alimuuliza. (uk 86)

Asisi alitumiwa kuwakashifu akina ‘sisi’ ambao hawakuweza kujinyima kwa sababu ya wengine, hawakuwa tayari kuomba mashauri yoyote kwa lolote walilofanya katika uongozi wao bali, walitegemea nguvu na tamaa yao katika uongozi. Mwandishi alikuwa akikizindua kizazi kipyä kuutegemea ushauri wa viongozi wenye akili razini kama mama M A ili waweze kurekebisha makosa ya viongozi wa hapo awali. Kwa haya wangeweza kuepuka kulisambaratisha bara la Afrika.

Kuna mhusika mwingine kwa jina Kipokeo, alikuwa rafiki wa Asisi na mtu asiyekuwa na elimu ya kiwango cha juu. Kupokea ni hali ya kuchukua kitu ulichopewa kutoka kwa mtu mwingine. Kipokeo aliachia masomo yake katika shule ya msingi. Alianza kufanya biashara ya ukahaba baada ya kuchapwa shulenii na mwalimu wa hisabati kwa kutolewa hesabu naye akagura shule ya msingi. Alipata kazi ya ujakazi kwa bosi mmoja ambaye alimkodishia nyumba na kumtaka wawe wapenzi, lakini alipogundua hakuwa peke yake, bosi alikuwa na msururu wa wasichana, basi aliiacha kazi ile ya ujakazi na akaanza kazi ya ukahaba. Tulielezwa ifuatavyo:

Alipochoshwa na kulea watoto wa wengine, Kipokeo aliazimia kujaribu vina vya maji mengine. Alianza Kung’ang’ana na maisha. Akaanza kuwapokea wavulana kisha wanaume wa kila hirimu. Kinolewacho hupata. Haikuchukua muda Kipokeo akapata. Wale wanene na wenye misuli aliwakadiria tu kwa kutazama na kujiambia kuwa hao wasinge kuwa na ndwele. (uk 20)

Vijana walikuwa wakionya dhidi ya kuyaacha masomo kwa sababu waliyaona magumu, hii ni kwa sababu hakuna kazi rahisi na Kazi zote zina changamoto zake, lakini walifaa kujua kuwa kisomo kina faida kwani baadaye mtu huweza kufanya kazi yenye mshahara bora ikilinganishwa na kazi zisizohitaji kisomo cha juu. Pia mwandishi aliwaonya vijana dhidi ya kufanya mapenzi kiholela, kwa kukisia kuwa mtu hana virusi. Mwandishi alitaka kuwakumbusha vijana kuwa virusi hugunduliwa baada ya mtu kupimwa na wataalamu wa matibabu. Vijana walionya dhidi ya kujihusisha na ukahaba au mapenzi ya kiholela ili kupata pesa kwa sababu ya uchochole, kwa

sababu kuna kazi zingine nyingi kama za kuuza bidhaa zinazohitaji mtaji mdogo. Mwandishi alikuwa akiizungumzia jamii kupitia maisha ya Kipokeo kama ifuatavyo:

Hata alipokuwa akisikiliza kijiredio chake kidogo ambacho kilikuwa kinatangaza kuhusu ARV, Kipokeo haukumpiga mshipa. “Kila mtu atakufa. Tena nkipata si mwisho wa kuishi. Ala! Kumbe kuna dawa ya kuzidisha uhai?” Alicheka. Wenye misuli hao aliwakubali mara moja kwa kibali chochote kile. Maskini! Umaskini ni balaa. (uk 20-21).

Baadaye Kipokeo alipewa mawaihda na Asisi na akakata shauri kurudi shulen. Wosia huo ulimbadilisha, alitafuta kazi akaifanya na akawa akisoma kwa wakati mmoja. Mhusika Kipokeo ni kielelezo cha madiliko, alikubali kubadilika na kujiunga na kikundi cha kina Asisi cha kuwatetea Wananchi. Vijana na wanajamii walikuwa wakihimizwa kuwa wanaweza kubadilika na kuunda jamii mpya.

Mhusika Kifuja alikuwa chifu wa Mabonde. Kufuja ni kutumia vibaya mali au pesa ni kutumia kwa ubadhirifu. Kifuja alikuwa na tabia zilizofanana na jina lake. Yeye na wenzake kina Mayowe, Chebaskwony, Dkt. Balaa na afisa Angusha waliifilisi jamii ya Mabonde kwa kujilimbikizia mali, walimiliki biashara takriban zote. Waliongozwa na tamaa iliyochangia kutengana kwa Wanamabonde katika matabaka mawili: Tabaka la matajiri na tabaka la maskini, kama mama M A alivyowaza:

...M A aling’ amua. Naam, yote yalianza kizazi cha akina Kifuja alipokubali kina Mayowe wawaongoze, wawaelekeze, wawashauri. Wakawashauri kuwa mpanda ngazi na mshuka ngazi hawapatani. Walipowashauri kuwa duniani kuna wana wakondevu na wana wanene wenye maumbo ya majitu wanaoghaniwa katika ngano za mazimwi, kina Kifuja wakasadiki... (uk 15)

Washauri wa viongozi huchangia pakubwa katika kuimarika au kuharibika kwa uongozi wa nchi. Viongozi basi walikuwa wakishauriwa wawe waangalifu katika uteuzi wa washauri wao, na watakapogundua kuwa kinachowaongoza washauri hawa ni ubinafsi basi wawapige kalamu. Mwandishi pia alikuwa akituaeleza kuwa ushauri kama huu ndio huwagawanya wanajamii katika makundi mawili: Mabwanyenye wenye kumiliki nchi na wachochole walala hoi. Kwa

hivyo viongozi wanafaa kuyaweka mahitaji ya wananchi katika nafasi ya kwanza ili wawasaidie kuinua kiwango cha maisha yao na kuimarisha hali zao.

Kifuja katika wadhifa wake wa chifu aliwateua wanakamati wa hazina ya ustawishaji maeneo ya Mabonde. Wananchi walimpendekeza Asisi awe mwenyekiti, lakini Kifuja alipendekezewa na Chebaskwony amteue Kipokeo. Kipokeo alitahadharishwa na nafsi yake kutokubali nafasi hiyo, hivyo alidinda kuichukua nafasi hiyo. Baadaye Kifuja alikutana na wale aliowateua pamoja na mkewe katika kamati hiyo na wakakubaliana wamtupilie mbali Kipokeo na nafasi hiyo ya mwenyekiti iachwe wazi. Jambo hili liliwapa fursa ya kufanya wapendalo. Kifuja aliwaambia wanakamati maneno yafuatayo:

Kwa sasa tutatia pesa kwenye akaunti zetu. Watu wakitaka kujua kwa nini miradi haiendeshwi kama maeneo mengine, waambie bado mwenyekiti anatafutwa,” Kifuja alisema. Visima vya maji vilichimbwa shambani kwake Kupe, kimoja kwa dadake Kifuja, kingine kwa rafikiye Shindo na cha nne kwa wakwe za Kifuja... Watu walipoteta walipata jibu hili; “Lazima miradi hii iwe na ulinzi madhubuti. Bado ni yenu tu watu watukufu hata kama kwa sasa imo katika mashamba ya watu binafsi.” Kelele za chura hazimzui ng’ombe kunywa maji. Hata majosho yalijengwa kwa namna sambamba na visima na si hayo tu. Mengine mengi yalifanyika. (uk 48)

Kamati zilizoundwa na viogozi hao zilijumlisha watu wa jamii yao na marafiki wa karibu wenye muonoulmwengu sawa na wao, walikuwa fisadi na hakukuonekana aliyeipinga mipango ya Kifuja na kamati yake. Mwandishi alituonyesha kuwa wananchi ndio huwaruhusu viongozi fisadi kuwatapeli, haya yote yalitendeka wakiwa wamenyamaza na walipopewa majibu ya aina hiyo hawakunekana kupinga. Wananchi wanazinduliwa ili wakomeshe vitendo vya vingozi kama hawa.

Mwandishi alionyesha jinsi Kifuja alijihuisha na ufujaji wa mali ya umma kuitia mbinu ya jazanda katika picha zilizochorwa na mwanawe wa kiume, ambaye hakuwa ametajwa kwa jina. Kila mara Kifuja alipomwomba mwanawe kumchorea michoro ya watu, ndege, wanyama, na almradi vitu asili na malighafi ya mabonde. Kifuja alichorwa na mwanawe akiwa ameshika ndani ya kinywa cha simba, simba huyu Kifuja alimlinganisha na afisi yake. Simba ni mnyama

anayewala wanyama na hata wanadamu. Basi huu mchoro ni jazanda ya ulafi na ufisadi wa Kifuja, alitumia afisi yake kufuja mali ya umma. (uk 49)

Mayowe Sokwe, alikuwa mume wa Sifichi na babake Kivuli (mtoto wa kiume). Alikuwa rafiki wa Kifuja na Chebaskwony. Yowe ni kilio cha sauti ya juu sana hasa kwa kutaka msaada, mhusika huyu alikuwa akitenda vitendo vilivyosababisha vilio kwa watu waliokuwa karibu naye. Alisawiriwa kama mtu asiye na utu hata chembe. Kama Wakristo wanavyosema injili huanza Nazareti ambako ni nyumbani, Mayowe alimpa mkewe Sifichi kichapo cha mbwa mara si moja. Siku moja alimpiga mkewe kwa sababu alikuwa amegundua mambo kadha kumhusu. Mwanzo Sifichi alikuwa ametambua jina la Mayowe la pili (Sokwe) ambalo hakuwa analijua, jina hili lilituwezesha kuelewa tabia yake ya hasira na fujo iliyofanana na ya sokwe aliyechokozwa. Pia siku moja mwanawe wa kiume Kivuli alimuuliza babake kwa nini alimgombeza mamake, lakini alimchapa kama tulivyoelezwa na msimulizi:

... siku moja alipigwa kofi ambalo karibu limpeleke jongomeo alipojaribu kumuuliza baba yake kwa nini alimgombeza mamaye vizuri tu. Baba mtu hakungoja swalilizame ndani ya akili zake. “Umefunzwa na mamako? Mwanaharamu! Umekuwa kama kivuli niendako, nakuona!” Kisha alivuta mkono na pa! Kilizabwa. (uk 143)

Isitoshe Mayowe alikuwa na mke wa kando waliyekuwa wamepata watoto naye, basi mtoto mmoja kati ya hawa alitumwa na mamake kwenda kumwitisha babake pesa kwani mtoto wao mdogo alikuwa ameaga dunia. Sifichi alikihoji zaidi kuhusu uhusiano wake na Mayowe na hapo kikamweleza kuwa babake alikuwa Mayowe na walikuwa wakitembea na kulala huko siku ya Jumatano wakati Sifichi alikuwa akienda kuuza vitambaa na fulana katika nchi jirani. Basi kutokana na ujasusi wake Sifichi alipewa kichapo cha kupigiwa mfano kama tulivyoelezwa:

... alipigwa, akapigwa na akapigwa. Mayowe alikuwa yumo kufadhaika kuwa kaua Kifuja alipowasili. “Mbona?” Mayowe aliuliza kana kwamba naye alikuwa mgeni. Alienda ndani akaleta karai ya maji baridi. Walisaidiana kummwigia Sifichi. Fahamu ziliporudi, waliondoka na kwenda zao, wakamwacha pale...(uk 146)

Vitendo vya Mayowe vilisababisha vilio kwa Wanamabonde k.v katika Mlaleo Academy alifukuzwa na usimamizi wa shule hiyo kwa sababu alikuwa akijihuisha na ulangazi wa madawa ya kulevyia kwa watoto wa shule. (uk 128) Lengo la mwandishi lilikuwa kuzieleza tabia za viongozi kama za ulangazi wa mihadarati, ambazo huathiri masomo ya wanafunzi na pia kusababisha kilio kwa wazazi wa watoto hawa.

Pia Kifuja na Mayowe walimiliki moja kati ya kampuni zilizotangaza kazi kwenye magazeti ya Mabonde kila siku, kazi hizi zilikuwa za udereva, upishi na kwa akina dada, kazi za nyumbani. Hazikutolewa bure Wanamabonde walihitajika kufanya jambo. Mwandishi alitueleza yafuatayo:

... zote walizitoa kwa kiasi fulani cha njenje. Kila aliyefika kwa mahojiano aliambiwa alitozwa pesa kwa malengo muhimu na wala sio kwa kuwabughudhi. "Kwa ajili ya kufanikisha mawasiliano na matangazo. Sisi hatupati kitu hapa! Tunawahudumia wazalendo wenzetu tu. Mungu atatulipa Inshallah..." Kwa kuhofia kuachwa nje, baadhi ya watu waliuza vikata vyao na wengine kuaweka jamaa zao kwenye madeni; baadhi waliomba loni za benki ili wapendwa wao wasafiri kupitia kwenye bahari kuu kwenda nchi ya maziwa na asali. (uk 130)

Hii ilikuwa njia ya kuwatapeli wananchi pesa kwa kisingizio cha kufanya mawasiliano na matangazo, kazi hizi ziliwahusisha watoto wadogo ambao walifaa kuwa shulenii. Viongozi bora wanafaa kuwa katika mstari wa kwanza kupinga ajira ya watoto na wala sio kuwauza au kuwatuma watoto wanakokumbana maafa kama kubakwa, kupigwa na kuchomwa kwa moto na waajiri wao.

Kuna mhusika Sifichi, neno ficha lina maana ya kuweka kitu au jambo mahali ili mtu mwingine asikione, jina hili ni ukasho wa neno ficha. Alikuwa mkewe Mayowe, na pia mamake Kivuli. Pia alikuwa mtetezi wa haki za binadamu. Kulingana na tabia yake kwa Mayowe na familia ya kina Mayowe ndipo tulielewa mbona mwandishi alimpa jina Sifichi. Tulielezwa kuwa kabla watengane na Mayowe alikuwa akiyakimu mahitaji ya familia ya Mayowe pamoja na shemeji zake. Mayowe alikuwa akimwomba Sifichi fedha na baadaye kukataa kuzilipa. Haya yote Sifichi aliweza kuyashughulikia kwa sababu alikuwa na mashine ya kushona fulana na vitambaa vyta mapambo, vingi aliviiza katika nchi jirani. Aliondoka Jumatano jioni na kurudi Jumaa asubuhi. Nyumba yao haikukosa kitu chochote kwa viwango vyta watu wa pato la kadiri. Mwandishi

aliwa akiwaelimisha wanawake kwamba wanahitaji kuwa na Siri kiasi ili kujiepusha na hali ya kuvunjwa moyo kama Sifichi.

Sifichi aliingia kwenye ndoa bila kutarajia, yote yalianza alipokuwa mwanafunzi wa shule ya upili aliponunuliwa jarida moja na Mayowe kutoka nchi jirani lililojulikana kama Mulika Nambari 16. Mayowe walifahamiana na Sifichi muda baada ya kumnunuliwa jarida hilo na wakati mwingine pia ambapo Mayowe alikuwa amejitolea kufadhili mkutano ulioandalialiwa na viongozi wa eneo kuwatuza washindi shulen i kwa akina Sifichi. Baada ya Sifichi kumchenga Mayowe kwa muda mrefu, kidogokidogo alijipata kwenye mtego wa Mayowe, wakati huu alikuwa msichana wa miaka 16. Kuna wakati Sifichi alikubali kuambatana na Mayowe katika Sukari Hotel na baadaye wakaenda Karata Lodge upande wa Njoro, siku hiyo Sifichi alijipata ameingia kwa mtego wa Mayowe, wakafanya tendo la ndoa na Sifichi akatunga mimba. Mayowe alimtaka Sifichi kuiavya mimba hiyo lakini Sifichi aliamua kumkwamia Mayowe ili amuo, kwa sababu aliona aibu kukaa kwao na pia aliona hatia kuavya mimba. Basi wakaanza kukaa pamoja kama mke na mume. Ujumbe huu wa mwandishi uliwalenga wasichana na hasa wa shule kuwa wao husema ‘la’ kwa wanaume huku wakimaanisha ‘NDIO’ bila kujua kuwa hawajakuwa na muda wa kutosha kufahamiana vyema, mwishowe wao hupata taabu maishani. Wanapogundua kuwa waliolewa na wahuni. Hivyo ni vyema kwa wasichana kukamilisha masomo yao na wafanye arusi kwa njia ifaayo, ili wapate Baraka za wazazi nao waume wao wawaheshimu.

Chebaskwony alikuwa mume wa Elimika (nesi) huko Mabonde, alikuwa babake Liwazo ambaye walitofautiana kimaadili. Alikuwa na wana wengine ambao hawakutajwa kwa majina lakini walifanana na baba yao kimaadili. Kulingana na maelezo ya mwandishi jina Chebaskwony lililinganishwa na mtu aliyependa wanawake wengi sana, lilikuwa sawa na wakoloni waliopenda koloni nydingi na pia viongozi waliokuwa na tamaa nydingi. Kama lilivyo jina lake, Chebaskwony hakutarajia kuwa angepata upinzani kwa chochote alichotenda. Mwanawe Liwazo alijiunga na kikundi cha kina Asisi na Kijasiri ambao walikuwa wapinzani wa Chebaskwony na aliweza pia kugura himaya na kasri ya babaye na kuwa mtu wa kawaida. Jambo hili lilimfanya Chebaskwony kuona kufedheheka, kudunishwa na kuumbuliwa hadi akapatwa na maradhi. Pia tulielezwa yafuatayo kuhusu tamaa yake:

Chebaskwony alipata ugonjwa wa mshtuko wa moyo kutohana na

tabia ya mwanawe ikabidi akimbizwe hospitali haraka. (uk 60) Kifo kilimwogofia Chebaskwony. Alikuwa amemaliza mradi wa maji ambao ulikuwa unamletea pesa kochokocco. Aidha alikuwa na majosho kochokocco...

Chebaskwony aliusta hata sukuma na mahindi choma na hata kuuza mbuzi sokoni katika minada mbalimbali. Chukua soko la muda karibu na darajani: Kina mama walitumia kibatari kuona nyakati za usiku ili wauze bidhaa zao. Hapo pia alikuwa na bidhaa: Alimradi nyanya, vitunguu na viberiti mbali na sukuma na kabichi. Athi – River ya chini pia alikuwa na mabanda...

Tetesi zilisema kuwa alikuwa na nyumba za kukodisha katika mataifa ya kigeni. Pia ilisemekana yeye na Kifuja walimiliki biashara kemkem zenyen fedha nyingi... (uk 61)

Viongozi waliochaguliwa walikuwa na ubiniasi kwani walichukua nafasi karibu zote za biashara hivi kwamba waliwazuia wananchi nafasi ya kufanya biashara. Mwandishi alikuwa akieleza wananchi kuwa ili waweze kukabiliana na shida kama hizi ingekuwa vyema wawachague viongozi wenye kuubeba mzigo wa wananchi. Mwandishi alieleza kuwa viongozi wanafaa kujiepusha na tamaa iliyokidhiri na waweke mahitaji ya wananchi katika msitari wa kwanza.

Huni ni hali ya kufanya mambo yasiyopendeza au yasiyo ya kistarabu. Kuna mhusika kwa jina Huni, alikuwa mjukuu wa Kifuja na aliishi Pwani baada ya kutumwa na babu yake huko ili asimharibie kura katika uchaguzi uliokuwa unakaribia wa Mabonde. Huni alikuwa mraibu wa miadarati na pia alijihusisha na biashara ya ulangazi wa miadarati kwa ushirikiano na babu yake Kifuja, wakati alikuwa Pwani na hata aliporudi Mabonde. Kabla ya kuwa ‘mdosi’ huni alikuwa akipanda bangi halafu akaanza kuiiza pamoja na madawa mengine ya kulevyia, Kifuja alijihami kwa kufanya urafiki na afisa wa polisi ili Huni asishikwe. Basi Huni aligeuka na kuwa mhuni kwa ufadhili wa babu yake. (uk 105) Ujumbe wa mwandishi ulikuwa wazi kuwa, vijana hutumiwa na wanasiasa kuijendeleza lakini wao hubaki nyuma na kuharibiwa maisha na viongozi hawa, vijana na jamii kwa jumla wanafaa wajue kuwa viongozi hawa wataongoza kwa muda tu halafu watatoweka. Swali ni je, vijana hawa hatimaye watakuwa wamefaidi nini?

### **3.2.1 Jazanda na Istiari**

Jazanda ni sawa na ‘kilichositiriwa’ Njogu na Chimera (1999). Wanasema kuwa mbinu hii hutumiwa kuelezea hali ambapo hadithi fulani inaweza kufasiriwa kwa namna tofauti. Wahusika au matukio yanayopatikana katika hadithi hiyo huwa na maana nyingine zaidi ya ile ya kijuujuu. Yaani kuna ulinganishi.

Ulinganishi huu unaweza ukakuzwa na kufanywa hadithi ambapo wahusika wake, matukio yake na muundo wake mzima, vinasimamia wahusika wengine na matukio mengine. (uk 32) Kwa mfano, katika “Mimba Ingali Mimba,” mhusika Nekesa ambaye alikuwa mja mzito alilinganishwa na nchi za bara la Afrika, nayo mimba yake ililinganishwa na raslimali, wanyama wa pori na utajiri unaopatikana katika nchi hizi. Utajiri huu ndio ulikuwa chanzo cha mvutano kati ya nchi za Kiafrika na nchi za Kimagharibi. Wanamagharibi wanazidunisha nchi za Kiafrika na mbinu zao za uzalishaji, nao Waafrika hawajiamini na wana mazoea ya kuzitegemea nchi za Magharibi. Hali hii ndio imechangia katika kukwama kwa nchi za Kiafrika kimaendeleo na kiteknolojia.

#### **3.2.1.1 Jazanda na Istiari katika “Mimba Ingali Mimba”**

Hadithi hii ni ya kijazanda kwani ilimhusu Nekesa mwanamke mjamzito, alikuwa mhusika mkuu katika hadithi hii. Nekesa alibeba mimba kwa miaka na mikaka na mtoto hakuzaliwa. Alipotaka kujifungua, mijadala ilikuwa ikizuka mionganoni mwa madaktari kutoka nchi za ughaibuni kuhusu atakapojifungulia, vipi? na kwa nini? Jambo hili lilifanya shughuli ya kujifungua kwa Nekesa ihairishwe kwa miaka minge. Nekasa hapa aliwakilisha bara la Afrika, mimba iliwalishaa raslimali zilizopatikana katika nchi za Afrika nao wakunga walikuwa na uamuzi kuhusu kujifungua kwa Nekesa waliwalishaa nchi za magharibi. Mwandishi alikuwa aktuonyesha jinsi nchi za Afrika ziliviyobaki nyuma kimaendeleo kwa sababu ya vikwazo zinavyowekewa na nchi za magharibi. Tuliangalia vikwazo kadhaa alivyowekewa Nekesa ndiposa akakawia kujifungua, kama msimulizi alivyotueleza:

Siku moja, madaktari na wakunga walikuja kumwambia wakati  
wa kuzaa ulikuwa umewadia. Aliupokea kwa hamu na ghamu...  
Alihisi minofu ikiongezeka mwilini. Aliona mfuko wa mtoto

ukipanuka ili kujiandaa kwa mgeni aliyejekuwa akitarajiwa. (uk 101-102)

Ari ya kuendelea, kuzaa na kuzalisha ilijengeka akilini mwa Nekesa (Waafrka) lakini tulielezwa kuwa bado hakujifungua mtoto hata kama wakunga walimtembelea tena kumpa matumaini na mafunzo ya uzazi, kama alivyoeleza msimulizi:

Alizinduliwa na daktari. “Uzazi jamani? Mtoto utakayemzaa ni wako. Je, unajua? Si wetu. Ndio maana nimekuja kukupa elimu ili utoe malezi bora. Lakini sasa twataka maoni yako. Sisi tunataka uzae wa kiume. Hapana! Wa kike... la! Mzungu... au Muhindi ama... ultaka kumzaa mweusi au mweupe? Na..., Ulitaka aabudu dini gani?” (uk 103)

Kulingana na maswali haya ilikuwa wazi kuwa madaktari kutoka nchi za magharibi ndio walikuwa na uamuzi kuhusu mtoto ambaye angezaliwa. Walionekana kutoa uamuzi wao na wala maoni ya Nekesa hayakuchukuliwa kwa uzito. Madaktari walidhihirisha udikteta katika maongezi yao. Mikutano iliendelea kufanywa ili kujadili vile Nekesa angejifungua mtoto wake lakini yeze hakupewa nafasi ya kushiriki mikutano hiyo na pia hakusikizwa. Tulielezwa yafuatayo:

Tena baada ya mafunzo, yaliyoandikwa kwa fotifoti, na kupelekwa huko mbali, kulikokuwa na taa nyingi, ambako usiku ulionekana kama mchana isipokuwa huo wa huko ulikuwa na rangi rangi hata kushinda za upinde. Kwa sababu wataalamu waliishi huko tu: Aliulizwa awachague wa kwenda kumwakilisha katika hospitali kuu ya kujifungua, kwa sababu yeze asingejua tofauti ya sindano, pamba, makasi, glavu na bendeji. (uk 104)

Waafrka walisawiriwa kama watu waliobaki nyuma kimaendeleo na kiteknolojia, Nekesa aliagizwa kumchagua mwakilishi ambaye angeweza kuelewa mambo ya wataalamu kama tulivyoelezwa. Jazanda nyingine iliyojiteza kuhusu kujifungua kwa mama Nekesa: Nchi za magharibi zilisawiriwa zikizidunisha mbinu za Waafrka za kuzalisha mali ambazo waliziona kuwa za kijadi na hawangeweza kuziamini (kazi ya wakunga ilionekana duni hawangeweza kumzalisha Nekesa). Madaktari tu ndio walioamini kuwa wangeweza kumzalisha lakini nia yao ilikuwa wabaki na mtoto (mapato). Kwa sababu Nekesa alikataa wito wa Wanamagharibi hakujifungua, mwandishi aliquwa akiilinganisha hali hii na nchi za Afrika ambazo zimelemazwa

na kubaki bila maendelao wala teknolojia kutokana na kutoshirikiana kwa viongozi kama mwandishi alivyotueleza:

Tena alikumbushwa kuwa asingehimili kizazi. Nyumba ya nyasi haihimili kishindo. Baada ya kushindwa kurairai, aliachilia na kukubali mtoto aandalawe mazingira na malezi na wakunga huko katika hospitali kuu. Hata hivyo anasikia madaktari wakisema, wakunga hawana utaalamu wa kumzalisha mtoto wa Nekesa. Wanataka madaktari tu, wafanye kazi hiyo.

Nekesa yuko pale pale. Paa la nyasi la nyumba yake linavuja matone ya mvua. Nje, moshi mzito unafunika paa na kulifanya lionekane jeupe kama ukungu wa asubuhi, wa macheo. Anaonekana kanyong'onyea na kutamaukiwa si haba. Kipato chake kidogo kiliisha alipokuwa akila vizuri, na kujibidiisha katika masomo ya uzazi. "Nangoja mtoto azaliwe." (uk 106)

Taswira ya nyumba ya Nekesa ilikuwa jazanda ya umaskini nako kubaki kwa nyumba hiyo kwa muda ni jinsi nchi za Afrika hazijakuwa uhuru na ilioneka kuwa bado zingeendalea kuwa chini ya himaya ya nchi za magharibi. Zilionekana kubaki nyuma kimaendeleo kama watu walio kwenye giza hawajui chochote. Waafrika walikuwa wanazinduliwa na mwandishi ili wajikomboe na kujifanyia maamuzi kuhusu maendeleo ya nchi zao ili wasikwame kama Nekesa ambaye alibeba mimba kwa miaka mingi sana kutokana na vikwazo vyta madaktari (viongozi wa nchi za Magharibi). Mwandishi alieleza yafuatayo kuonyesha hali ya kutamauka ya bara la Afrika: "Siku zinapita, majuma yanapita. Miezi inapita na miaka inapita. Nekesa anasubiri mtoto azaliwe. Subira huvuta heri na sisi tunangoja. Nekesa! Atapata uchungu wa kuumwa kizazi lini? Wimbo nao umenata mdomoni:

*Akiumwa huhisije?  
Akija husukumwaje?  
Akikwama iweje?  
Sipozaa itakuwaje?  
Nangoja.*" (uk 107)

### **3.2.1.2 Jazanda katika "Mwavyaji wa Roho" (2011)**

Mwandishi alitumia mbinu ya jazanda kueleza kuhusu hali ya nchi za Afrika. Chumo alipofika ofisini kwa Kitambi aliwapata kina kitambi na wenzake wakisikiliza habari juu ya rais mstaafu wa nchi fulani huko ughaibuni, rais huyu mstaafu alikuwa amefunguliwa mashtaka kwa kufuja pesa za umma wakati alikuwa meya kwa kuwaajiri wafuasi wa chama chao. Akina Kitambi

walisonya walipozisikia habari hizo, na ndipo chumo aliwaza na kulilinganisha swala la ujisadi Afrika na giza. Chumo alijizungumzia maneno yafuatayo: "Ndio maana ya kuwa mtu mweusi, kila kitu cheusi na kiza kumeza na kuyaficha mengi yasikuche na macheo. Kana kwamba uadilifu na uajibikaji pia ni mweusi." (uk 72)

Kulikuwa na Jazanda ya hali ngumu ya maisha Waafrika, hali hii ilisababishwa na ukosefu wa ajira na jinsi vijana walivyoathirika na madawa ya kulevyo. Hali hii ilichangiwa na ujisadi na tamaa ya viongozi ambao walikuwa wakiwauzia vijana mihadarati pia waliwauzia nafasi za kazi badala ya kuzitoa kwa umma bila malipo. Viongozi hawa walijitia hamnazo kuhusiana na ukosefu wa ajira mionganoni mwa vijana. Tulismuliwa jinsi meya wa mji huo alivyomwandikia mkurugenzi mmoja barua ili kumnyang'anya tenda ya kuzoa taka katika miji mikuu mitatu. Kulingana na meya alisema kuwa alimnyang'anya tenda hiyo kwa kuwa alikuwa akiingilia kazi ya ndani ya baraza la mji. Naye mkurugenzi huyo alikana madai hayo akasema kuwa, alikuwa akinyang'anywa tenda hiyo kwa kuwa hakumlambisha mkono. (uk 72) Jazanda ya utoaji tenda na athari ya ukosefu wa ajira ilisawiriwa na mwandishi kama ifuatavyo:

Tenda hiyo ilijikunyata na nafasi mia mbili za ajira ya vijana wa kike na Kiume. Ukipita katika uwanja wanakobarizi watu wa mjini wakati wa Chamcha, sio ajabu utawaona vijana wanaojilalia hoi, wengine na misokoto ya bangi, wengine wanajidunga sijui dawa gani na wengine hata hawajui ni mchana, wanashikana mchana wa Mungu, tena mbele ya hadhara kutaka kufanya kitendo cha ndoa. Na utawaona wenzao hawashughuliki ama wanamsihi mwengine apeane tunda aache kusumbua. Sasa umma haupumziki hapo tena maana ni hatari kwa usalama haikuwa ajabu kwa wakazi wa mji. (uk 73)

Viongozi wa jamii iliyosawiriwa na mwandishi walihatarisha maisha ya wananchi badala ya kuwalinda. Mwandishi alitueleza kuwa Kitambi alimiliki hospitali na aliitumia kama mahali pa kufanya mapenzi na wasichana wadogo. Alifanya mapenzi nao kwa lazima au kwa hiari, tulielezwa haya wakati Chumo rafikiye Jael alikuwa ametumwa na Jael akamweleze Kitambi kuwa, Jael alikuwa ametiwa ndani kwa sababu ya ulangazi wa mihadarati. Kitambi ambaye alikuwa kiwakilishi cha viongozi wa nchi za Afrika alilinganishwa na jogoo, nao wasichana walilinganishwa na vifaranga. Kama tulivyoelezwa na msimulizi:

Ndipo ilikuja akilini. Jael aliniambia ami yake aliwapenda wasichana wadogo. Aliwapima mwenyewe kuhakikisha hakujiathiri. Kisha alifanya ya jogoo kukiparamia kifaranga na kuwazawadi hela nyingi. Hakumrudia kiweto kwa mara ya pili. Alikaa na kuchongea wengine ... (uk 74)

Pia mwandishi alituonyesha jinsi viongozi wa nchi za Bara la Afrika walikuwa wamejiami kuifilisi jamii, vijana nao hawakuwa wakichangia katika ujenzi wa jamii kwa sababu walikuwa wameathiriwa na madawa ya kulevyo hivyo hakuna kazi waliyoimudu. Mama mmoja alikuwa akizungumza katika runinga kuhusu hali ya vijana katika jamii hiyo, aliwarejelea viongozi kama papa na nyangumi katika mazungumzo yake. Alisema yafuatayo: “Tumezaa wana wetu na kuwalea vyema, sasa nyinyi na biashara yenu muwafanye vizuu! Mimi nafa jamani! Hakuna wa kuwadhibiti hawa papa na nyangumi? Uuuui!” mama alilia. (uk 79) Mama huyu alikuwa kiwakilishi cha jamii iliyokuwa ikilia kutokana na udhalimu wa viongozi waliojipenda na hawakuwajali waliowachagua. Hata hivyo jamii hapa imesawiriwa kama iliyozembea katika kuwfurusha viongozi waovu na kuwachagua wanaostahili.

### **3.2.1.3 Jazanda katika *Zinguo la Mzuka***

Mweusi na Zinguo walifananishwa na viongozi Waafrika ambao walikuwa wamekosa msimamo dhabiti katika uongozi wao. Tambiko walizofanya hazikufua dafu kwa sababu hazikuwfukuzilia mbali Mzuka na Mweupe waliolanganishwa na viongozi wa nchi za magharibi. Zinguo na Mweupe Walidhihirisha kuwa hawakuweza kuwaondoa Mweupe na Mzuka nao Mweupe na Mzuka walikuwa wamekataa na wala hawakuwa tayari kubanduka katika uongozi wa nchi za Afrika.

**Mweupe:** (Anamtazama kwa uchungu.) Tutaona!  
Tutajua mbivu na mbichi.  
Nitaona kama utachinja kwenye haya madhabahu.  
Watu wako wazinguliwe wawe huru na kufanya sherehe  
za ushindi wako! Ukinichezea kimbunga kitaingia  
humu na hutaweza kukizima. (uk 8)

Mzuka aliwarejelea Mweupe na mzuka kama shetani, (uk 31) yaani, viongozi wa nchi za magharibi. Waliifilisi nchi ya Kusinyika huku wakiziendeleza nchi za magharibi kwa chochote walichokinyonya kutoka nchi ya Kusinyika. Waliwazingua Zinguo na Mweusi halafu wakaitawala nchi ya Kusinyika kwa ulaghai, kwa ushawishi au kwa mabavu. Zinguo alitaka

kutoa kafara katika madhabahu ili kuwafukuza Mweupe na Mzuka, aliwaomba wananchi wamletee nafaka au mifugo wa kutoa kafara, Wanakisinyika hawakupata chochote cha kumpeleke. Walikuwa wamempatia kila kitu naye kwa ujinga wake alikuwa amempa Mzuka. Wanakusinyika walimjibu ifuatavyo: "Hatuna! Umechukua yote na kuwazawadia mizuka. Hatuna! Hii mili ni kavu, hata jasho haina. (uk 49)

Wakati mchezo ulikuwa ukiendelea kuigizwa hadhira ilikuwa kimya hadi ikafananishwa mara kadhaa na wafu, vizuu, kaukau, vifyefye, maiti na mizuka. Mzuka aliwaita hivi kwa Sababu, kama wananchi hawakujifurukuta wala kuonekana kufanya chochote dhidi ya kiongozi wao Zinguo alipokuwa akiyatuma madhabahu vibaya. Hii ni taswira ya nchi za Afrika zilizopotoshwa na viongozi wao huku wakibaki kimya. Mwandishi alitueleza kuhusu kunyamaza kwa Wanakusinyika kama ifuatavyo:

**Zinguo:** Hawa ni mifupa. Vifyefye: kama kaukau kwenye kikaango (uk 21)

**Zinguo:** Hawa wafu wanajua haki ama ni watu wa tumbo tu?

**Zinguo:** (Akijizungumzia.) Watu vizuu: Watu mizuka hao! Mkono mtupu haulambwi...

**Zinguo:** Ni mizuka tu.

Wamekufa ijapo wapo hai na macho yanapepesa. (uk 23)

### **3.2.1.4 Jazanda katika *Yasinya***

Mwandishi alimbuni mhusika wa kufikirika mama M A, ambaye alimlinganisha na bara la Afrika. Mama huyu alikuwa na huzuni na uchungu kwa kuwaona wanawe walivyokuwa wakimvua nguo hadharani (uharibifu wa mazingira) na walivyokuwa wakipigana kwa sababu ya ardhi na malighafi. Hali hii ililingana na jinsi nchi za Afrika hupigana badala ya kushirikiana ili zifaidi kutoka kwa ardhi na raslimali zinazopatikana Afrika. Viongozi hawa walisawiriwa kama wasiojali kuzihifadhi raslimali hizo kwa mahitaji ya kizazi cha kesho. Walioliharibu bara walilinganishwa na wanaume walio kuwa na nia ya kumharibu mama M A. Tulielezwa kuwa kijasiri alipata ndoto kumhusu mama M A na wanawe, mama huyu aliwaza kuwahusu watoto wake kama ifuatavyo:

Hakuna ambacho kisingeuzwa na watu hawa na watu wao. Lo!  
Kumbe tamaa inaweza kuwa kali na ghali hivyo? Na huu ndio ugonjwa na sumu iliyokuwa ikiwaua wana wa M A. Alitazama katika mawazo na kuona ramani ya bara la Afrika. Afrika, naam bara kuu. Afrika ililinganishwa na mwanamke mrembo. Ni

mrembo ambaye anang'ang'aniwa na wanaume ambao wana nia ya kumharibu. Aliwaza kuhusu hao wanaume waharibifu. (uk 12)

Mwandishi alitumia mbinu ya jazanda kuieleza hali ya mioyo ya viongozi wa Mabonde, iliyogeuka kuwa mawe na miamba ambayo haingeweza kuhisi, kusikia wala kujali. Mikono yao ilitwaa bila kukoma. Vinywa vyao vikafyonza bila kuchoka. (uk 31) Mwandishi alikuwa akituonyesha jinsi viongozi katika jamii ya Wanamabonde walivyokuwa wakijihuisha na ujisadi hasa viongozi, ndiposa aliwalinganisha na vitu visivyozea kuhisi uchungu wala kuwa na utu. Alikuwa akiieleza jamii kuwa matendo kama haya huwaadhire watu wanaoongozwa ambao pia wana haki ya kuishi na kufaidi kutokana na raslimali za nchi yao.

Mwandishi alieleza tabia ya Kipokeo kupitia jazanda ya mwili kugeuka kuwa duka (uk 35). Kipokeo alipoacha shule na kujaribu kazi ya nyumba ikamshinda, aliamua kuuza mwili wake yaani, kushiriki katika ukahaba. Mwandishi alitueleza kuwa alijuza ndiposa apate kibaba. Mwili wake ulilinganishwa na duka. Ujumbe wa mwandishi ulikuwa: vijana wengi waliathiriwa na hali ya ukosefu wa kazi na hata uzembe, hawakutaka kujikaza maishani, walitaka kazi zilizopatikana kwa urahisi na zisizochosha. Ndio maana walikuwa wakijihuisha na ukahaba ili waweze kujikimu maishani. Kipokeo aliwakaribisha vijana kwa wazee, wanene kwa wembamba, warefu kwa wafupi bora walitoa pesa.

Picha iliyochorwa na mwana wa Kifuja wa kiume ilimlinganisha Kifuja na jitu. Tulielezwa yafuatayo: “Baba mwenyewe licha ya kwamba alikuwa ameketi, alionekana kuwa mrefu kuishinda nyumba yao, tena mnene mara tatu kupita mlango wa nyumba hiyo yao ya msonge” (uk 49). Kulingana na maelezo haya ni wazi kuwa Kifuja alikuwa akijilimbikizia mali ya umma, akala na kunenepa kama jitu. Hii ni jazanda ya ubinafsi na tamaa ya viongozi fisadi.

Asisi alituhumiwa na Kifuja kwa mauaji ya mhadhiri mmoja, baadaye Asisi alitambua kuwa msichana (Deni) alikuwa ameshirikiana na Kifuja kumuua mhadhiri huyo, basi Asisi alienda kumkabili na katika ugomvi wao Asisi aliwalinganisha Deni na wenzake, na kupe na mbung'o. Nao wananchi walilinganishwa na ng'ombe. Ni wazi kuwa Deni alikuwa mmoja wa wachache waliokuwa wakiibia nchi ya Mabonde na kuwadhulumu wananchi, hawakuwajali

waliowachagua ilihali Wanamabonde ndio waliowalipa kwa kodi waliyotozwa. Asisi alimkaripia Deni ifuatavyo:

Kupe mnyonyaji. Mbung'o muua ng'ombe. Mbung'o! Raha yake kuona ng'ombe akirorama kwa maumivu mengi. Kisha amwone akitoka mbio, mkia juu badala ya kutulia ale nyasi. Katika ufu mbung'o ananyonya damu gani? (uk 59)

Mwandishi aliangazia hali ya Mabonde wakati tu Asisi alikuwa ametoka jela. Hali ilikuwa mbaya na ya kuogofya kwa sababu usalama wa mwananchi ulikuwa ukihatarishwa na viongozi wa Mabonde. Bundi ni ndege wanao husishwa na maafa katika jamii nyingi za Kiafrika walitoa milio ya kutisha, nao mbwa walibweka kuashiria kuwa kulikuwa na hatari. Wanyama hawa walilinganishwa na hali ya hatari ya nchi ya Mabonde. Hali yenewe ilisawiriwa ifuatavyo: "Bundi waliofanya viota karibu na hapo kwao walirorama na kuwafanya mbwa kubweka katika kijiji chote." ( uk 76)

Mjukuu wa Kifuja kwa jina Huni, alikuwa akiogopwa na kila mtu kwa sababu alimfanyia Kifuja kazi, biashara aliyokuwa akifanya ya ulangizi wa madawa ya kulevyia pia kwa sababu alikuwa mraibu wa madawa ya kulevyia, basi hizo zilikuwa sababu tosha za kuwafanya watu kumwogopa. Asisi alimlinganisha Huni na nyoka, aliposema kuwa hata shetani alimwogopa. Tulielezwa kumhusu Huni kama ifuatavyo: "Asisi hakuamini. Nani angeweza kumshika huyo nyoka? Alijua Huni aliogopewa hata na shetani mwenyewe. Shetani na foko jembe lake asingeweza kumshtua mtu kama huyo. Nani?" (uk 106) Kifuja, chifu wa Mabonde na mjukuu wake Huni walikuwa tishio kwa jamii badala ya kuwasaidia na kuwalinda wananchi waliohitaji kulindwa.

Kijasiri alifanya m Kutano na kijana aliyeitwa Kioshi, Kioshi alikuwa akifanya kazi kwa kampuni iliyomilikiwa na Kifuja, Mayowe, Dkt. Angusha na afisa Balaa. Alikuwa ameacha kuwafanya kazi kwa sababu aligundua kuwa kama angeendelea kuwafanya kazi, mwishowe angegeuka na kuwa mraibu wa madawa ya kulevyia. Alifaalu kutoka huko kwa kudai kuwa alikuwa mgonjwa na hata ikambidi kutorokea eneo tofauti na lile walilokuwa wakifanya biashara hiyo. katika mazungumzo yao kioshi alijilinganisha na kunguru na nyumba ya nyasi, nao viongozi aliwalinganisha na papa, nyangumi na chewa. Alisema maneno yafuatayo: "... sio rahisi

kushinda vita dhidi yao...” “Mbele ya papa na nyangumi? Ama niseme chewa.” (uk 126) aliendelea kueleza zaidi, “Nimekimbia huku mimi kunguru kuponya ubawa wangu. Mimi ni nyumba ya nyasi sihimili vishindo. (uk 127)

Baada ya Mayowe kugundua kuwa mkewe Sifichi alikuwa amekipata kijibarua alichokuwa ametumiwa na mke wake wa kando, alimpa kichapo cha mbwa. Kijibarua hicho kilikuwa kikimwarifu kuwa mtoto wao alikuwa ameaga dunia. Mwandishi aliyalanganisha matendo ya Mayowe na ya mnyama kama ifuatavyo: “... aligeuka mnyama. Alichukua mshipi na kuanza kumcharaza mke wake. Alimpiga bila mwisho. Hakujuu kuwa Sifichi alianguka chini na kuzirai. Kifuja ambaye alikuwa amekuja kumpa pole rafiki yake ndiye aliyegundua kwamba Sifichi alikuwa hapumui. Walimmwagia maji kumwamsha. Sifichi aliwekwa kitandani alikokaa na kugaragara kwa mumivu usiku kucha. (uk 139) ulinganishi huu unamfananisha Mayowe na mnyama kwa sababu hakujali kuwa Sifichi angeaga dunia kutokana na kichapo hicho bali walimwacha akiwa katika hali mbaya na kwenda kujivinjari. Tabia yake ililingana na jina lake Sokwe. (mnyama)

Kuna jazanda ya mabadiliko wakati mambo yalianza kuwageukia viongozi fisadi: Kifuja, Mayowe na Chebaskwony. Wote mauti yalikuwa yakiwanyemelea. Hali ya anga ilionyesha dalili za mvua kubwa kunyesha, mvua ni dalili ya mabadiliko na matumaini ambayo huleta mazao mashambani na kubeba uchafu kutoka kwenye mazingira. Hivyo wakati ulikuwa umekaribia wa Wanamabonde kupata uhuru wao baada ya viongozi dhalimu kuondoka katika mamlaka. Wakati huo Mayowe alikuwa amelazwa hospitalini akiwa katika hali mahututi, naye Kifuja alikutana na Chebaskwony ili wapange jinsi wangeweza kuyalinda maisha yao kwa sababu walisema kuwa maisha yao yalikuwa hatarini, kama walipokuwa wakizungumza, mwandishi alitueleza yafuatayo:

Kule nje, mawingu yalijikusanya na kufanya wingu kuwa jeusi tititi. Mara ndege walirejea viotani na nchi kunyamaza ji... Ubaridi ulianza kujipenyeza ndani ya sebule ya Chebaskwony. Yeye na mgeni wake (Kifuja) wakaanza kuhisi baridi. Hakuna aliyenena na mwenzake. Kwa mbali Chebaskwony aliwaza juu ya wake zake saba na himaya zake mbalimbali.” (uk 151)

Mwandishi alitumia jazanda kuyaeleza maisha ya mwanadamu, Mayowe aligundua alikuwa ameambukizwa virusi vya ukimwi, alitamauka si haba na akaamua kwenda kwa marafiki zake na kuwaaga. Mwanzia, msaidizi katika kampuni ya akina Liwazo alipomwona Mayowe katika kampuni hiyo aliyaltinganisha maisha ya Mayowe na umande, aliona jinsi Mayowe alivyokuwa ameadhiriwa na virusi vya ukimwi. Mwanzia alimweleza Shuku (msaidizi mwenzake) kuwa, wakati Mayowe alikuwa na siha yake alikuwa akiwatetesha watu kama vile mhariri wa Kiswahili, Bwana Liwazo. Mwanzia alimwambia Shuku maneno yafuatayo: “Hakuna haja ya kuringa maishani. Maisha kumbe umande? Jua likija unatoweka.” (uk 156) Mwandishi alikuwa akiwaonya wanajamii kuwa wasiwe wenyewe pupa maishani kwa sababu, kama umande jua likichomoza lazima yatatoweka.

### **3.3.1 Ndoto**

Ndoto ni maono yanayotokea usingizini, pia huitwa ruya. Ndoto huwa na maana au ujumbe kwa mwanadamu. Katika kazi za Sanja kuna ndoto ambazo alizitumia ili kuweza kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake. Ndoto hizi zilieleza matatizo yaliyozikumba nchi za bara la Afrika, mwandishi alioanisha mbinu ya ndoto na mbinu ya jazanda ili kuifanya hadhira yake kuuelewa ujumbe aliotaka kuwasilisha kwao. Ndoto alizotumia ni ndoto ya Kijasiri kuyahu maisha ya mama M A na wanawe, ndoto ya Asisi akiwa gerezani wakigombana na Kifuja kuhusu uongozi mbaya wa Kifuja, ndoto ya Asisi kumhusu mama M A na wanawe, ndoto ya Asisi akiwa mbele ya mama M A akimwomba mawaidha kuhusu uongozi wa Mabonde na ndoto ya Zinguo akiwa gerezani kuhusu vita kati ya kundi lake na lile la Wanakusinyika. Tulichunguza ndoto hizi ili kuweza kuelewa ujumbe wa mwandishi.

#### **3.3.1.1 Ndoto katika Yasinya**

Mwandishi alitumia ndoto ya Kijasiri kumhusu mama M A na wanawe kueleza jinsi nchi za bara la Afrika zilikuwa zimekwama kimaendeleo kutokana na tamaa, ubinafsi na ukoloni mamboleo kutoka kwa viongozi wake. Kijasiri alikuwa ameketi chini ya mparachichi alipopata ndoto. Ndotoni alimwona mama M A na hali yake ilielezwa na msimulizi kama ifuatavyo:

M A alikuwa mtumwa wa mabara mengine, wanaume waliotaka  
ndoaa ya lazima. Fikira zake zilimtoroka na kutoweka tena.  
“Mwaka wa ngapi huu? Mwaka wa ngapi? Enhe? Sasa ni miaka

mingapi baada ya mwanangu wa kwanza kuzaliwa?”  
ziliendelea kudadisi. “Nusu ya karne na pengine zaidi.” Zilijibu.  
Nusu ya karne hiyo yote nimekaa ndani ya nyumba hii? Aliwaza.  
(uk 8)

Mwandishi aliyaliganisha maelezo kumhusu mama M A na hali ya nchi za bara la Afrika, yaani jinsi viongozi wa nchi za magharibi na viongozi wa nchi za Afrika, walivyokuwa waking’ang’ania uongozi wa nchi za Afrika. Utawala huu ulikuwa wa kikoloni kama ilivyoelezwa, waling’angania nchi hizi na kuzipora kilichokuweko bila kujali maisha ya vizazi vijavyo. Hivyo mwandishi alikuwa akizungumzia ukoloni mamboleo katika nchi za bara la Afrika.

Mwandishi alionyesha jinsi mambo yalivyokuwa kinyume na matarajio ya waanzilishi wa jamii huru za mataifa ya bara la Afrika. Mama M A alipomzaa mtoto wake wa kwanza (baada ya kupata uhuru,) basi kulikuwa na matumaini ya kupata jamii mpya, lakini watoto hawa ndio waliokuwa wakisabisha mateso ya mama M A. Mama huyu alikuwa ametamaushwa na hali ya watoto wake wenye pupa. Mama M A alikumbuka yafuatayo:

“Jamii ikaona kwamba, huyu mtoto anayezaliwa, huyu ambaye mamake alikuwa ameporwa na kuchafuliwa na wageni siku nyingi angezaa jamii mpya ili jamii hii iwe na kizazi kipy...” (uk 9) “... huyu mtoto alipokuwa anakua alisema alitaka nipate maisha bora, niwe mama wa kizazi kitukufu; Je, mbona wamenipiga ngumi na mateke kushoto kulia bila kujali hisia zangu au za wale wanaonihurumia siku zote? Aliona miaka ya ujana ikipotea bure. Aliona umri wake ukigeuka yabisi na kuuacha moyo wake na ukiwa.” (uk 10)

Mwandishi alionyesha jinsi bara la Afrika lilikuwa maskini hata baada ya miaka mingi ya kupata uhuru. Mama M A aliaibika kuona jinsi alivyokuwa akiomba na kukopa katika ukongwe wake. Mwandishi alikuwa akililinganisha jambo hili na hali ya nchi za Afrika ambazo hata baada ya kupata uhuru wao miaka zaidi ya hamsini iliyopita, bado walikuwa wakiomba misaada kutoka nchi za magharibi. Viongozi wa nchi za Afrika walikuwa wamesababisha umaskini huu kwa kufuja mali ya umma. Mwandishi alitueleza yafuatayo:

“Je, alizaa kwa nini? Kwa nini mtu awe na watoto wasiozaa?”  
Aliwaza. “Nilitoa nyonyo zangu hizi wanangu wakanyonya. Je

mimi sikuwapa maziwa ya kutosha?" aliwaza tena. Aliangalia mikono yake ambayo ilikuwa na mikunyanzi sasa. Ndio. Alikuwa amekomaa. Je, kuna yule angetarajia mama kama yeze awe bado anakopa? Awe anaombaomba bado, yeze M A Asiko." (uk 10)

Mwandishi alionyesha jinsi malengo ya viongozi wa mwanzo wa nchi za bara la Afrika yalivyokuwa mazuri, yalilenga kuwaimarisha Waafrika. Hali ya Waafrika punde tu baada ya uhuru ilikuwa ya kukatisha tamaa walikuwa maskini wasio na kisomo na hakukuwa na matibabu ya magonjwa. Lakini wakati huo waafrika walikuwa wakishirikiana katika kila jambo, jambo hili lilitoweka baada ya wao kupata 'uhuru' na kuanza kutawaliwa na viongozi Waafrika. Mama M A alikumbuka enzi hizo, alikumbuka maneno ya marehemu bintiye wa kwanza aliyezitakia nchi za Afrika ufanisi. Msimulizi alitueleza yafuatayo:

Alikuwa na falsafa nzuri. Alipigana daima kuitimizia jamaa yake malengo matatu makuu: kuondoa ujinga, kuondoa umaskini nyumbani na kupigana na maradhi. Haidhuru, mwito na "tuvute pamoja kama jamii tutaweza," ulimpa ari kubwa sana. Alipotaka karo ya mwanawe au binti, alipotaka kujenga ua wa nyumba, alipotaka kulima, alipotaka kujenga ghala au kufyeka nyasi walishikana mikono. Ilikuwa raha iliyoje? (uk 11)

Mwandishi alieleza jinsi viogozi Waafrika walivyokuwa na tabia ya ubiafsi na tamaa katika uongozi wao, waliuza mali ya umma kama chai na kahawa n.k. bila kusaza chochote. Hawakujali maslahi ya kizazi cha baadaye. Alishangaa jinsi tamaa ilivyoweza kuwa kali na ghali. Na huu ndio ugonjwa na sumu iliyokuwa ikiwaua wana wa M A. (uk 12)

Baada ya mkoloni kuondoka Waafrika walikuwa na matumaini ya kujitawala, lakini viongozi wa nchi za Afrika waliochukua usukani walidhihirisha ukatili kwa Waafrika wenzao zaidi ya wakoloni weupe. Waliuza raslimali za bara la Afrika bila kujali wala kubali, waliacha bara katika hali ya kutamausha. Pia waliwafanya waafrika wenzao watumwa kama mama M A anavyokuwa akiwaza kuhusu viongozi hawa:

Je, imani yetu tuliyoweka kwacho imegeuka mashuzi? Mbona nasikia vilio vya wanangu kama nyakati za Chebaskwony?  
...Kifuja kukaa kama babakambo na wanangu? Kama wana waliojitoa mhanga ili kulikaribisha rika lake kwa mama yao!  
Wakaaminika miili yao akakanyaga mithili ya malaika badala ya

mazulia. Wakambeba badala ya punda na nyumbu! Leo wenzake ni wageni wa mafunza. Huhisi vipi wakinyong'onyea?" (uk 14-15)

Mama M A pia aliwaza kuhusu hali ya umaskini katika nchi za bara la Afrika Iliyosababishwa na ubinafsi ya viongozi kama Mayowe, mali ya Mabonde iliishia mifukoni mwa wachache. Wananchi waliokuwa wengi ndio waliumia na hali yao kugeuka kuwa ya kutamausha. Mama M A aliwaza ifuatavyo:

Wanangu wakinipigania, wakienda bila chochote: Mararu milini, midomo iliyokatikatika, muguu ilijoja keya, macho yaliyoja matongo na vinywa vilivyokaukiana mate, kina Mayowe walikuwa wapi? Aliwaza tena kwa sauti. (uk 15)

Mwandishi alieleza jinsi viongozi wa nchi za Afrika walivyokuwa wamezungukwa na washauri waliowapotosha. Jamii iligawika katika makundi mawili ambayo ni: Tabaka la chini na tabaka la juu yaani, maskini na matajiri mtawalia. Waliokuwa maskini walizidi kuwa maskini zaidi na waliokuwa matajiri walizidi kuwa matajiri zaidi. Mwandishi alitueleza kuwa M A aling'amua yafuatayo: "Naam, yote yalianza kizazi cha akina Kifuja alipokubali kina Mayowe wawaongoze, wawaelekeze, wawashauri. Wakawashauri kuwa mpanda ngazi na mshuka ngazi hawapatani. Walipowashauri kuwa duniani kuna wana wakondevu na wana wanene wenye maumbo ya majitu wanaoghaniwa katika ngano za mazimwi, kina Kifuja wakasadiki." (uk 15) Ndoto hii ilieleza matatizo yaliyozikumba nchi za bara la Afrika. Badala ya viongozi Waafrika kutambua shida zilizowakumba Waafrika ili waweke mikakati, misingi bora na kulenga makuu ya kesho, waliendelea kujilimbikizia mali na kucheza ngoma ya walimwengu wenye hadaa. Ndoto hii ilisawiri hali halisi ya bara la Afrika na utendakazi wa viongozi wa nchi za Afrika amba walikuwa watepetevu, wenye tamaa na wasio wajali wananchi waliowachagua.

Asisi aliota ndoto akiwa gerezani, aliota akikabiliana na Kifuja. Alikuwa amefungwa jela kwa amri ya Kifuja kwa tuhuma za kumuua mhadhiri. Kifuja walimuua mhadhiri kwa ushirikiano na msichana Deni halafu wakamsingizia Asisi kosa la mauaji hayo. Mwandishi alitusimulia jinsi Asisi na Kifuja walivyogombana kuhusiana na uongozi mbaya wa Kifuja. Wawili hawa walikuwa wakiwakilisha vikundi viwili katika jamii: Asisi aliwakilisha kikundi kilichopigania mabadiliko katika jamii na ambacho kilikuwa maskini, naye Kifuja aliwakilisha viongozi fisadi waliojijali bila kuijali jamii iliyowachagua. Asisi alijipata akimwambia Kifuja yafuatayo:

Mimi Asisi natafuta sifa gani? Napigana na njaa, maradhi maji safi ya kunywa na kuangalia mawingu kama kuku amwogopaye tai, kuona kama kuna dalili ya wingu jeusi popote niweke mbegu kwenye ardhi. Je, si hayo yananitosha? (uk 65)

Kifuja naye alimjibu Asisi ifuatavyo: “Watu wadogo, kama vipanya tu. Kama si mimi Kifuja kuwapa konde hili tena kwa bei ya kutupa tu, Si mngekuwa bado maskwota?” kifuja aliuliza. (uk 65) Ugomvi huu uliingia katika kiwango kingine wakati Asisi alipandwa na mori alipokumbuka jinsi Kifuja aliwadhulumu wanajamii wakati Kifuja alikuwa akijihuisha na ukulima, ndipo kulizuka vita kati ya Kifuja na Asisi iliwalazimu akina mama kuingilia kati ili kurejesha hali ya utulivu kati ya watu hawa wawili. Msimalizi alitueleza yafuatayo:

Iliwachukua kina mama muda mrefu kurudisha hali ya utulivu na shughuli za upanzi zikaanza. Watoto na wakongwe ndio walikuwa na furaha sana. Rangi ya kijani lakini zaidi miche iliyoota mchangani na kuanza kutia vitawi ilitoa mvuto ambao hisia zao tu ndizo zingeweza kueleza. Asisi hakuelewa hisia hizo. (uk 65)

Ndoto hii ilibashiri jinsi mambo yangefanyika wakati wa kutafuta ukombozi katika jamii ya Mabonde. Kama Waswahili wasemavyo ‘Amani hajji ila kwa ncha ya upanga’. Ilimaanisha kuwa kizazi cha viongozi waliowakilishwa na akina Kifuja walifaa kukabiliwa vikali ili jamii ikombolewe. Baada ya haya kutokea basi shughuli za uwekezaji katika kila sekta zingeanza na kungekuwa na ujenzi wa jamii mpya yenye matumaini (rangi ya kijani ya majani ya mimea).

Asisi aliota ndoto kuhusu mama M A na wanawe baada ya kutoka jela, ndoto hii ilisawiri hali ya bara la Afrika kuwa jambo la dharura lilifaa kufanywa kuliokoa kutoka kwa mikono ya viongozi binafsi na fisadi. Viongozi hawa walikuwa wakifaidika na raslimali, madini na ardhi za bara la Afrika lakini, hawakutaka kulitunza bara la Afrika wala kukijali kizazi cha baadaye. Mwandishi pia alikuwa akionyesha jinsi nchi hizi zilikuwa zimebaki nyuma kimaendeleo kwa sababu ya mvutano mionganoni mwa nchi husika. Viongozi wa nchi hizi waling’ang’ania mali ya Afrika wakisahau kuwa walikuwa na jukumu la kuleta maendeleo kwa wananchi waliowachagua. Asisi alipata jinamizi lile na alimwona mama M A akinena na wanawe kama ifuatavyo:

Angalia nilivyonyong’onyea? Nyinyi hamwoni maradhi yaliyonisibu? Mnapigana tu. Nani ana uwezo wa kunyonya zaidi ya mwagine? Je, afya yangu ikienda na maangamizi haya?” M A

akawauliza wanawe tena. Watoto wale walikuwa kana kwamba hawakumsikiliza mama yao. Waliendelea kukabiliana tu. Mara Asisi alimwona M A akigaragara kwa maumivu makali. Alishawishika kwenda kumsaidia... (uk 76-77)

Kulikuwa na ndoto ya Asisi akiwa mbele ya mama M A. Asisi alikuwa kiwakilishi kizazi kipyga na jamii mpya ambayo ilikuwa tayari kupokea ushauri kutoka kwa wakubwa wake, wenye ushauri razini kwa viongozi wa kizazi kipyga. Naye mama M A alimshauri kuwa kiongozi aliyekamilika alikuwa yule aliyekuwa na uwezo wa kumtunza mke wake wa ndoa (nchi anayoiongoza) bila kumwoa mke mwengine. Pia kiongozi huyu huhakikisha kuwa ndoa za vijana katika nchi anayoitawala zimesimama ili kuilinda jamii ya kesho na mwisho aweze kuwaamini wapinzani wake ili washirikiane na wala sio kuvutana kama walivyofanya viongozi wa jamii ya Mabonde na nchi za Afrika. Asisi alizungumza na mama M A na akamuliza maswali kuhusu uongozi, mama M A alimjibu na akumpa mawaidha kutoka kwa kisa kuhusu kiongozi fulani aliyekuwa mhusika katika hadithi iliyokuwa ikisimuliwa katika kijiji cha akina mama M A. Asisi alijibiwa ifuatavyo:

“Vizuri. Vizuri kwani hutegemei nguvu za ujana wako na hekima ya dunia,” aliambiwa...

“Sikiza mwanangu, uhuru ni kujituma, ni kujinyima wengine wafaidi. Je, umewazia kuwapa wenzio kwanza mahali pa uchache?” (uk 86)

“Hadithi zinaendelea kusema kuwa huyu mfalme aliwalipia vijana mahari na kuwapa mali ya kuanzishia ndoa zao na maisha yao mapya. Hata angeweza kwenda likizo ya mwezi na kumwacha aliyekuwa mpinzani wake na mke wake mwenzi. Unaona? Siku ile utaacha mke wako bila kuhofia wapinzani wako kumnyakua, basi, utakuwa salama.” (uk 87)

### **3.3.1.2 Ndoto katika *Zinguo la Mzuka***

Mwandishi alitumia ndoto ya Zinguo akiwa gerezani kuashiria ukombozi wa jamii ya Kusinyika. Baada ya Wanakusinyika kuchoshwa na uongozi mbaya wa Zinguo na wenzake, waliwavamia katika madhabahu na kuwakamata. Walipelekwa kwenye kituo cha polisi na kufunguliwa mashitaka kwa kufuja mali ya umma. Ndoto ya Zinguo ilikuwa kama ifuatavyo:

Gerezani Zinguo anaota. Anaona umati. Umati wa watu unasukumana kuja mbele. Kisha kelele nyingi zaidi. Hatimaye

kunakuwa na mayowe. Zinguo anachanganyikiwa. Anawatazama walikuwa wenzake. Kaza anajiunga upande wa watu. Watu wachache wanaokuja upande wa Zinguo, wamesimama, hawatikisiki kutokana na mzubao. Vikundi hivi viwili: cha Wanakusinyika na cha Zinguo vinapigana na kikundi cha Zinguo kinashindwa kikundi cha umma kinashinda. (uk 91)

Ndoto hii ilibashiria kuanguka kwa viongozi dhalimu kama Zinguo na Kaza, ilibashiri pia jinsi viongozi hawa watakavyoaibishwa kwa madhila waliyoifanya umma. Mwandishi alikuwa akiitia jamii moyo kuwa kulikuwa na matumaini ya ukombozi na uhuru, baada ya viongozi fisadi kuondolewa kwa matendo yao. Mwandishi alikuwa akiieleza jamii kuwa wananchi ndio wenye jukumu la kuwfurusha viongozi fisadi na wala sio kuketi na kuangalia mambo yakiharibika.

### **3.4.1 Kinaya**

Kinaya hujengwa kwenye msingi wa kuwepo mgongano au ukinzani fulani kati ya hali halisi na matarajio ya wanaohusika. Sanja aliisawiri jamii ya nchi za bara la Afrika, yaani jinsi viongozi walikuwa wakitenda mambo yaliyokuwa kinyume na matarajio. Kulikuwa na mifano ya kinaya katika kazi nne tulizoteua kuzichanganua.

#### **3.4.1.1 Kinaya katika “Mimba Ingali Mimba”**

Mwandishi alitueleza jinsi Nekesa alivyokuwa amebeba mimba kwa miaka na mikaka, jambo la kubeba mimba kwa miaka mingi sio kawaida katika hali halisi. Kwa kawaida mimba hubebwa kwa miezi tisa. Tulielezwa juu ya kisa hiki kama ifuatavyo: “Miaka na mikaka imepita akitarajia. Akitarajia mtoto azaliwe, ampakate, ampe titi tamu la mama anyonye ...” (uk 101) Nekesa alicheleweshwa kuzaa kwa sababu ya mvutano kati yake na madaktari wa nchi za magharibi, walitaka mtoto huyu azaliwe kwao kwa sababu walikuwa na ujuzi, elimu na utaalamu wa kutosha kuliko wakunga wa nchi za Afrika. Mvutano huu ulionyesha jinsi nchi zilizoendelea zilivyokuwa zikizidunisha mbinu za kuzalisha mali katika nchi zinazoendelea. Mwandishi alikuwa akiieleza kuwa nchi zinazoendelea zilihitaji kuimarishwa kwa kupewa elimu ili kuondoa ujinga. Mwandishi alielesa kuwa kutokana na hali ya nchi zinazoendelea kubaki nyuma kielimu na kiteknolojia, ndipo nchi zilizoendelea zilipata nafasi ya kuwatawala na kuwanyanya Waafrika.

Vilevile ni kinaya kuwa mtoto aliyetarajiwa kuzaliwa alikuwa na wazazi wawili waliomzaa. Tulielezwa yafuatayo kuhusu mvutano wa mtoto huyu: “Alishindwa kuona uhalali wa kudai uzazi iwapo wakunga walidai kuwa wazazi wa mtoto wake. Mtoto mmoja, wazazi wawili?” (uk 106) Mvutano huu ulisababishwa na madaktari wa nchi za magharibi kutaka kupewa mtoto kwa sababu walimuelimisha Nekesa kuhusu uzazi, naye Nekesa aliamini kuwa kwa sababu aliibeba mimba alifaa kuwa mzazi wa mtoto huyu. Mwandishi alimtumia mtoto kuwakilisha raslimali na mazao yaliyopatikana katika nchi za Afrika, walitaka mazao lakini hawakutaka gharama ya kulea na kubeba mimba. Walimnyang’anya Nekesa mtoto (raslimali za nchi za Afrika) ilihali ilikuwa wazi mtoto alikuwa wa Nekesa. Kulingana na ujumbe wa mwandishi hali kama hii ndiyo ilizifanya nchi za Afrika kubaki nyuma kimendeleo kwa sababu ya kunyang’anywa utajiri wa nchi zao.

### **3.4.1.2 Kinaya katika “Mwavyaji wa Roho”**

Ilikuwa kinaya wakati meya wa eneo hili alitaka kumnyang’anya mkurugenzi mmoja tenda ya kuokota taka katika miji mitatu ya jamii iliyoangaziwa na mwandishi, alitaka tenda hiyo iwe mikononi mwake lakini nia yake haikuwa nzuri. Tulielezwa yafuatayo: “Tenda hiyo ilijikunyata na nafasi mia mbili za ajira ya vijana wa kike na kiume.” (uk 72) Kinaya ni kwamba kulikuwa na uwanja wa umma ambapo vijana walikuwa wakibarizi, walijilalia hoi kwa kukosa ajira. Meya kama kiongozi alifaa kuwa katika mstari wa kwanza kumuunga mkono mkurugenzi huyu, ili watoe nafasi hizo za kazi kwa vijana na wala sio kuanza kupanga vile angefaidika na tenda hiyo. Mgogoro wa tenda hii ulianza wakati mkurugenzi huyo alikataa kumpa meya kiinua mgongo ndiposa meya akaanza kumpinga.

Ilikuwa kinaya wakati Daktari Kitambi aliitumia hospitali yake kama mahali pa kufanya mapenzi na wasichana wadogo aidha kwa hiari, kwa ushawishi au kwa kulazimishwa. Katika hali halisi ni wajibu wa daktari kuwatibu watu wapate siha njema lakini sio kuwaharibia maisha kama alivyokuwa akifanya daktari huyu, kwa wasichana aliofaa kuwaita binti zake. Mwandishi alitueleza yafuatayo: “Aliwapima mwenyewe kuhakikisha hakujithiri. Kisha alifanya ya jogoo kuparamia kifaranga na kuwazawadi hela nyingi.” (uk 74) Daktari Kitambi hakumrudia msichana mara ya pili alipomtumia mara moja tu aliwatafuta wengine kwa msaada wa mpwa wake Jael.

Chumo alitumwa na Jael kwa Daktari Kitambi amjulishe kuwa alikuwa amekamatwa kwa ulangazi wa miadarati. Aliporudi kwenye kituo cha polisi, msimulizi alitueleza yafuatayo: "... nilimpata Jael ameketi katika afisi ya mkuu wa polisi anakula vibanzi kwa kuku wa kukaangwa. Mezani palikuwa na soda. Alicheka alipoona mshangao wangu." (uk 76) ni kawaida mtu akikamatwa kuwekwa korokoroni, lakini ni kinaya kwa mfungwa kulishwa kwa vinono kama Jael alivyolishwa.

Kitambi alitoa hotuba wakati wa kampeni za uchaguzi uliokuwa umekaribia. Alikuwa akiwaeleza wananchi sera zake, moja kati ya sera hizo alisema angekabiliana na madawa ya kulevyo. Alieleza kuwa viongozi/wapinzani wengine walikuwa wakifanya biashara ya ulangazi wa miadarati ilihali yeye ndiye aliyekuwa akitenda hayo kwa ushirikiano na mpwa wake Jael. Mwandishi aliiukuu hotuba yake ifuatavyo: "... Kitu cha kwanza nitakachofanya ni kuzuia ujambazi na vijana wetu kuharibika kwa kutumia miadarati. Nisaidie tuwaondoe hawa wafisadi ili tulete uongozi wa haki..." (uk 80). Kitambi alistahili kuwa mfano mwema kama kiongozi kwa kuwapa vijana kazi badala ya kuyaharibu maisha ya wanajamii kwa miadarati.

Ilikuwa kinaya kuona jinsi watu walivyokufa katika kampeni za Kitambi: Mtoto mdogo, vijana saba na wakongwe kadhaa pia nyumba zilibomolewa. Kitambi alitoa agizo lifuatalo baada ya maafa haya: "Afisi za NACADA zijengwe kama kumbukumbu yao hapo mavani." (uk 82). Mawazo yake yalifanana na ya mpwa wake Jael, baada ya kitambi kufaulu katika uchaguzi, Jael alifanywa kuwa mkurugenzi wa maswala ya vijana, aliwashtumu vijana kuwa walikuwa wazembe, wasiokuwa na mwelekeo na wapenda miadarati badala ya gange. (uk 83) Jael aliwashtumu ilihali wao na Kitambi ndio waliokuwa wakiwauzia miadarati. Hii ni taswira ya hali ya maisha katika nchi za Afrika yaani, viongozi wa Kiafrika huwadhuru wananchi na baadaye kuweka kumbukumbu za mambo maovu waliyotenda na yakaathiri jamii.

### **3.4.1.3 Kinaya katika *Zinguo la Mzuka***

Mada ya tamthilia hii ilikuwa kinaya kwa sababu badala ya Zinguo kumzingua Mzuka mambo yalikuwa yakitendeka kinyume. Yaani, Mzuka ndiye alikuwa akimzingua Zinguo na kuishia kuitawala nchi ya Kusinyika. Ilikuwa kinaya kuwa Wanakusinyika (kiwakilishi cha nchi

zinazoendelea) waliathirika katika nchi yao ‘huru’ ilihali waliokuwa wakifaidika na raslimali za nchi ni watu kutoka nchi zilizoendelea (Mzuka). Mwandishi alisema yafuatayo kuitia Mtu 2:

**Mtu 2:** ...Mlivikwa mavazi ya mzuka, mlijuaya madhabahu yalikuwa yamewekwa ili kuzingua Mzuka sio kumweka humu wala kumjengea mbuyu wa kukaa? Tukampa hifadhi, tukamneemesha kwa chakula cha wana wa Kusinyika! (uk 81)

Ilikuwa kinaya wakati mzuka alimweleza Zinguo kuwa nchi yake ni maskini na hakujua kutumia raslimali, lakini alikuwa akijua kuwa ni yeye aliyeziiba raslimali na kuwaacha Wanakusinyika katika hali ya umaskini. Pia aliwaambia hawakuwa wamejenga madhabahu thabiti (serikali) ilihali Mzuka na Mweupe ndio aliokuwa akiwapa mawaidha potovu kuhusu uongozi na hivyo kuifanya serikali ya Kusinyika kuanguka. Mzuka alisema yafuatayo:

**Mzuka:** ... (Akisema pembeni). Hujui kutumia raslimali yenu kujenga madhabahu thabiti! Nchi inanuka umaskini. (uk 16)

Jukumu la kiongozi ni kuwalinda wananchi na wala sio kuwa tishio kwa usalama wao. Ilikuwa kinaya kwamba Zinguo alimbaka mjakazi wake ati kwa sababu mke wa Zinguo hakuweko. Kama kiongozi Zinguo alifaa kumlinda msichana huyu na hata kuhakikisha alikuwa shulenii, lakini alimwajiri mtoto huyu jambo ambalo serikali nyingi huharamisha. Zinguo alimbaka msichana huyo kwa nia ya kujitakasa. Mwandishi alitaka kuonyesha jinsi Waafrika walivyolemazwa na tamaduni potovu. Utamaduni wa aina hii umepitwa na wakati na haukumstahiki kiongozi kama Zinguo. Mwandishi alitueleza yafuatayo: “Zinguo anamvuta Sichana ndani: wanavutana lakini anamshinda na kwenda naye. Kunakuwa na giza ghafla. Mlio wa chenene, bundi na mibweko ya mbwa inaskika. Kilio cha kutaka msaada kinasikika kwa mbali ndani. Kuna minung’ uniko katika hadhira. Baada ya muda anatoka ndani. Anaonyesha furaha mara huzuni.” (uk 28)

Viongozi wanafaa kuwa macho na wangalifu kuhusu mambo yanayotendeka katika nchi yao. Ilikuwa kinaya kwamba Zinguo alivuliwa nguo, akavishwa matambara na moto wake ukazimwa akiwa usingizini. Mwandishi alikuwa akionyesha jinsi viongozi wa nchi zinazoendelea walivyozembea kazini, hawakufanya walichostaahili kufanya. Mwandishi alitueleza yafuatayo:

Baada ya kipindi kifupi anasinzia na kulala. Anasikika kung'orota. Mzuka anakuja na kuketi naye pale alipolala. Anachukua kila kitu chake hata pamoja na kumvua na kumwacha na magwanda makuukuu. Hatimaye Mzuka anamwaga maji ndani ya moto kuuzima. Anaondoka haraka. Zinguo anazinduka. (uk 38)

Wananchi wa Kusinyika walikuwa wamechoshwa na uongozi wa Zinguo, kwa sababu alikuwa akijisifu tu kuwa ye ye ali kuwa kiongozi bora lakini hakuna maendeleo aliyokuwa akifanya. Alisema alimshinda Mzuka lakini ilikuwa wazi kuwa hakuweza kumshinda Mzuka kwa sababu hali ya Wanakusinyika ilikuwa ya kutamausha kutokana na unyonyaji wa Mzuka wa raslimali. Wanakusinyika walikuwa wamegeuka kuwa kama vifyefye au kaukau. Mwandishi alitueleza jinsi Zinguo alikuwa akijisifu:

**Zinguo:** (Anajitanua kifua.) Kama sio mimi Zinguo, Mzuka angekuwa amewafyonza nyote fy! Mna bahati mimi zinguo ni mkuu wenu! fyateni mikia na mfylate midomo! Nimelinda migodi, mbuga zenu na usalama ndio huu nawawekea. Je, kuna ye yote ameathirika? Tafuteni moto! (uk 40)

Kulikuwa na kinaya wakati Zinguo alivishwa na mzuka suti, kofia na fimbo, wananchi walinung'unika kwa sababu waliona jinsi kiongozi wao alikuwa akidanganyika. Baada ya Mzuka kupata alichotaka kutoka kwa nchi ya Kusinyika, alimvua Mzuka ile suti, kofia na fimbo aliyokuwa amempa tena kwa fujo. Zinguo hakuona akihadaiwa na Mzuka hata baada ya kutendewa haya mara kadha. Zinguo alisema yafuatayo yaliyodhihirisha ujinga wake:

**Zinguo:** Mnaomboleza nini?  
Hamwoni ninamkapa?  
Hamwoni kuhani wenu anapata umaarufu wa kidunia?  
Kutambuliwa na kuvalishwa gwanda hili si kidogo!  
Ni sifa kwenu na nchi yenu tukufu ya Kusinyika na madhabahu yake!  
Hii ni thamani ya vitu vinavyokuja, anavyoleta Zinguo.  
(Sauti za waombolezaji zinasikika kutoka nje bado.) (uk 46-47)

### **3.4.1.4 Kinaya katika Yasinya**

Ilikuwa kinaya kuona jinsi mama M A alivyokuwa amewazaa watoto na kuapa kuwa angewalinda kwa vyovyote ili wafaidi kutokana na raslimali za nchi zao. Walipozaliwa, yalikuwa matumaini yake kuwa kizazi hiki kingezaa jamii mpya. Mwandishi alituonyesha hali ya kutamauka ya mama M A alipoona jinsi watoto wake waligeuka kuwa kinyume na alivytarajia. Ajiuliza maswali yafuatayo: “Kwa nini mtu awe na watoto wasiozaa? Utasa unatoka wapi?” (uk 10)

Ilikuwa kinaya wakati Asisi alihudhuria sherehe za mkutano wa maombi ya umma. Wakati waheshimiwa walianza kupewa soda, Asisi alikuwa na njaa na alitamani apewe angalau soda moja. Alijua kuwa kwa sababu walikuwa mbele ya Mungu basi wote walikuwa sawa, lakini alikuwa akijidanganya kwani kulikuwa na ‘wakubwa’. Mwandishi alitueleza kilichomtendekea Asisi siku hiyo: “Alipojaribu kuwasogea wakubwa alikutana na radi. ‘Songa kule ama utiwe ndani!’” Alifoka askari wa mheshimiwa. “Sijaribu kukaribia waheshimiwa!” askari wa pili akafoka kwa ukali zaidi kwa lafudhi ya kikwao.” (uk 32)

Viongozi katika jamii yoyote ile wana jukumu la kuwalinda wananchi, ilikuwa kinaya kuona jinsi walivyokuwa katika mstari wa mbele kuyaharibu maisha ya wanajamii. Kifuja, chifu wa eneo la Mabonde alijhusika na ulanguzi wa mihadarati kuitia kwa mjukuu wake Huni. Maafisa wa polisi pia walishirikiana na Kitambi kuilinda bishara hiyo. Matokeo ya biashara hii yalikuwa kuzuka kwa jamii yenye vijana wasiochangia chochote katika ujenzi wa jamii, yaani kizazi cha baadaye kilikuwa taabani. Mwandishi alitueleza yafuatayo:

Huni alikwea ngazi na kuvuka daraja kutoka kwa mtumizi wa mihadarati hadi kwa mradi wenyewe na hatimaye ‘mdosi’. Babu ya mtu naye akadhamini biashara na hapo akapata za ‘kuwapa asali’, kidogo walambesi naye apate uwezo. Vilio vya akina mama na wanawake kuwa wana wao wadhikika kwa uraibu huo hazikupita wala kupata wa kusikiliza na kuzitekeleza. Kijasiri, Asisi na kundi lao waliwekwa seli ili juhudii hafifu kufanywa kufichua shughuli za Huni Pwani. Upinzani wa akina mama uliponoga Pwani, Huni alihama na kurudi nyumbani kwao. (uk 105)

### **3.5.1 Maswali ya Balagha**

Hii ni mbinu ambayo mwandishi hutumia maswali ambayo hayahitaji majibu. Maswali hayo hayahitaji majibu kwa sababu majibu yake yako wazi kwa msikilizaji au msomaji. Huwa ni mbinu nzuri ya kumfikirisha msomaji, kumshawishi kuhusu jambo au hali fulani na pia kusisitiza usemi. Kuna matumizi mengi ya maswali ya balagha kama tulivyochangana.

#### **3.5.1.1 Maswali ya Balagha katika “Mimba Ingali Mimba”**

Nekesa alingoja kwa miaka na mikaka mtoto wake azaliwe, aliwaamini madaktari wa ughaibuni waliokuwa wakimpa moyo kuwa mtoto wake angezaliwa. Kwa sababu hii, Nekesa alitamauka kwa sababu baada ya muda huu wote mtoto hakuzaliwa hivyo alijiuliza maswali mengi. Maswali haya yalionyesha jinsi Waafrika walivyokuwa wakizitegemea nchi za magharibi kwa kukosa kujiamini. Maswali haya pia yalidhihirisha mbinu ya uzungumzinaksi. Mwandishi alitueleza kuwa Nekesa alijipa moyo kwa kujiambia maneno yafuatayo: “Labda leo atazaliwa. Si walisema atazaliwa, na ni wangu?” (uk 101)

Mbinu za maswali ya balagha na uzungumzinaksi katika akili ya Nekesa zilionyesha furaha waliyokuwa nayo Waafrika walipojua kuwa kulikuwa na madini, raslimali, mbuga za wanyama na vingine (mimba) ambavyo vingewanufaisha na kuwaendeleza. Mwandishi aliangazia swala la kutojiamini, Nekesa alijiuliza maswali kuonyesha kuwa hakuamini kuwa ni kweli angeweza kuzaa. Mwandishi alitueleza yafutayo: “Wakati mwingine na kwa dakika nyingi, angebung’aa na kuuliza iwapo hata yeye angeweza kuitwa mzazi? (uk 102). “Hata Nekesa? Hili tumbo linaweza kubeba? Siamini,” (uk 103) hali ya kutojiamini ya Nekesa ilikuwa sawa na hali ya Waafrika wanaoamini kuwa ili wafaulu katika shughuli fulani basi lazima wawalushe Wanamagharibi. Hii ndio sababu inayozifanya nchi zinazoendelea kubaki nyuma kimaendeleo.

Maswali ya Nekesa yalikuwa hayana mwisho, maswali yake yalidhihirisha kuwa bado Afrika haikuwa imepata uhuru wa kufanya uamuzi wowote. Kwa sababu, kama mtoto alikuwa wa Nekesa kwa nini aliulizwa maswali ambayo hangeweza hata kuyajibu. Mama humiliki mtoto aliyezaa lakini hali ya Nekesa ilikuwa tofauti kwa sababu, madaktari walidai kumiliki mtoto. Nekesa alizinduliwa na daktari na kuambiwa mtoto atakayemzaa angekuwa wake. Walitoa wasifu wa mtoto waliyetaka azaliwe: “Wa kike, Mzungu ama Muhindi. Walimuuliza kama

alitaka kumzaa mweusi au mweupe? Walimuuliza pia alitakaaabudu dini gani?” Maswali haya yalisua tashwishwi kama kweli mtoto huyu angezaliwa na kama angezaliwa angekuwa wa Nekesa kweli? Nekesa alijiuliza maswali yafuatayo kwa sababu ya maswali aliyoulizwa: “... Mtoto wa Nekesa, ni wake kweli? Kama kuzaa ni kwake, kwa nini aulizwe rangi? Kwa nini aulizwe dini? Kwa nini aulizwe jinsia?” (uk 103)

Kulikuwa maswali ambayo Nekesa alijiuliza na yalionyesha kuchanganyikiwa kwake. Hii ilikuwa taswira ya nchi za Afrika, jinsi zilivyokuwa zimebabaishwa na nchi za magharibi (shinikizo kutoka kwa madaktari) amba walikuwa wawakilishi wa nchi za magharibi. Maswali haya yalikuwa kama yafuatayo: “Hata kujifungua mtoto wako, ilihitaji mikutano?” (uk 104) “Huyu mtoto, si wangu tena? Kwa nini nilee mimba hapa, halafu aende kuzaliwa nje? Mama zetu hawakufanya hivyo. Kuhisi uchungu kulimpa mama fahari. Mbona mimi nisisikie alivyosikia mama aliyenizaa?” (uk 105) Mtoto mmoja wazazi wawili. (uk 106) Hali hii ilidhihirisha kuwa nchi za Kiafrika hazijapata uhuru kamwe hata kama walidai kuwa ‘huru,’ bado walikuwa wakitawaliwa na wakoloni. Wakoloni walikuwa wakidikteti jinsi ya kuendeleza shughuli katika nchi za bara la Afrika.

Kulikuwa na maswali ambayo Mwandishi aliyatumia kuuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake ambayo yalidhihirisha hali ya kutamauka kwa Waafrika. Hakuna matumaini ya kujitawala, kuzalisha mali na kuwa huru. maswali yenyewe yalikuwa kama yafuatavyo: “Nekesa! Atapata uchungu wa kuumwa kizazi lini?” Wimbo nao umenata mdomoni:

*Akiumwa huhisije?  
Akija husukumaje?  
Akikwama iweje ?  
Sipozaa takuwaje?  
Nangoja. (uk 107)*

Waafrika walisawiriwa na mwandishi kama waliokuwa katika hali ya taharuki. Walikuwa wamebaki nyuma kimaendeleo, wamenyang’anywa raslimali zao, hawajapata viongozi wa kubadilisha hali yao na ndio maana walionekana kutamauka kama Nekesa.

### **3.5.1.2 Maswali ya Balagha katika “Mwavyaji wa Roho”**

Chumo aliyejekuwa msimulizi wa hadithi alikuwa akitafakari jinsi rais mstaafu wa nchi fulani kule ughaibuni alivyofikishwa mahakamani kwa kufuja mali ya umma. Aliwaza kama ingewezekana kuwashtaki viongozi wa nchi za Afrika kwani ni kana kwamba kila kitendo walichokifanya kilihusishwa na ufisadi. Msimulizi alijiuliza maswali yafuatayo: “Kama watemi wetu wangekuwa huko ng’ambo basi wasinge funguliwa mashtaka. Uwashtaki kwa mangapi uwache mangapi?” (uk 72) Alitamatisha kwa kusema kuwa wangehukumiwa tu jambo moja ‘kinyongo’. Viongozi wa nchi zinazoendelea wamejihuisha na vitendo vingi vyta ufisadi na hivyo hawajakuwa mfano mwema kwa jamii na kizazi kijacho.

Tulielezwa jinsi meya wa mji wa jamii iliyoangaziwa na mwandishi, alivyoandika barua ndefu ya kumnyang’anya tenda mkurugenzi mmoja aliyejekuwa akifanya kazi ya kuzoa taka katika miji mitatu mikuu. Alitaka kumnyang’anya tenda hiyo kwa sababu mkurugenzi hakuwa ametoa kitu, katika nchi ya kitu kidogo. Msimulizi aliuliza maswali yafuatayo: “... sababu, hakumlambisha mkono wangu mtupu katika nchi gani?” (uk 72) Mwandishi alikuwa akiieleza tabia ya ufisadi wa viongozi Waafrika.

Mwandishi alitumia maswali ya balagha kuonyesha jinsi pesa zinavyoweza kumfanya mtu kuheshimika. Kitambi alikuwa akiwalambisha maafisa wa usalama ‘asali’ ili waruhusu biashara yake ya ulangazi wa mihadarati kuendelea na kwa hivyo walikuwa wakimwita ‘mzee’. Afisa wa polisi ndiye alimuuliza Jael maswali yafuatayo: “Mbona hukuniambia wewe ni mpwa wa mzee? Wajua hawa vijana wangu wametoka mafunzioni tu juzi na hawajui kazi yao! Nani hamjui mzee?” (uk 76)

Mwandishi alitumia maswali ya balagha kuonyesha jinsi vijana walivyokuwa wametumia miadarati na kuathirika vibaya. Miogoni mwao mlikuwa vijana wa viwango tofauti tofauti vyta elimu ambao walikuwa waraibu wa madawa ya kulevyia. Msimulizi alieleza yafuatayo kuhusu hali yao: “... Sura za wale vijana kwenye runinga zilinijia kwa kishindo, vifyefye vyta watu. Wasichana kwa wavulana, wengine wanaporomosha Kizungu kama nini?” (uk 79) Vijana hawa walikuwa wakihojiwa kwenye runinga na katika mazungumzo yao walisema kuwa hawangeweza kuishi bila kutumia madawa hayo. Maswali haya yalionyesha kuwa swala la

mihadarati lilikuwa janga la kitaifa kwa sababu liliwaadhirri hata waliokuwa na elimu ya juu yaani, kutoka vyuo vikuu, shule za upili na wale wa shule za msingi.

Kulikuwa na maswali yaliyoulizwa na Kitambi katika hotuba yake ya kisiasa, maswali haya yalidhihirisha kinaya. Kitambi alikuwa akijinasibisha na umma kwa kusema kuwa wote walitaka vijana waliokuwa na maadili mema, lakini, yeze ndiye alikuwa akiwauzia vijana mihadarati. Mwandishi alisisitiza kuwa ni viongozi wawa hawa waliodai kuijali jamii ambao walikuwa wakiiharibu. Mwandishi alitueleza kuwa Kitambi alijitetea ifuatavyo: "...Nisaidie tuwaondoe hawa wafisadi ili tulete uongozi wa haki. Je, nani ambaye hataki jamii na vijana wenye maadili? ..." (uk 80) "Je, kuna mayatima wangapi kutokana na viini na kutokana na utumizi wa madawa? Nyumba ngapi zimevunjika sasa?" (uk 81) Daktari kitambi alizungumza kana kwamba alikuwa msafi lakini, alijua kuwa ni yeze aliyeyasababisha aliyooyataja.

### **3.5.1.3 Maswali ya Balagha katika *Zinguo la Mzuka***

Maswali ya balagha yalitumika kusisitiza ujumbe wa mwandishi kuwa bado nchi za Afrika hazijapata uhuru. Viongozi waliochaguliwa walikuwa wakipewa ushauri na viongozi wa nchi za ughaibuni. Kwa kifupi viongozi wa nchi za magharibi walikuwa wakizitawala nchi zinazoendelea, kupitia ushauri waliokuwa wakiwapa viongozi wa Kiafrika. Waliyahadaa ili wanyakue mali yao. Walijitajirisha na kuziacha nchi zinazoendelea zikiwa zimefilisika. Waafrika wanaonekana kama ambao hawangeweza kujiongoza bila ushauru wa viongozi wa nchi zilizoendelea. Maswali haya ni kama yafuatayo:

**Mweupe:** ... kama sio mimi, yule ndugu yako angekuwa wapi? Si hapo ulipo?

**Mweusi:** ... wewe mbona huketi kwako na kuangalia yako?

**Mweupe:** Nani alikutoa matongo machoni?

Nani alikuvalisha nguo akakuwekea sherehe ya tambiko?

Nani aliyapanga haya madhabahu?...

Mtu mweusi anajua maana ya uhuru? Anajua uongozi? (uk 6)

Mwandishi pia alieleza kuwa, Waafrika walikuwa amebaki nyuma kwa sababu ya kukosa ujuzi wa kiteknolojia hivyo walikuwa wakizitegemea nchi zilizoendelea kiteknolojia. Ndio maana Mweupe alimbeza Mzuka kwa swali lililokuwa linadhihirisha kejeli: "*What do you know about technology?*" (uk 7) Hali hii ya kuzitegemea nchi zilizoendelea imezilemaza nchi zinazoendelea.

Vile vile mwandishi aliangazia swala la ukabila na ubaguzi katika uongozi au hata nchi nzima ya Kusinyika. Madhabahu hapa yalitumiwa kijazanda kumaanisha uongozi. Mazungumzo haya yaliyosheheni maswali ya balagha yalikuwa kati ya Mtoto 1 na Mtoto 2. Mazungumzo yaliendelezwa ifuatavyo:

**Mtoto 1:** Wewe pia umepagawa mzuka? Usiwe mbinafsi.

Hujui sisi kabilo letu ni gani? Dogo Dua! ...

**Mtoto 2:** ... lakini imani yetu njema Wasia. Mbona hivi?

Mbona madhabahu ni ya wachache? (uk 9)

Mwandishi alioanisha maswali ya balagha na kinaya alipomsawiri Zinguo akijishaua jinsi angemshinda Mzuka ilihali ilikuwa wazi kuwa alikuwa ameshindwa kumfukuzia mbali (Mweupe). Zinguo aliuliza ifuatavyo: “Nilimshinda baba yake, yeye ni nani?” (uk 11)

Zinguo aliuliza hadhira swalii: “... na nyinyi mbona hamkulipiga hili dude?” (uk 14) Hii ilikuwa ishara kuwa alikuwa ameshindwa kukabiliana na Mzuka. Sauti kutoka kwa hadhira ilimjibu na kumweleza kuwa yeye alipewa wadhifa wa kuwa Zinguo na akapewa madhabahu ili aweze kuwa na mamlaka ya kumfukuza Mzuka kwa tambiko (mamlaka ya uongozi). Sauti kutoka kwa hadhira ilimjibu: “Hapo si ukumbini hapo? ... wewe ulipo unapajua? ... Tazama uone hayo ni maji ya nini?” (uk 14)

Kupitia wimbo wa Sichana lililokuwa likifanya kazi kwa Zinguo, mwandishi aliangazia matatizo yaliyowakumba watoto alitaja ajira za watoto, mishahara duni na kunyimwa nafasi ya kwenda shuleni. Sichana liliimba kifungu kama ifuatavyo:

*Lakini?*

*Huduma nalipwa?*

*Maslahi napata?*

*Nitasoma na nini?* (uk 26)

Zinguo alijaribu kuihadaa hadhira kuwa alikuwa akiipigania na wala hakuwa akipora mali yake, bali alikuwa akichukua tu. Hadhira ilimkaripia ishara kuwa ilikuwa imezinduka na haikuwa ikidanganyiki kama alivyokuwa akiidanganya hapo awali. Ilimuuliza yafuatayo: “...unajipigania! unapigania lipi? Unalala na mizuka usiku, unakula, unakunywa?” (uk 39)

Kufikia mwisho wa mchezo Wanakusinyika walionekana kuzinduka, hivyo Mtu 1 aliuliza maswali kwa hadhira, maswali hayo yalikuwa kama ifuatavyo: “Je, hatuwezi kuyajenga?” (uk 77) Maswali haya yaliwazindua watu waanze kuyajenga madhabahu upya, baada ya madhabahu ya hapo awali kuharibiwa (viongozi dhalimu kuondolewa). Wanakusinyika walizinduka na kuwaondoa viongozi fisadi kama Zinguo, Kaza na Mzuka, waliwafungulia mashtaka kwa kupora mali ya umma. Mtu 1 aliwahimiza kuwa walikuwa na uwezo wa kuyajenga madhabahu tena. Hivyo kwa msomaji, kama mmoja wa wanajamii alikuwa akihimizwa kuwa anaweza kuleta mabadiliko na mwamko mpya kwa kuwafurusha viongozi fisadi na kuwachagua walio na maadili mema.

### **3.5.1.4 Maswali ya Balagha katika Yasinya**

Mama M A aliwaza na kujiuliza maswali kuhusu maendeleo na hatima ya wana wa Afrika. Aligundua kuwa hakukuwa na maendeleo wala uzalishaji ulioendelea katika nchi za Afrika. Utasa huu ulisababishwa na viongozi fisadi ambao walikuwa wakiweka kila shilingi kwa akaunti zao na zingine wakatumia kwa mahitaji yao. Mama M A alijiuliza maswali yafuatayo: “Kwa nini mtu awe na watoto wasiozaa? Utasa unatoka wapi?” (uk 10)

Viongozi dhalimu walisababisha madhila na mahangaiko kwa wananchi, jambo hili lilikuwa tofauti na maono ya wazazi (waanzilishi) wa mabonde. Mwandishi aliwalinganisha viongozi hawa na kiongozi Chebaskwony, ambaye alikuwa dhalimu, mwenye tamaa ya pesa na mali pia alikuwa mbin afsi wa kupigiwa mfano. Mwandishi alitueleza mama M A alijiuliza maswali yafuatayo: “Je, imani yetu tuliyoweka kwacho (kizazi) imegeuka mashuzi? Mbona nasikia vilio vya wanangu kama nyakati za Chebaskwony.” (uk 14)

Mwandishi aliifikirisha hadhira yake kuhusu wamiliki wa vibanda ambao walikuwa wakiwalipa wafanyakazi wao mishahara duni ilihali uchumi alikuwa ukipanda kila uchao. Huu ulikuwa unyanyasaji na ukatili wa hali ya juu. Maswali haya yaliulizwa na Asisi, katika uzungumzinafs alipokuwa akielekea kwa Kipokeo. Maswali yalikuwa kama yafuatayo: “Mshahara gani? Shilingi mia tisa kwa juma, nitakula au nitalipa kodi ya nyumba? ...” (uk 19)

Kipokeo alijiuliza maswali kuhusu vitendo vya ujisadi ambavyo vilikuwa sehemu ya maisha ya viongozi wa Mabonde, mwandishi alitaka kusisitiza sababu ya uchumi kuharibika. Kipokeo alikuwa akiwaza kama ifuatavyo:

... kila mtu tani yake ubaya uko wapi? Nani hajui hakuna ajira?  
Nani hajui? Viwanda vikifungwa, ni Kipokeo amefunga? Kipokeo analima pamba? Kipokeo ndiye amekataa kuwalipa wakulima wa pamba ama wale wa tumbaku? Kipokeo ndiye ameharibu barabara viwandani ili gharama ya uzalishaji iende juu? (uk 21)

Mwandishi alimfananisha Kipokeo na viongozi hawa dhalimu ili kuelezea matendo ya viongozi hawa ya kutowajibika, ubinafsi na ujisadi yaliyokuwa yakiwaumiza wananchi.

Kipokeo alikuwa akifanya kazi ya ukahaba na kwa sababu alikuwa amejitolea kuifanya kazi hiyo, hakumbagua mwanamume yeoyote. Hakujali kuambukizwa virusi vya ukimwi, janga ambalo lilikuwa limelikumba taifa nzima. Kipokeo alijiuliza maswali haya katika mawazo yake hivyo kulikuwa na mbinu ya uzungumzinafsi. Msimulizi alitueleza kuwa Kipokeo aliwaza ifuatavyo: “Shilingi hainuki. Hata ikitoka kwa maiti nitaichukua. Niache kwani nina wazimu? Kwani, kazi yangu itakuwa gani tena?” (uk 21)

Emali (mamake Asisi) alikuwa akizungumza na wateja wake wa mboga. Mwandishi alikuwa akituonyesha hali ya umaskini ya wakazi wa Mabonde kwani hawakuwa na pesa za kununua hata mboga, tulielezwa kuwa mama huyu alielewa hali ya Wanamabonde, hakukosa kuwakopesha kwa sababu hawakuwa na kwingine kwa kukimbilia. Mwandishi alikuwa akiieleza jamii kuwa ni vyema kuwa na utu. Mwandishi alitueleza walipokopa mboga Emali aliuliza maswali yafuatayo: “Nitawakatalia haya matawi nanyi mtaenda wapi?” (uk 35)

Vile vile kulikuwa na maswali ya balagha kuhusu ujisadi wa Kifuja na njia ambazo alitumia kuifisadi nchi ya Mabonde. Baada ya Kipokeo kukataa kuchukua nafasi ya uwenyekiti katika kamati ya kuimarisha maeneo iliyoundwa na Kifuja. Kifuja alijenga majosho na miradi ya maji kwa wakwe zake, kwa dada yake na kwa marafiki zake. Njia zizo hizo ndizo zilizotumiwa na viongozi wengine kama Chebaskwony kuifilii jamii. Mwandishi alikuwa akiizindua jamii iwe makini kwa vitendo vya viongozi fisadi kama hawa. Kipokeo aliwaza ifuatavyo: “... Mbona

kama mradi unahu su jamii nzima iwe siri kwa wanajamii wengi?” (uk 44) “Tena mbona wanaotoa mawazo yao kuonwa kama maadui?” (uk 45)

Mwandishi aliuangazia ushujaa wa Asisi. Maswali haya yaliulizwa na Liwazo alipoenda kumwangalia Asisi gerezani. Alishushwa na ukakamavu wa Asisi kwani hakuwa na lawama yoyote, lakini alikuwa ametiwa ndani na hakuonekana kuwa na kinyongo na waliomtia ndani. Ujumbe wa mwandishi ni kuwa ni vyema kwa wanajamii kusamehe ili kudumisha amani katika jamii. Asisi alidhihirisha hali ya ukomavu hadi Liwazo akajiuliza maswali yafuatayo: “Mtu anaumia bila hatia huku anawajali wanaomkandamiza?” (uk 69)

Mama M A aliwaza kuhusu wanawe halafu akawauliza maswali yafuatayo: “Angalia nilivyong’onyea? Nyinyi hamwoni maradhi yaliyonisibu? Mnapigana tu. Nani ana uwezo wa kunyonya zaidi ya mwingine? Je, afya yangu ikienda na maangamizi haya?” (uk 76-77) Mwandishi alikuwa akiilinganisha hali ya mama M A na ile ya nchi za bara la Afrika yaani, zili kuwa zikifarakana na kung’ang’ania raslimali, madini na mipaka ya ardhi za Afrika huku zikipoteza muda mwigi ambao ungetumika katika maendeleo.

Kama hali ilivyo katika nchi nyingi za Kiafrika timu za mpira zimekuwa zikisambaratika kwa kukosa uongozi bora na wasimamizi wa timu hizi kufuja pesa za timu. Mhusika Asisi alikuwa akiwaza kuhusu timu ya Mabonde ambayo ilikuwa imeshindwa kusafiri kwenda kupimana nguvu na timu nyingine kwa sababu haikuwa na pesa. Mwandishi alitueleza Asisi aliwaza na kujiuliza maswali yafuatayo: “Si shirika la ulimwengu duniani huleta pesa za ufadhili? Hata za kustawisha kandanda ya vijana hakuna?” (uk 77)

Kulikuwa na maswali ya balagha yaliyoulizwa na Asisi kuhusu kifo cha babake (Mahiri.) Tulielezwa jinsi kisa cha kifo chake kilifichwa na hakukuwa uchunguzi uliofanywa. Maswali haya yalionyesha kuwa mtu wa kiwango cha chini cha kifedha hakuhitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina hasa kama kifo chake kilikuwa kikihusiana na viongozi fisadi. Mahiri aliuawa na kina Kifuja kwa sababu alijitokeza kumtetea mtoto wa Chemos, mtoto huyu alikuwa ameshtakiwa na kina Kifuja. Kwa sababu ya kuwapinga kina Kifuja na wenzake, Mahiri aliuawa. Asisi alijiuliza maswali yafuatayo: “Hapakuwa na uchunguzi. Tena wa nini?” (uk 85)

Kijasiri alijiuliza maswali kuhusu madhila yaliyokuwa yakiwakumba kina mama hasa wajane kwa sababu ya kutotoa kitu kidogo mahakamani. Hii ndiyo ilikuwa hali ya mahakama za Mabonde, ili kesi kuamuliwa, ilimlazimu mtu kutoa kitu kidogo. Kijasiri alijiuliza maswali haya hivyo kulikuwa na mbinu ya uzungumzinafsi. Hapa ilikuwa baada ya kukutana na Afisa Angusha alipokuwa ameenda kudai malipo ya mumewe Halili, aliye kuwa amekufa akiwa kazini katika kampuni ya Maba iliyomilikiwa na Kifuja, Mayowe, Afisa Angusha na Dkt. Balaa. Afisa Angusha alimtaka Kijasiri awe mpenzi wake wa siri ili aweze kuishugulikia kesi yake na alipwe fidia kwa haraka. Kijasiri alikataa na akumkemea afisa Angusha hadi akatoroka. Tulielezwa kuwa Kijasiri alijiuliza maswali yafuatayo: “Je, ni wajane wangapi wanapitia machungu hayo? Kesi za wangapi hazisuluhishiki maana ‘wangu mtupu haulambwi?’” (uk 98)

Huni alikuwa mhuni hivi kwamba haingekuwa rahisi kwa askari kumkamata kwa sababu alifadhiliwa na babu yake chifu Kifuja kwa ushirikiano na afisa Angusha wa Mabonde. Asisi alijiuliza maswali yafuatayo: “Nani angeweza kumshika huyo nyoka?” (uk 106) Biashara ya Huni ilikuwa ya ulanguzi wa miadarati, iliyoathiri na kuharibu maisha ya vijana na jamii kwa jumla. Waliohusika na usalama wa umma walikuwa washika dau katika biashara hii, hivyo ilikuwa vugumu kupigana na biashara ya miadarati na athari zake huko Mabonde. Maafisa wa polisi walitepetea kazini kama vile Afisa Angusha, alikuwa mmoja wa wamiliki wa kampuni ya Maba iliyotumiwa kuuza madawa ya kulevyia huku wakidai kuwa walikuwa wakichapisha vitabu hapo. Mwandishi alikuwa akiieleza jamii kuwa viongozi wengi hujishughulisha na biashara zinazoiathiri jamii badala ya kuijenga jamii.

Mayowe alienda kumuaga kwaheri rafiki yake aliye kuwa meneja katika kampuni ya kina Liwazo, Mayowe alikuwa ameenda kumuaga kwani alikuwa ameambukizwa virusi vyatukio. Meneja naye alipoiona hali ya rafiki yake, aliwaza kuhusu mke wa Mayowe na kuhofia asiwe ameambukizwa virusi. Mwandishi alikuwa akitueleza jinsi wanaume katili wanavyozinyima familia zao raha na mwishowe wanakufa na kuziachia familia zao shida, wao pia huwaambukiza wake zao magonjwa. Meneja aliwaza ifuatavyo: “Ni wa kuambukizana? Alimwambukiza nani? Mkewe anajua?” (uk 155)

Wakati Kijasiri alikuwa gerezani na hakukuwa na matumaini ya Asisi na wenzake kumtoa gerezani, Asisi aliwaza kuhusu ukarimu wa Kijasiri. Asisi aliwaza ifuatavyo: “Uliwafadhili wangapi wakati wewe na Tumaini mlikuwa hamna? Wangapi walikuja mikono mitupu wakaenda imefurika? Wakafumba na kufumbata ukarimu wako, mkawaondolea makunyanzi yaliyowazeesha hata vijana wadogo?” (uk 162-163) Mwandishi alitumia maswali ya balagha kuifanya jamii kuwajali wasiojiweza mionganoni mwao.

### **3.6 Hitimisho**

Majazi ni mbinu ambayo Sanja alitumia katika baadhi ya vitabi vyake. Tuligundua kuwa Sanja alitumia majazi bayana isipokuwa katika jina Chebaskwony ambapo maana yake ilikuwa fiche kwa msomaji. Maana ya jina hilo ilieleweka tu baada ya mwandishi kutoa ufanuzi wa jina hilo. Majina ya watu, nchi, miji, maduka na hata hoteli yalisheheni maana kochokocho kama tulivyochanganua. Mwandishi aliweza kuwasilisha maswala mazito mazito kupitia mbinu hii bila kutumia maneno makali au maneno mengi. Hata hivyo katika hadithi fupi ya “Mimba Ingali Mimba” (2006) mbinu hii haikutumika, mwandishi alimtumia mhusika mmoja tu kwa jina Nekesa.

Mwandishi alitumia mbinu ya jazanda katika kazi zake kwa mapana. Kazi zake zote zilikuwa na sifa ya kijazanda aliyoitumia kuwasawiri viongozi wa Kiafrika amba walikuwa wakizilemaza nchi hizi kwa vitendo vyao vya ufisadi na wengine ubinafsi. Kuna viongozi waliowategemea viongozi wa nchi za Magharibi bila kujua kuwa hata Wanamagharibi walitaka kuzifilisi nchi hizi za Kiafrika kwa manufaa yao binafsi.

Mbinu ya ndoto ilitumiwa ili kufafanua matatizo yaliyozikumba nchi za Kiafrika. Mambo aliyyoyazungumzia Sanja yaliuelezea muonoulimwengu wake na pia jinsi jamii aliyokulia ilivyoyachukulia mambo. Sanja aliisawiri jamii iliyokuwa imebaki nyuma kimaendeleo na kiteknolojia hivi kwamba wananchi walikuwa waking’ang’ana na shida kama magonjwa, elimu, ujinga na maji safi.

Mbinu ya kinaya ilitumiwa na mwandishi kwa mapana katika kazi hizi nne teule kueleza jinsi mwandishi aliisawiri jamii ya nchi za bara la Afrika. Viongozi walitenda mambo kinyume na

kawaida hivi kwamba ilikuwa rahisi kwa mtu kudai kuwa hiyo ndiyo ilikuwa kawaida ya mambo. Mbinu hii ilimwezesha mwandishi kuwasilisha hisia zake za kusinyika kutokana na vitendo vya viongozi hawa. Alipendekeza kuwa viongozi wa aina hii hawastahili kuwa mamlakani kwa kuwaonyesha Waafrika kuwa wana jukumu la kuwafurusha viongozi hawa na kuwachagua viongozi waliowajibika.

Kupitia kwa maswali ya balagha mwandishi aliweza kuwasilisha ujumbe mzito kwa hadhira yake. Pia aliweza kuifikirisha jamii kama njia moja ya kuizindua jamii kuwafurusha viongozi fisadi ili wawachague viongozi waliowajibika. Kwa ujumla mwandishi aliboresha kazi yake kupitia kwa ufundi alioudhihirisha katika matumizi ya mtindo aliouteua. Istilahi na tamathali alizozitumia ziliimarisha ujumbe wake na kupatia kazi zake mvuto wa kipekee.

## SURA YA NNE

### **MTINDO WA SANJA KATIKA YASINYA, ZINGUO LA MZUKA, “MIMBA INGALI MIMBA” NA “MWAVYAJI WA ROHO”**

#### **4.1 Utangulizi**

Katika utafiti wetu tulichunguza dhana ya mtindo hasa kipengele cha tamathli za usemi katika kazi nne teule za Sanja: “Mimba Ingali Mimba” (2006) na “Mwavyaji wa Roho” (2011) (hadithi fupi) *Zinguo la Mzuka* (2011) (tamthilia) na *Yasinya* (2014) (riwaya). Tulijikita katika nadharia ya Umitindo iliyotuwezesha kuichanganua kazi yetu kitaalamu. Tulichunguza tamathali za usemi tano ambazo ni: Majazi, jazanda, ndoto, kinaya na maswali ya balagha na tuligundua kuwa mwandishi alizioanisha mbinu hizi na ujumbe aliotaka kuuwasilisha kwa hadhira yake kwa njia mwafaka. Tamathali za usemi tulizoziteua zilituwezesha kuishughulikia mada yetu kikamilifu.

Katika sehemu hii tulidhibitisha kuwa mtindo ni sifa ambazo mwandishi huipa kazi yake, yaani mwandishi anaweza kutumia vipengele fulani vinavyoitambulisha kazi yake hivi kwamba mtu anapoisoma anaweza kusema kuwa hii ni kazi ya mwandishi fulani. Kuna mtindo wa kijumla ambao hujitokeza katika kazi za kifasihi kwa jumla lakini pia kuna mtindo maalum au mazoea ya mwandishi fulani ambao huudhihirisha mtindo wa mtu binafsi. Pia tuliona kuwa ili msomaji aweze kusema kuwa hii ni kazi ya mwandishi fulani lazima awe amesoma kazi kadhaa za mwandishi huyo, ili kuweza kutambua vipengele vinavyomsaliti/vinavyoamtambulisha mwandishi huyo.

Kutokana na maoni ya wataalamu tuliowaangazia ilikuwa wazi kuwa mtindo unaomtambulisha mwandishi fulani hujumlisha mambo kadha kama: Hisia za mwandishi, usimulizi, uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi alizotumia, uakifishaji, muundo/mwanzo na mwendelezo wa kazi yake na uchanganyaji wa tanzu mbali mbali. Katika sehemu hii tulifanya uchanganuzi wa vipengele ambavyo vilijitokeza katika tamathali za usemi tulizochunguza na jinsi zilivyodhihirisha upekee wa mwandishi Sanja katika kazi zake nne teule.

#### **4.1.1 Hisia za Mwandishi**

Katika kazi nne tulizochanganua, ilikuwa wazi kuwa mwandishi alidhihirisha hisia zake katika ujumbe wake ambazo zilikuwa: Kusinyika, kukirihika, kuchukizwa na kutofurahishwa.

Mwandishi aliteua mada ya riwaya *Yasinya*. Kusinyika huku kulisababishwa na uongozi mbaya wa viongozi Waafrika. Viongozi kama chifu Kifuja, Chebaskwony, Mayowe, Dkt. Balaa na afisa Angusha walidhihirisha ubinafsi, walijilimbikizia mali ya umma na kusahau wajibu wao kama viongozi. Kupitia mbinu ya jazanda mwandishi aliwalinganisha viongozi hawa na nyangumi, papa, chewa na wana wa Afrika waliokuwa wakifarakanwa wakati walistahili kushirikiana. Kila wakati walikuwa wakipigana kwa sababu ya ardhi, maji, wanyama wa pori, madini na raslimali zingine zilizopatikana Afrika. (uk 73-74) Vitendo hivi vya ubinafsi na ujisadi viliifanya jamii ya Wanamabonde kugawika katika matabaka mawiili: Tabaka la matajiri na la maskini, jambo ambalo ni la kusinya. Nchi ya Mabonde ilikuwa kiwakilishi cha nchi nyingi za Afrika ambako vitendo vya viongozi huisinya jamii na kuilemaza. Waafrika wamelemazwa kwa miaka zaidi ya hamsini, na kufikia sasa bado wanang'ang'ana na maradhi, ujinga, umaskini na uzembe wa kutoungana ili juhudini za kuvuta pamaja zifaalu, kama alivyosema mama M A. (uk 15)

Katika tamthilia ya *Zinguo la Mzuka*, Wanakusinyika walipewa nafasi ya hadhira. Mwandishi alionyesha hisia za kusinyika zilizochochewa na ujinga wa viongozi Mweupe na Zinguo, Viongozi hawa hawakuwa wakitumia madhabahu (uongozi) vizuri kuikomboa jamii ya Wanakusinyika. Wanakusinyika waliudhika kutohadaa Mzuka na Mweupe (wawakilishi wa nchi za magharibi) wakiwahadaa Mzuka na Mweupe (wawakilishi wa nchi za Afrika), na kuifilisi nchi ya Kusinyika raslimali zake hivi kwamba hawakuwa na kitu cha kutoa kafara katika madhabahu yao. Mzuka alikuwa akibeba mali ya nchi ya Kusinya na kuihifadhi kwao kwa minajili ya siku za baadaye. (uk 49) ilikuwa kinaya kuona kuwa badala ya Zinguo na Mweusi kuwazingua Mzuka na Mweupe mambo yalitendeka kinyume Mzuka na Mweupe ndio walikuwa wakiwazingua.

Katika "Mimba Ingali Mimba" mwanamke Nekesa alibeba mimba kwa miaka na mikaka jambo ambalo lilimsinya na pia lingeweza kumsinya mtu ye yeyote. (uk 101) Hali hii ililingana na nchi za Afrika zenye raslimali na utajiri mwingi (mimba) lakini, hazijakuwa zikiwafaidi wananchi wake

kwa sababu ya kukosa ujuzi wa kiteknolojia na tabia ya kuzitegemea nchi za magharibi. Jambo hili lilizilemaza nchi zinazoendelea kwa miaka na mungi, hakuna uzalishaji mali ulioendelea. Kila wakati walitaka kuzalisha mali kwa uongozi wa wakunga (wataalamu kutoka Afrika), madaktari kutoka ughaibuni (wawakilishi wa nchi zilizoendelea) walidai kuwa wakunga hawangeweza kuzalisha kwa kuwa hawakuwa na ujuzi. Madaktari walikuwa wakiomba wapewe muda zaidi wa kufanya majadiliano na matayarisho ya kuzaliwa kwa mtoto (raslimali na utajiri wa nchi hizi). Matayarisho haya yalichukua muda mwingi na kuzilemaza nchi zinazoendelea, hivyo zilibaki nyuma kimaendeleo jambo ambalo liliwasinya Waafrika sana.

Katika “Mwavyaji wa Roho” msimulizi alitumia toni ya kuudhika ambako kulisabishwa na matendo ya viongozi kama Kitambi. Kwa ushirikiano na mpwa wake Jael walifanya biashara ya ulangazi wa madawa ya kulevyta. Matokeo ya biashara hii yalikuwa kuzuka kwa jamii iliyosinyika na iliyotamauka, vijana waligeuka na kuwa waraibu wa mihadarati na walifanya hata tendo la ndoa mchana hadharani kutokana na athari za madawa ya kulevyta. (uk 72-73) Wazazi walisinywa na vitendo vya viongozi hawa na ndiposa mama mmoja aliwarejelea viongozi hawa kama papa na nyangumi. (uk 79)

#### **4.1.2 Usimulizi**

Katika riwaya ya *Yasinya* na hadithi fupi “Mimba Ingali Mimba” mwandishi alitumia usimulizi wa nafsi ya tatu au ya kwanza. Msimulizi huyu hakuwa sehemu ya wahusika bali alikuwa akiripoti yaliyokuwa yakitukia katika jamii ilioangaziwa na mwandishi.

Japo kazi ya tamthilia huwasilishwa kimatendo jukwaani na pia kwa mazungumzo kuna usimulizi unaopatikana katika drama, unaodhihirika katika maelekezo ya jukwaani ambayo huwekwa kwenye mabano. Tamthilia ya *Zinguo la Mzuka* sio tofauti, kila onyesho na tukio lilikuwa katika maelezo yaliyokuwa kwenye mabano ambayo yalitoa maelezo ya mandhari, maleba n.k. Usimulizi katika tamthilia hii ulikuwa katika hali timilifu na wakati uliopo. Katika “Mwavyaji wa Roho”, Sanja alitumia usimulizi wa nafsi ya kwanza, mhusika mmoja (Chumo) katika hadithi alitoa maelezo ya matukio kwa niaba ya mwandishi.

#### **4.1.3 Uteuzi wa Msamiati**

Kazi teule za Sanja tulizochunguza zilisheheni msamiati ulioeleweka na hadhira yake. Maneno aliyyoyateua hayawezni kuorodheshwa katika msamiati changamano, msamiati aliotueua ulieleweka kwa urahisi. Sanja alitumia sajili zinazopatikana katika maisha ya kawaida hivyo lugha yake ilieleweka kwa urahisi. Msamiati aliotumia Sanja uliwatofautisha wahusika k.v. katika “Mimba Ingali Mimba”, mhusika Nekesa alisawiriwa kama asiyekuwa na elimu yoyote kwa sababu hakukimudu Kiingereza, alisema ‘sifolo edukesho’ badala ya ‘*civil education*’. Pia maandishi yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza alisema yalikuwa yameandikwa kwa ‘fotifoti,’ akilinganishwa na madaktari kutoka nchi za magharibi walioimudu lugha.

Katika *Yasinya* mhusika Huni alitumiwa kuelezea sajili ya vijana/mtaani. Siku moja Huni alishikwa na askari kwa sababu alikuwa akipanda bangi, alishikwa na askari Yusi na wenzake alipoachiliwa na akaambowi ahame Mabonde aliwajibu ifuatavyo: “Sawa wazee. Lakini msing’oe aisee. Nikipigisha nitawachotea kitu safi”. Yaani, alisema kuwa ilikuwa sawa, na akawarai wasiing’oe bangi hiyo kwa sababu wakati atauza atawapa pesa za kutosha.

Katika Zinguo la Mzuka mwandishi aliteua maneno ya Kiswahili na Kiingereza. Mweupe alinukuliwa akitumia maneno ya Kiigereza kumkejeli Mweusi: “*what do you know about technology*”.

Kwa jumla mwandishi Sanja alitumia kwa kiasi kikubwa lugha ya Kiswahili na maneno machache ya Kiingereza na Sheng’. Aliwasawiri wahusika wake kama walioimudu lugha ya Kiswahili isipokuwa mifano michache tuliotaja. Hali hii huchangiwa na jamii alimokulia mwandishi au kiwango chake cha elimu.

#### **4.1.4 Muundo wa Kazi**

Kama tulivyoeleza katika sura ya pili hadithi fupi huwa na muundo sahili yaani, wa moja kwa moja kutohana na ufupi wa kazi. Katika “Mwavyaji wa Roho” na “Mimba Ingali Mimba” mwandishi alitumia muundo sahili katika kuwasilisha matukio ambayo yalikuwa yamesimuliwa moja kwa moja. Katika *Zinguo la Mzuka* kulikuwa na mazungumzo au dayolojia yaliyotumiwa na mwandishi ili kujenga mgogoro uliosababishwa na matarajio ya Wanakusinyika kutaka

kuongozwa vyema na viongozi wao Zinguo na Mweusi. Hili halikutendeka kwa sababu Mzuka na Mweupe walikuwa akiwazingua Zinguo na Mweusi, na wakati mwingine kuwalazimisha au kuwadanganya Mzuka na Mweusi hivyo wakaishia kutenda kinyume na matarajio ya Wanakusinyika. Kama tulivyojadili mgogoro katika tamthilia huchukua nafasi kubwa katika kukuza dhamira na maudhui ya mwandishi. Muundo wa riwaya ya *Yasinya* ulikuwa changamano kwa sababu kulikuwa na usimulizi wa moja kwa moja ulioambatanishwa na kisengere nyuma/mbinu rejeshi na kisengere nbele/mbinu elekezi ambazo zilimwezesha Sanja kutoa ufanuzi wa wahusika na mambo aliyoangazia katika kazi hii kwa kina.

#### **4.1.5 Uchanganyaji wa Tanzu Mbali mbali**

Sanja alitumia tanzu mbali mbali katika kazi zake lakini sisi tuliangazia zile zilizohusiana na mbinu ya mtindo hasa kipengele cha tamathali za usemi. Mwanzo alitumia utanzu wa nyimbo, katika Zinguo la Mzuka (uk 25-26) Sichana aliimba wimbo uliokuwa na ujumbe wa kueleza madhila aliyopitia kama Mwanakusinyika na mjakazi wa Zinguo. Alisema alikuwa akifanya ajira badala ya kuwa shuleni, hakuweza kununua viatu kwa sababu familia yake ingekosa chakula, baadaye alibakwa na zinguo na hakuwa na wa kumwokoa.

Katika *Yasinya* (uk 13) mwandishi alitumia nyimbo katika ndoto ya Kijasiri kumhusu mama M A na wanawe. Wimbo wenyewe ulikuwa na maudhui ya kumsifu mama M A pamoja na wanawe. Katika mbinu ya majazi, Kijasiri alikuwa na ujasiri wa kumwandikia mamake barua akiwa gerezani (uk 120), barua hii ilimhimiza mamake asije akasema kuwa Kijasiri alikuwa akiteseka kwa sababu alikuwa mwanamke. Barua hii ilidhihirisha sifa ya ujasiri wa Kijasiri na hata madhila waliyopitia Wanamabonde kutoka kwa viongozi wao akina Kifuja na Mayowe. Kulikuwa na matumizi ya utanzu wa semi: Methali na nahau, katika matumizi ya majazi Asisi alimhimiza Kijasiri kuwa “siku ya kufa kwa nyani miti yote huteleza.” (uk 109) Alikuwa akibashiri kuwa siku moja haki ingetendeka na viongozi fisadi kutupiliwa mbali katika nchi ya Mabonde. Katika (uk 162) Asisi alitumia nahau “wakafumba na kufumbata” kuonyesha jinsi Kijasiri alikuwa mkarimu wa hali ya juu. Kulikuwa methali iliyomrejelea Kipokeo “kinolewacho hupata” (uk 20) alikuwa amepata ujuzi katika biashara ya ukahaba. Kulikuwa na msemo uliotumiwa na msimulizi kuhusu pesa walizoziitisha Mayowe na Kifuja. Walidai kuwa ilikuwa:

“kiasi fulani cha njenje” (uk 130) wananchi walikuwa wakitoa kiasi fulani cha pesa ili kutafutiwa nafasi za kazi.

Katika “Mimba Ingali Mimba” (uk 102) Nekesa aliuimba wimbo uliodhihirisha matumaini aliyokuwa nayo ya kumpata mtoto, (uk 107) alikuwa ametamauka kwa sababu ya kungoja mtoto azaliwe bila mafanikio kwa miaka na mikaka. Mwandishi pia alitumia utanzu wa semi, alitumia maneno kama miaka na mikaka, miaka na dahari kuonyesha jinsi maendeleo ya Afrika yalikuwa yamecheleweshwa kutokana na mvutano wa kimataifa. Kulikuwa na methali: “nyumba ya nyasi haihimili kishindo” (uk 106) kumaanisha kuwa maneno ya Nekesa kwa madaktari kutoka ughaibuni kutaka azalie kwao Afrika hayakusikilizwa. Madaktari ndio waliokuwa na uamuzi wa kujifungua kwa Nekesa. Kulikuwa na methali nyingine, “subira huvuta heri,” baada ya kungoja kwa muda huu wote bado kulikuwa na matumaini ya kuwa na maendeleo katika bara la Afrika.

Katika “Mwavyaji wa Roho” kulikuwa na mdokezo wa methali iliyooanishwa na nahau “hakumlambisha mkono wangu mtupu katika nchi gani?” (uk 72) kuonyesha ufisadi wa meya aliyetaka hongo kutoka kwa mkurugenzi aliyekuwa akizoa taka katika miji mitatu mikuu. Msimalizi pia alitumia nahau ifuatayo: “alitaka nami niuze unga” yaani Jael alimtaka Chumo auze madawa ya kulevya (uk 75). Kulikuwa na methali iliyotumiwa na Chumo kueleza kwa nini alipatiwa nyumba katika mtaa wa Ukwasini, alipatiwa nyumba hiyo ili kuilinda siri ya biashara za Kitambi na Jael. Methali yenewe ni kama ifuatavyo: “mgaagaa na upwa hali wali mkavu” (uk 77)

#### **4.6 Hitimisho**

Kutokana na sifa hizi tulizochunguza ilikuwa rahisi kuutambua mtindo wa mwandishi Sanja ambaa ni wa kijazanda. Kazi zake zilijaa ulinganisho wa watu na vitu ili kuweza kuwasilisha ujumbe wake wa kusinyika. Ilidhihirika wazi katika kazi nne teule tulizochunguza kuwa alikuwa amechukizwa na kusinywa na vitendo vya viongozi dhalimu na fisadi katika bara la Afrika. Katika maudhui yake ilikuwa wazi kuwa Sanja alikuwa na matumaini ya ukombozi na ujenzi wa jamii mpya. Katika uchanganuzi wetu tuligundua kuwa kazi za mwandishi huyu zilisheheni maudhui yafuatayo: Uongozi mbaya, usherati, ajira ya watoto, ukoloni mamboleo, ukoloni mkongwe, ukatili, mahusiano ya kijamii na kimataifa, ukiritimba, ubinagsi, umaskini, utamaushi,

ufisadi, ukabila, njaa, madawa ya kulevyia na athari zake, ujinga, unafiki, utepetevu, mabadiliko, ushujaa, uzalendo, demokrasia na ujenzi wa jamii mpya.

Mwandishi Sanja alitumia mtindo hasa kipengele cha tamathali za usemi kilichochimuza mtindo wa kipekee katika kazi zake. Mtindo huu ulimwezesha kuyazungumzia maswala haya kwa njia isiyotumia maneno makali au ya kuwaumbua walioangaziwa. Kupitia kipengele tulichokichunguza mwandishi aliweza kufikia lengo lake la kuwaelimisha wanajamii, kuwazindua, kuwaonya na kuwaburudisha.

## **SURA YA TANO**

### **HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Katika utafiti wetu tulikuwa na malengo matatu ambayo yalikuwa: Kuchunguza iwapo kuna tofauti za kimtindo katika tanzu tofauti tofauti za fasihi simulizi, kutambua vipengele vya mtindo na hasa tamathali za usemi zilivyotumiwa katika kazi nne teule za Sanja na kudhihirisha upekee wa kimtindo katika kazi nne teule za L. Sanja. Tuliweza kuyaafikia malengo haya na matokeo yalikuwa kama yafuatayo:

#### **5.2 Muhtasari wa Matokeo**

Katika sura ya pili tulichunguza jinsi mtindo hutofautiana kutoka utanzu mmoja hadi mwengine. Tulieleza dhana ya mtindo kulingana na watalamu mbalimbali. Tulitoa maelezo kuhusu mtindo na uhusika wake, yaani mitazamo iliyotolewa na wataalamu kuhusu mtindo, tulieleza mtazamo wa Kiisimu, mtazamo wa Kifasihi, mtazamo wa Kifasihi na wa Kiisimu kwa pamoja na mtazamo wa mtindo kama swala la mtu binafsi. Tulieleza mtindo ulivyodhihirika katika tanzu mbali mbali za fasihi andishi: Riwaya, tamthilia na hadithi fupi.

Katika sura ya tatu tulitambua kuwa mtindo hasa kipengele cha tamathali za usemi zilitumiwa kwa njia mbali mbali kuuwasilisha ujumbe wa mwandishi na kudhihirisha upekee katika kazi nne teule za mwandishi Sanja. Tamathali tulizozichunguza zilikuwa: Majazi, jazanda, kinaya, ndoto/njozi na maswali ya balagha katika vitabu vinne tulivyoviteua. Tuligundua kuwa kazi za Sanja ni za kijazanda, kwa sababu mwandishi alitumia mbinu ya kijazanda kwa mapana ili kueleza jinsi viongozi wa Kiafrika walizifilisi nchi za Kiafrika kutokana na vitendo vyao vya ufisadi, ubinafsi, kutoshirikiana na kuwaruhusu viongozi wa nchi za Magharibi kuzitawala nchi za Kiafrika.

Katika sura ya nne tulidhibitisha upekee wa mtindo wa Sanja katika *Yasinya, Zinguo la Mzuka*, “Mwavyaji wa Roho” na “Mimba Ingali Mimba.” Tulichanganua jinsi kazi ya Sanja ilivyodhihirisha upekee na tukagundua kuwa kazi zake zilidhihirisha hisia za kusinyika,

kukirihika na kutofurahishwa hisia ambazo zilichochewa na jinsi umma ulikuwa ukigandamizwa na viongozi wao nchini Afrika.

Kwa kurejelea nadharia ya Umitindo tulichunguza vipengele ambavyo humtambulisha mwandishi wa kazi fulani. Katika kiwango cha maandishi/grafolojia, tulitambua kuwa Sanja alitumia uhuru wake wa ukiushi kwa kutumia viwakilishi kama alama za Viulizi. Ukiushi huu ulitufaa katika kuichanganua mbinu ya maswali ya balagha, mwandishi aliutumia kimaksudi katika kazi yake. Kupitia maswali ya balagha tuliweza kuupata msisitizo wa mwandishi katika maswala aliyoyaangazia mwandishi. Mwandishi pia alitumia herufi za mlazo/italiki katika kuchanganya ndimi. Pia mbinu hii ilitumika katika tamthilia kutoa maelezo ya mandhari na maleba na hivyo kumwezesha mwandishi kuuwasilisha ujumbe wake vyema kwa hadhira yake.

Katika kiwango cha umbo tulitambua kuwa mwandishi aliteua msamiati uliomwezesha kuuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake, katika kiwango hiki pia tuligundua kuwa alichanganya lugha mbali mbali k.v. Kiswahili, Kiingereza na Sheng'. Kiwango hiki pia kilihusu ukiushi wa uteuzi wa wahusika kwenye kazi hizi. Uteuzi wa wahusika ulituwezesha kuchanganua mbinu ya majazi kwa kiasi kikubwa. Tuligundua kuwa Sanja alipendelea majazi bayana (majina yenye maana wazi). Pia ukiushi huu ulitusaidia kuchanganua mbinu ya jazanda na istiari, wahusika wengi walilinganishwa na wanyama au vitu kutokana na sifa au tabia zao ili kutoa maana ya ndani. Tuliweza pia kuchunguza usimulizi alioutumia mwandishi na mtazamo wake uliotuwezesha kuelewa kuwa hisia zake zilikuwa za kusinyika, kukirihika na kutofurahishwa. Mada alizoteua zilioana na ujumbe katika kazi zake nne teule na pia zililingana na sajili alizozitumia mwandishi katika kazi hizi.

Katika kiwango cha kisemantiki tuliona kwamba, kulikuwa na ukiushi wa kimaana katika matumizi ya tamathali za usemi kama kinaya, majazi, maswali ya balagha pia tulichunguza maana iliyochimuzwa na mbinu nyinginezo za lugha ambazo ni ndoto/njozi na jazanda. Tuligundua kuwa mbinu hizi zilitumiwa ili kuchochea hisia na kumpa msomaji taswira ya hali halisi ya mazingira ya kazi hizi za fasihi.

Katika kutambua ukiushi katika kiwango cha maandishi/grafolojia, kiwango cha umbo na kiwango cha semantiki, nadharia tete zetu za: Mtindo hutofautiana baina ya tanzu tofauti tofauti za fasihi andishi, vipengele vya mtindo vilitumiwa kwa njia anuai katika kazi nne teule za L. Sanja na mtindo wa mwandishi Sanja ni wa kipekee katika kazi zake nne teule zilikuwa za kweli.

Kuhusu umuhimu wa utafiti wetu, tulidhibitisha kuwa ili kueleza mtindo kama dhana ya mtu binafsi sharti mchanganuzi ashughulikie kazi anuai za mwandishi mmoja. Zaidi tuliangazia tanzu mbali mbali za mwandishi mmoja, uchanganuzi ambao haujafanywa na wachanganuzi wengine. Hivyo basi, utafiti huu ulitoa mwanga wa kuchanganua mtindo katika tanzu anuai utakaomwelekeza mchanganuzi katika kueleza mtindo kama dhana ya mtu binafsi. Utafiti huu utawawezesha watafiti wa baadaye kurejelea mchango wa kazi hii kimtindo kama msingi wa utafiti wao.

### **5.3 Hitimisho**

Katika utafiti huu malengo ya utafiti na nadharia ya Umitindo zilituongoza katika kuufanikisha utafiti wetu. Mwandishi Sanja alitumia tamathali za usemi kwa njia yakipekee ili kuuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake. Upekee huu kama tulivyotambua umedhihirika katika hisia anazodhihirisha mwandishi katika kazi zake, usimulizi aliotumia, uteuzi wake wa mamiati, muundo wa kazi zake na uchanganyaji wa tanzu mbali mbali katika kazi zake. Vipengele hivi ndivyo vinazifanya kazi za mwandishi huyu kuwa za kipekee kwa sababu vinamfanya msomaji kutambua vipengele vinavyomsaliti/vinavyomtambulisha mwandishi huyu katika kazi nne tulizoangazia.

### **5.4 Mapendekezo**

Kama tulivyotangulia kusema katika sura ya pili, kazi ya mwandishi mmoja inaweza kufasiriwa tofauti tofauti na wahakiki mbali mbali. Kwa mantiki hii, tulipendekeza kwa vile utafiti wetu ulijikita katika kipengele kimoja cha mtindo ambacho ni tamathali za usemi na upekee wa kimtindo unaodhihirishwa na kipengele hicho. Ni maoni yetu kuwa kazi hizi zitaweza kuchunguzwa zaidi na wachanganuzi kwa sababu hatukushughulikia vipengele vyote

vinayopaswa kuchunguzwa. Wahakiki wa baadaye wanaweza kuchunguza maswala mengine kama vile:

1. Tamathali zingine za usemi k.v. taswira, tataruki, kisengere nyuma, kisengere mbele, takriri, kejeli, chuku, sadfa, tashhisi, tashbihi zilizotumika katika kuwasilisha ujumbe.
2. Vipengele vya mtindo kama vile wahusika, usimulizi, ploti/msuko na mandhari na jinsi matumizi yake yanavyochangia kuendeleza dhamira na kujenga maudhui.
3. Watafiti wengine waweze kutumia nadharia zingine kutafiti vipengele kama wahusika, usimulizi, ploti/msuko na mandhari katika kazi nne teule za Sanja tulizochunguza.

## 6.1 MAREJELEO

- Baldic, C. (2001). *Oxford Concise Dictionary of Literacy Terms*. Oxford: Oxford University Press.
- Collins (1979). *Collins English Dictionary*. Great Britain: Hapercollins Publishers.
- Crystal, D. na D. Davy. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman.
- Flaubert, G. (1964). *Madame Bovary*. France: Penguin Publishers Group.
- Gachohi na Waihiga. (2013). *Kioo cha KCSE Kiswahili*. Nairobi: Target Publishers Ltd.
- Galperin, I. R. (1981). *Stylistics*. Moscow: Moscow State Linguistic University Press.
- \_\_\_\_\_. (1981). *Text as an Object of Linguistic Studies*. Moscow: Nauka
- Ebrahim, H. (1969). *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.
- Katutu, R. M. (2013) *Mtindo katika Diwani ya ‘Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine.’* Tasnifu ya Uzamili (M.A). Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Kitali, H. N. (2011). *Fani na Usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Pango na Mama Ee*. Tasnifu ya (M.A). Chuo kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Kitsao, J. (1975). *A stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts*. Tasnifu ya Uzamili (M.A). Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Kitula, K. (2013). *Miali ya Insha: Shule za Upili*. Nairobi: East Afrika Education Publishers Ltd.
- Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.
- Leech, G. N. na Short, M. (1981, 2007). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. 2<sup>nd</sup> Edition Harlow: Longman Group Ltd.
- Mbatia, M. (Mh). (2000). *Mwenda wazimu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- \_\_\_\_\_. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics & Publishers.
- Mugenda na Mugenda. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Act Press.
- Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi: Mulika*. Dar-el-Salaam. TUKI.
- \_\_\_\_\_. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar - es - Salaam: Chuo Kikuu cha Dar - es - Salaam.

- Ndung'u, N. (1996). *Uhakiki wa Fani katika Riwaya za Katama Mkangi: Ukiwa, Mafuta na Walenisi*. Tasnifu ya M.A, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ongarora, S.O. (2007). *Mtindo katika 'Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.'* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.
- Otieno, N. O. (2005) *Muumano wa Leksia katika Matini: Babu Alipofufuka*. Tasnifu ya M.A, (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Sanja, L. L. (2006). *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*, katika McOnyango, (mhr). Nairobi: Focus Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2011). *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*, katika Sanja Leonard Leo (mhr). Nairobi: Focus Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2011). *Zinguo la Mzuka*. Nairobi: Focus Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2014). *Yasinya*. Nairobi: Focus Publishers.
- Saussure, F. (1983). *Course in General Linguistics* (Trans. Roy Harris) London: Duckworth.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar - es - salaam: Press and Publicity Center.
- \_\_\_\_\_ (2011). *Fasihi*. Dar - es - Salaam: KAUTU Ltd.
- Simpson, P. (2004). *Stylistic: A Resource Book for Students*. London: Routledge.
- Spitzer, L. (1948). *Literature: Modern History and Criticism*. Princeton, NJ: Princeton Univ. Press.
- TUKI. (2006). *Kamus ya Kiingereza – Kiswahili*. Toleo la Tatu. Dar-es-Salaam: TUKI.
- Wafula, R. na Kimani, N. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: focus Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide - Muwa Publishers.